ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri waMiundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae

30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope

54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid Jimbo la Kiembesamaki

55.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

57.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane - Tarehe 22 Oktoba, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika: (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: (kny) Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Kukinga na kusimamia masuala ya Ukimwi Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu wanaoishi au Walioathirika na Virusi vya Ukimwi na Mambo mengine yanayohusiana na nayo.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani ya Mswada unaohusu Maswala ya Sheria ya Kurekebisha Amri ya Barabara sura 134 na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 26

Ukarabati wa Mitaro Iliyobomoka

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny) Mhe. Jaku Hashim Ayoub:- Aliuliza**:-**

Kwa kuwa Baraza la Manispaa Zanzibar lina wajibu mkubwa wa kuweka Mji wa Zanzibar safi na kuchukua hatua kwa mambo yanayohatarisha usalama wa Afya za wananchi na maisha yao.

(a) Je, Baraza la Manispaa limechukua hatua gani kuhusu mitaro iliyojengwa ambayo imeanza kubomoka hasa katika eneo la Kisima Majongoo kuelekea Kikwajuni?

(b) Je, ni lini Baraza la Manispaa kwa mara ya mwisho limefanya ukarabati huo tangu kukamilika kwa ujenzi wa mitaro hiyo Mjini Zanzibar?

(c) Kwa kuwa mitaro hiyo katika baadhi ya maeneo imekuwa kero kutokana na kugeuka kuwa mazalio ya mbu na kutishia usalama wa wananchi wa maeneo yaliyokumbwa na tatizo hilo, ni hatua gani za haraka zitachukuliwa kukabiliana na hali hiyo?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:- Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 26 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo. Lakini kwanza naomba kutoa maelezo yafutayo:-

Mhe. Spika, Jukumu la kuweka Mji wa Zanzibar katika hali ya usafi linasimamiwa na Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na wakaazi wa mji huu wakiwa katika vikundi au mtu mmoja mmoja. Baraza la Manispaa limekuwa likifanya juhudi kubwa ya kukusanya taka na kusafisha Mitaro na ukarabati wa Miundo Mbinu inayohusika na usafirishaji wa maji machafu na sehemu za kutupa taka. Lakini kumekuwa na muamko mdogo kwa baadhi ya wananchi kutokufuata taratibu na miongozo iliyopo ya kuweka mji wetu katika hali ya usafi.

Baadhi ya wananchi wamekuwa wakitupa taka katika Mitaro ya maji na hivyo kusababisha kuziba. Aidha baadhi yao wamekuwa waking'oa mafuniko ya Mitaro na kuyauza.

Mhe. Spika, baadhi yao wamekuwa pia wakifanya biashara katika maeneo ambayo hayakupangwa kufanyia biashara na kutupa taka zinazotokana na biashara hizo katika sehemu ambazo hazikutengwa kwa utupaji wa taka za aina hiyo. Hivyo kupelekea uchafuzi zaidi na ugumu wa uzoaji taka. Hivyo nachukuwa fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wengine kwa ujumla tushiriane kuelimishana juu ya kufuata taratibu na sheria ziliopo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake namba 26 lenye vipengele (a,b na c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Baraza la Manispaa limechukuwa hatua za kusafisha Mtaro huo na kuyabadilisha mafuniko yaliokatika kwa kuyaweka mapya kazi hiyo imeanzia katika eneo liliopo Benki ya *FMD* na kuelekea Kisima Majongo hadi Michenzani *block 10*.

(b) Mhe. Spika, kazi za usafishaji na ubadilishaji wa baadhi ya mafiniko kwa mara ya mwisho imefanyika mwezi mmoja na nusu na imesimama kwa muda kutokana na kuhitaji kwa gari ya kubebea vitu vizito ambalo litasaidia kuyanyanyua mafuniko.

(c) Mhe. Spika, Baraza la Manispaa linaendelea na hatua zake za kuifanyia usafi Mitaro hiyo na mengine kwa lengo la kuimarisha usafi na kuondokana na maradhi yanayoweza kusababishwa na kutuwama kwa maji ikiwa ni pamoja na kugeuka kuwa mazalio ya mbu. Aidha katika kuhakikisha kwamba suala hilo la usafi linazidi kuwa endelevu Baraza linakamilisha mipango yake ya uanzishaji wa vikundi vya usafi kwa kila shehia na kazi hiyo itaanza ndani ya mwezi huu wa Oktoba mwaka 2013.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba kuna wafanyabishara ambao huwa wanatupa taka katika maeneo yalioko karibu na Mitaro ambayo inasababisha Mitaro hii kuziba.

(a) Nataka Mhe. Waziri anijibu kwamba kwa kuwa wafanyabiashara wale huwa wanakata leseni za kuzolea taka. Sasa ni nani mwenye jukumu la kusafisha ule mji baada ya kumaliza biashara zao, ni Baraza la Mji ambalo linakata fedha wafanyabiashara wale kwa ajili hiyo au ni wafanyabiashara wenyewe wazoe taka zile?

(b) Kwa sababu Manispaa ya Mji huu ni uso wa Zanzibar na kuwa Mtaro si wenye *systerm*, mji mzima haipendezi, hususani katika kipindi cha mvua sio tu kwa kuhatarisha afya sisi Wazanzibari. Lakini ni aibu hata kwa wageni wanapotembelea katika mji wetu huu ambapo *first step* huwa ni hapa *Zanzibar town*.

(c) Je, Mhe. Spika, kwa kuendelea na khulka hii ya kutunza uchafu kwa Mitaro ya mji huu Unguja Mjini, huoni ni kwamba ni kulitia aibu Taifa letu hii la Zanzibar na

vile vile kurudisha nyuma biashara zetu za utalii, kwa sababu watalii hawatakuja katika mazingira machafu ya kama yale?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

(a) Mhe. Spika, ni kweli Baraza la Manispaa linakatisha leseni kwa wafanyabiashara ambao wapo kisheria. Lakini kama nilivyojibu suali langu mama wanaoharibu ni wale ambao hawakati leseni kwa sababu wapo katika maeneo ambayo hayakuruhusiwa kisheria na hayo maeneo ambayo hayakuruhusiwa kisheria huwa hayatozwi leseni.

(b) Ni kweli Mitaro haipendezi kwa wageni lakini Mitaro haipendezi hata kwa wenyeji na haipendezi kutokana na tabia yetu sisi baadhi ya wananchi tunaotupa taka katika Mitaro hiyo na kusabisha maji yasiende katika mtiririko wake. Kuna matatizo mengi Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu mama katika eneo hili. Lakini nadhani ni kuchukuwa nafasi ya kuweza kueleza matatizo ambayo nimeyaona mimi mwenyewe asubuhi hii kuanzia saa 1:30 mpaka saa 2:03 nimetembelea baadhi ya Mitaro nimeona matatizo mengi.

Sasa kwa kueleza taarifa ambazo nimeziona katika hayo matatizo kwa kujibu suali hapa nafikiri Mhe. Spika, ninaweza nikachukuwa muda mrefu sana. Lakini matatizo ni mengi na kama nilivyosema kwenye jibu mama matatizo haya yanasababishwa na baadhi yetu sisi wananchi kuwa na tabia mbaya ya kufanya mambo kinyume na utaratibu na kinyume na sheria ya nchi hii.

(c) Sioni kwamba hali hiyo ikiendelea ni kusababisha kupunguza haiba ya Sekta yetu ya Utalii naiona ni kweli kabisa kama hiyo hali itaendelea basi tutasababisha kupungua haiba ya utalii katika mji wetu wa Zanzibar. Lakini mimi kama waziri nitahakikisha ninalisimamia Baraza la Manispaa ili liweze kutekeleza wajibu wake.

Lakini vile vile kama niliovyosema, sisi wananchi na viongozi tunatakiwa tuchukuwe jukumu kubwa sana la kuelimishana ili hayo matatizo ambayo yanajitokeza yasiweze kujitokeza ili utalii uendelee kuwa ni sekta muhimu ya

kuchangia pato la taifa na tusiwavunje moyo wageni ambao wanatembelea hapa Zanzsibar.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametuwezesha kuwemo humu katika hali ya afya na uzima.

Mhe. Spika, kutokana na Sensa ya miaka ya nyuma iliyopita tulikuwa watu wanaofika kama laki tatu au laki nne. Lakini kutokana na Sensa ya hivi sasa Mhe. Spika, tuko watu kama milioni moja na laki tatu na kwa kuwa miji yetu kwa mikoa yote mitano ni miji ambayo iliyokuwa sehemu mbali mbali kwa uvamizi wa wananchi na kwa kuwa kujenga kwetu tunajenga kiholela holela.

(a) Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba imefika wakati sasa hivi kwa wakati huu kushirikiana na Wizara ya Majenzi? Wizara ya Mazingira na Wizara nyengine ambazo zinahusika na mambo mbali mbali ya uvamizi wa uhamiaji holela. Kushirikiana ili kuhakikisha kwamba sasa hivi ni kufanyiwa *survey* kwa Mikoa yote mitano na kuweka mazingira bora ambayo yataweza kuwasaidia wananchi wetu katika kuondoa uchafu Mitaro ya aina hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Asha Bakari Makame ambaye yeye ni Makamo Mwenyekiti wa wake zetu suala lake la nyongeza.

Kwanza nakubaliana na Mhe. Asha Bakari Makame kwamba kweli kuongezeka kwa idadi ya watu ndani ya mji kunachangia sana kuleta uchafuzi wa mazingira hasa pale panapokuwa hapana mashirikiano au hapajawekwa mikakati madhubuti kati ya taasisi zinazohusika na kuendeleza miji yetu.

Ni kweli kabisa hivi sasa ndani ya Mji wa Zanzibar, Mjini Magharibi kuna watu wasiopungua laki tano na ushee hapo nyuma haikuwepo idadi hii. Kwa hivyo, lazima kuna mparaganyiko wa mambo.

Lakini serikali hivi sasa iko katika shughuli za kupanga mji wetu upya kupitia Idara ya Mipango Miji. Kwa hiyo, hapo itakapokuwa imekamilika basi hizi taasisi zote ambazo Mhe. Asha Bakari Makame amezitaja pamoja na zile ambazo hajazitaja zitakuwa zinashirikiana kikamilifu hasa wakati zinapotoa vibali vya ujenzi wa nyumba ndani ya mji wetu, ili kuepusha hayo madhara ambao tunayopata sasa na yasiendelee kupatikana huko tunakokwenda.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona na kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba jimbo la Kikwajuni ni jalala la maji yote machafu yanayotoka katika maeneo mbali mbali katika mji wetu wa Zanzibar?

(b) Uongozi wa Jimbo la Kikwajuni katika mwaka 2011 tuliufanyia kazi Mtaro huu ambao umekwenda kuuangalia sasa hivi na tatizo la Mtaro ule sio taka kama ambavyo ulikuwa umeeleweshwa. Tatizo la Mtaro ule ni mchanga ambao unatokana na maji machafu ambayo yanatoka maeneo mbali mbali na yanakuja kufika pale na kwa sasa hivi Mtaro ule umejaa michanga ambayo hayo maelengo yake yaliokuwa yamekusudiwa hayawezi kupatikana sasa hivi, kwa sababu umekuwa haufanyi kazi yoyote?

(c) Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kufuta Mtaro ule na kuweza kufanya utaritibu mwengine ili maji yaweze kwenda vizuri na salama katika eneo la Kikwajuni?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni suali lake la nyongeza.

Kwanza nataka nikubaliane na maoni yake ya kusema kwamba ule Mtaro sasa hivi ni mchafu mno kama nilivyosema, asubuhi hii kuanzia saa 1:30 mpaka 2:03 niliutembelea mimi mwenyewe ule Mtaro nikifuatana na watendaji wangu wa Baraza la Manispaa na nimeona hali halisi ya Mtaro ule. Kwa hivyo, naelewa na kabla ya leo nilikuwa napita katika maeneo yale naona hali halisi ilivyo.

Lakini Mtaro ni kweli umejengwa kama nilivyosema kuna matatizo mengi matatizo yaliopo katika Mtaro ule hata katika ujenzi wake kuna makosa ambayo yamefanywa na Mkandarasi na makosa ambayo sisi wenyewe wakati tunatoa cheti cha mwisho kwa mkandarasi itakuwa hatukuangalia vyema.

Kwa maana hiyo yapo matatizo ambayo yanasababishwa na ujenzi wa ule Mtaro wenyewe.Lakini nadhani si jalala la maji machafu kwa sababu Mtaro ule

unatoa maji kutoka *Block* nambari 10 na unatakiwa vile vile pale kwa Mzee Skachi kuna Mtaro ambao ulikuwa uunganishwe lakini haikufanyika kazi hiyo.

Lakini jambo jengine linalosababisha uchafu wa Mtaro ule ndio lile nililosema mwanzo bado kuna tabia ya baadhi ya wananchi tunafanya mambo kinyume na utaratibu, wapo wananchi ambao karo zao za maji machafu wameziunganisha na Mtaro ule. Wako wananchi ambao wanavunja mafuniko yale kwa kuweka magari yao tena magari yenyewe mazito, kwa hiyo zile *culvert* zinatumbukia ndani ya Mtaro ule na hatimae maji yanakuwa *blocked* yanakuwa hayaendi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, kuna matatizo mengi sana ambayo yanasababishwa kama nilivyosema hapo mwanzo. Lakini vile vile Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni mmechimba visima. Visima vile havitumiki kwa kusaidia watu maji tu. Lakini pembeni ya visima watu wanafua wanakoga na maji yanaingia mle.

Kiutaratibu ukichimba kisiwa na kukiwa na mfereji wa nje unatakiwa utengeneze karo pembeni ili yale maji yanayotumika pale yaingie kwenye karo na sio kwenye Mtaro ndio maana nikasema na sisi Waheshimiwa Wawakilishi lazima tulikubali hili kwamba tunawajibika, twende tukalifanyie kazi pamoja na nia njema ambayo tumeionesha kwa kuwasaidia wananchi wetu.

Serikali ina mpango gani, kwa hatua za dharura nimemuagiza Mkurugenzi wa Baraza la Mji kaunzia wiki ijayo atafute gari kwa sababu gari letu limeharibika na vipuri vyake kulitengeneza ni gharama kubwa sana na magari ambayo tumeyapokea kwa mradi bado hatujaidhinishiwa kuyatumia.

Kwa hiyo, nimemuagiza akodi gari yafunuliwe yale mafuniko yote pale ili ifanyike *Operation* kuweza kuusafisha Mtaro ule. Lakini hata tukifanya hiyo *Operation* ni lazima sisi wananchi na viongozi tukubali kuelimishana na turekebishe tabia ili Mtaro ule uendelee kuwa endelevu na uendelee kuwasaidia kuwepo na usafi wa mji wetu kama ulivyokusudiwa.

Nam 64

Kupatiwa Makoti ya Uokozi Vikundi vya akina Mama

Mhe. Saleh Nassor Juma- Aliuliza:-

Kwa kuwa Dira ya Maendeleo 2020 na Mpango wa SMZ wa kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi (MKUZA) malengo yake makubwa ni kuongeza kipato cha wananchi pamoja na kupunguza umasikini. Kwa kuwa akinamama wengi wamejikita katika kilimo cha mwani, chaza na uvuvi wa madagaa, jambo ambalo huwalazimisha kufata mazao yao kwenye kina kirefu cha maji hususan katika kipindi cha maji mafu (*low tide*) huku wakiwa hawana vifaa vya uokozi (*life jackets*).

(a) Je, ni lini Serikali itafikiria kutoa misaada ya makoti ya uokozi hayo kwenye vikundi vya akinamama?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Alijibu**:-**

Kwanza kabisa, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi ya kwamba Dira ya Maendeleo 2020 na Mpango wa SMZ wa kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi (MKUZA) malengo yake makubwa ni kuongeza kipato cha wananachi pamoja na kupunguza umasikini.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake nambari 64 kama ifuatavyo:-

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo tayari wakati wowote itakapopata uwezo wa kifedha kusaidia wajasiriamali wa mazao ya baharini, wakiwemo wakulima wa mwani, chaza, kaa na samaki kwa kuwapatia vitendea kazi na vifaa vya uokozi.

Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Mradi wa *MACEMP* iliwasaidia vifaa na makoti ya kuokolea maisha (*Life Jackets*) wajasiriamali mbali mbali wa Unguja na Pemba. Kwa mfano, upande wa Unguja ni kiongwe, Ngambwa, Kizimbani na Kizingo na kwa Pemba ni Tumbe, Kisiwa Panza, Fundo na Makangale.

Hivyo, Wizara yangu pindi itakapopata uwezo wa kifedha tutaendelea kuwasidia wajasiriamali wa mazao ya baharini.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa akina mama hawa wana jitihada sana na kwa kweli napenda kuwapongeza sana jinsi wanavyojishughulisha na mambo haya kwa nchi nzima napenda sana kuwapongeza.

Kwa kuwa zana wanazotumia ni zana hafifu, ni lini hasa serikali itatoa ruzuku au msaada kama vile *Life Jackets* kwa akina mama hawa wanaolima mwani katika maeneo ya Kijini pamoja na Mzuri sehemu za Makunduchi kule, Makombeni ni lini watawasaidia hizi *diving foot* na halkadhalika hawa akina mama wanaochokoa pweza katika maeneo ya Vitongoji pale Umangani, Jengoni?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Spika, ni kweli na kwenye jibu mama nimeeleza tutawasaidia pale wizara yangu itakapopata fedha ili kwenda na wakati na kwa sababu nafikiri mimi na wewe tulifanya matembezi ya pamoja tukaona ugumu halisi uliotokea kwa wananchi wale. Kwa hivyo, nataka kutoa tamko mbele ya Baraza lako tukufu kuwa wizara yangu itakapopata fedha itawasaidia wananchi wale kwa sababu imewaona na kazi zao ngumu zilizotokea kule.

Nam 65

Msaada kwa Wavuvi kwenye bei ya Samaki

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Alijibu:-

Naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi suala lake nambari 65 kama ifuatavyo:-

Kabla ya kumjibu kwanza kabisa nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa asilimia kubwa ya Zanzibar wanategemea sana sekta ya uvuvi kwa maisha yao, na kwa kuwa bei ya mazao ya baharini hupanda na kushuka kulingana na uzalishaji kwa vile katika kipindi cha usiku wa kiza wavuvi wa dagaa huvua madagaa mengi kiasi cha kuzidi masoko yote. Jambo ambalo huteremesha sana bei ya bidhaa hiyo.

Serikali kwa kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kuwasaidia wazalishaji wa bidhaa za baharini kwa kuweza kuifanya bei ya samaki kuhimili vishindo vya uzalishajikama.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imeweza kusambaza mafriza katika maeneo mbali mbali yenye masoko Unguja na Pemba kwa lengo la Kuwasidia wavuvi wa samaki kuhifadhi samaki katika kipindi ambacho bidhaa ya samaki hukosa soko na kupelekea kuepukana na kuuza bidhaa hio kwa bei ya hasara.

Aidha wizara yangu kwa kupitia Idara ya Mazao Baharini inaendelea na juhudi za kutoa taaluma ya usarifu wa uhifadhi wa dagaa wakati wa kulianika kwa lengo la kuongeza ubora wa thamani ya bidhaa hiyo. Hivi sasa dagaa jingi kavu linasafirishwa nje ya Zanzibar kama vile Tanzania Bara na Congo.

Mfano mwaka 2010 jumla ya tani 6.20 za dagaa kavu zenye thamani ya shilingi milioni tatu na laki zimeshasafirishwa nje ya Zanzibar.Mwaka 2011 tani 23.36 za dagaa kavu lenye thamani ya shilingi za kitanzania milioni kumi na nane laki moja thamanini na tisa

na mia mbili limesafirishwa nje ya Zanzibar. Mwaka 2012 jumla ya tani 123.98 za dagaa kavu zimeshasafirishwa lenye thamani za shilingi milioni thamanini, laki saba, ishirini na mbili elfu zimesafirishwa nje ya Zanzibar.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza niipongeze serikali kwa bidii yake kubwa kwa kuweza kushajihisha usafirishaji wa dagaa nje ya nchi.

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa samaki wanaovuliwa kule si dagaa tu na kuna samaki wa minofu wanapatikana lakini nalo soko ni tatizo na kwa kuwa serikali haina uwezo wa kuweka *cold rooms* kwa kila eneo la Diko, ni lini serikali itawashajihisha wafanyabiashara badala ya kujikita zaidi katika masuala ya utalii, waeke viwanda vya minofu kama ilivyo Kanda ya Ziwa kule Tanzania Bara ili kuweza kusindika minofu. Kwa sababu hii itasaidia kufanya *demand* iwe kubwa na *price* iendelee kuwa *stable* au iweze kupanda, *that's (a).*

(b) Kwa kuwa dagaa ni moja katika *component* za kutengeneza chakula cha kuku, ni lini Serikali yetu hii ya SMZ itawashajihisha wafanya biashara ambapo hata humu wapo akina Mhe. Ali Salum na Mhe. Raza pale, kutengeneza viwanda vya vyakula vya kuku kusudi waweze kulinunua dagaa hili badala ya kulipeleka nje ya nchi tuweze kulinunua hapa hapa na badala ya kaagizishia kuku wale wa mapaja makubwa tuzalishe hapa hapa?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi, ninadhani katika bajeti yetu tulizungumza kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuwa tumepata wataalamu sasa kuweza kuzungumza nao na kuweza kuweka viwanda vya kusindika samaki hapa nchini petu. Lakini mazungumzo bado yanaendelea na bado hatujafikia mwisho.

b) Ni lini tutaweza kuwashajihisha kuweka chakula cha kuku. Sera ya serikali yetu ni biashara huria, ipo wazi na kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko itashajihisha wananchi wake na kuweza kuweka viwanda hivi kwa kuzalisha chakula cha kuku.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwakilishi viwanda vidogo vidogo vya kutengeneza kuku Zanzibar vipo na si ghali havihitajii sana awe lazima Mr. Raza, na kwamba wewe uwe ni mfano kwa Jimbo la Wawi.

Weka kiwanda cha kuku, vyote gharama yake ya mashine ni milioni, uwezo huo unao. Naomba uweke kitega uchumi hicho. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa wananchi wengi katika Wilaya yangu ya Mkoani hujishughulisha na uvuvi wa dagaa, lakini hushindwa kulisarifu dagaa hilo kutokana na kukosa utaalamu wa kulisarifu. Je, Mhe. Naibu Waziri huoni ni vyema kuwapatia utaalamu ili waweze kupata tija ya dagaa? Ahsante sana Mhe.Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:-

Wizara yangu itafanya juhudi kubwa ya kufika kama ilivyofika katika mkoa wako ili kukupatia wataalamu na kuweza kukusaidia katika utaalamu wetu ambao utasaidia wananchi hawa kukuza kipato na kupata utaalamu zaidi wa kuanika dagaa.

Mhe. Spika: Naomba Waheshimiwa Wajumbe tuendelee.

Nam. 84

Ukosefu wa Huduma ya Maji kwa Wananchi wa Bwejuu

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Pamoja na jitihada kubwa za Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kuwasaidia wananchi kupata maji ya uhakika bado kuna maeneo ya Bwejuu jitihada hizo hazijazaa matunda kutokana kutoungwa mkono na Mamlaka ya Maji.

Jee, lini Mamlaka ya Maji (ZAWA) itaunga mkono juhudi za Mwakilishi na Mbunge wa Muyuni kuwapelekea wananchi wa Bwejuu maji safi na salama**?**

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu**:-**

Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Na. 84 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kijiji cha Bwejuu ni miongoni mwa vijiji 9 vya Unguja na Pemba vilivyobahatika kupatiwa huduma ya maji safi na salama kupitia mradi wa *AFDB* katika miaka ya tisini. Hata hivyo kutokana na ongezeko la idadi ya watu pamoja na ukuaji wa sekta ya utalii kunakosababisha matumizi makubwa ya maji, baadhi ya vijiji vyengine huduma hiyo haipatikani vizuri.

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na jitihada za kuwasambazia wananchi wa mjini na vijijini huduma ya maji safi na salama kikiwemo Kijiji cha Bwejuu. Miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na kushirikiana na Mhe. Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni.

Hata hivyo hivi karibuni kumejitokeza hitilafu ya kuungua *pump* iliyokuwepo na kwa jitihada ya Mamlaka ya Maji wamefunga *pump* nyengine mpya ambayo ilikuwa na kiwango kidogo kulinganisha na *pump* iliyokuwepo hapo awali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mhe. Mwakilishi na Mbunge wa Jimbo la Muyuni wamejitahidi sana kupeleka maji katika eneo kubwa la jimbo lile na kwa kuwa umekiri kuwa *pump* imeharibika na imetengenezwa, lakini kwa taarifa tulizonazo kwamba ni Mbunge na Mwakilishi wa jimbo ndio waliotengeneza ile *pump*.

Jee, serikali ilichangia kiasi gani katika kutengeneza *pump* ile?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza tunawashukuru Mbunge na Mwakilishi kwa jitihada zao na kushirikiana na Mamlaka ya Maji kwa kuliondoa tatizo kubwa la upatikanaji wa maji katika kijiji hiki cha Bwejuu.

Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ilichokifanya ni kufunga *pump* nyengine ambayo kama nilivyoeleza kwamba *pump* hiyo ilikuwa ndogo, lakini kwa sasa hivi Mamlaka ya Maji tayari imo katika jitihada ya kutafuta *pump* nyengine kubwa ambayo italingana na uwezo wa matumizi na mahitaji ya wananchi wa kijiji hicho.

Tukijaaliwa tunategemea *pump* hiyo si muda mrefu itapelekwa katika maeneo hayo ya kijiji cha Bwejuu.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri tu.

Mhe. Spika, mimi swali langu ni dogo sana.

Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake kasema kwamba malengo ya wizara ni kusaidia kupeleka huduma ya maji mjini na vijijini. Lakini ninataka nimuulize kwamba mara nyingi pamoja na jitihada hizo kunakuwa kunajitokeza matatizo ya upasukaji wa mabomba ya hayo maji na inapelekea muda mrefu kutokushughulikiwa hata pale taarifa zinapopelekwa katika Mamlaka ya Maji.

Jee, ni sababu gani za msingi zinazopelekea kutokufanya uharakishaji wa utengenezaji wa mabomba yao na kupelekea kupotea kwa maji ovyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba huwa kunajitokeza upasukaji wa mabomba ya kusambazia maji katika maeneo mbali mbali. Hayo niseme ni mambo ya kawaida kwa sababu ile ni miundombinu ambayo kama miundombinu nyengineyo. Lakini wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji hulisimamia suala hilo la utengenezaji wa mabomba hayo mpaka kukamilika na kwa sasa hivi tunapopata taarifa tu, basi Mamlaka ipo makini na kufuatilia shughuli hizo kwa ajili ya kuwapatia wananchi huduma hiyo ya maji safi na salama.

Mhe. Salmin Awadhi Salmin: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, alipokuwa akijibu swali la msingiMhe. Naibu Waziri alisema kwamba lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwapatia wananchi wake maji safi na salama, mjini na vijijini. Na kwa kuwa mradi ule ambao alioutaja umepeleka maji katika maeneo ya Bwejuu na Paje, pia umepeleka maji katika eneo la Makunduchi.

Sasa tangi lile lilitiwa kule Makunduchi la mradi huo hivi sasa limekuwa likivuja na halitumiki. Jee, serikali kupitia lengo lake lile lile la kupeleka maji safi na salama mjini na vijijini, ina mpango gani wa kulitengeneza lile tangi liliopo pale Makunduchi ili wananchi wa Kijiji cha Makunduchi wapata maji?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba tangi la Makunduchi ni bovu na wizara yangu inalijua hilo. Kwa jitihada ya wizara yangu ina mpango wa kujenga tangi jengine ndani ya Kijiji cha Makunduchi, kwa sababu tangi lililokuwepo ni tangi ambalo limejengwa kwa sandarusi na tukiangalia katika utafiti tuliofanya matangi mengi yaliyojengwa katika mfumo ule

sasa hivi kwa kweli yana matatizo na utengenezaji wake hata kama utayatengeneza kwa muda mdogo tu basi yanarejea katika hali ile ile.

Mpango tuliouwandaa ni kwamba kuweka matangi mapya katika maeneo yote ambayo tumejenga matangi ya aina hiyo na matangi hayo yakawa tayari yameshafanya matatizo

Na. 50

Uwekaji Kifusi Barabara ya Mto-Mkuu

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Katika ujenzi wa barabara za vijiji (Mkoa wa Kaskazini Pemba) Kampuni ya *H Young* ilitanua barabara kwa ajili ya kuchimba kifusi katika eneo la Mto-Mkuu na barabara ikabakia bila ya kuwa na kifusi jambo ambalo imesababisha isiweze kupitika tena kwa kupoteza kifusi kilichokuwepo.

Jee, kwa nini hadi hii leo barabara ile haijatiwa kifusi ikaa inatumika kama ilivyokuwa kabla ya Kampuni hii ya *H Young* kuchimba kifusi hicho?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 50 kama ifuatavyo?

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba Kampuni ya H Young Limited ya Kenya ndio kampuni iliyoshinda zabuni ya ujenzi wa barabara tano kwa ajili ya kuimarisha maendeleo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Barabara hizo kwa ujumla zina urefu wa kilomita 35 ambazo zitajengwa kwa kiwango cha lami. Mdhamini mkuu wa mradi huo ni Shirika la Maendeleo la Marekani na matarajio yetu kuwa mradi huu utakamilika na barabara zitakuwa zenye viwango.

Katika ufanikishaji wa mradi huo bila shaka yoyote italazimika baadhi ya vifaa na huduma zitoke hapa hapa nchini kwetu.

Mhe. Spika, *yumkin* suala zima la kifusi, mawe, michanga ya kupikia lami kwa dhumuni la kupunguza gharama zitapatikana maeneo ya karibu na shughuli hizo za ujenzi zinapofanyika. Jambo la msingi la kuzingatia ni taarifa za kiathari za kimazingira na mambo mengine kama hayo kuyazingatia katika utekelezaji wa mradi husika.

Hadi muda huu takriban asilimia 77 ya kazi za mradi huo zimeshafanyika na mradi unakwenda kwa kasi ya kuridhisha.

Majibu

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Kampuni ya H Young ilifanya matengenezo kwa kuitanua sehemu ya barabara hiyo na kuitia kifusi ambapo kilipatikana katika maeneo ya mlimani baada ya daraja la Mto-Mkuu kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Bahanasa, Daya Mtambwe. *Yumkin* sehemu hiyo ya mlimani kwa hivi sasa imeharibika kidogo.

Mhe. Spika, wizara tayari imewasiliana na mkandarasi huyo ili ayafanyie matengenezo tena kwa kuzitia kifusi sehemu zote zilizoharibika kabla ya kukabidhi kwa mradi huu.

Na ni kweli Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi amefanya mazungumzo ya kina na wakandarasi hao na mazungumzo hayo yameleta tija.

Mhe. Spika, ninapenda kulihakikishia Baraza lako na Mjumbe wako kwamba mazungumzo hayo yaliyofanyika wizara yetu tutayaratibu na kuona yanatekelezwa kwa vitendo kama vile ambavyo wamekubaliana.

Mhe.Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa pongezi za dhati kwa majibu niliyopata kutoka kwa Mhe. Naibu Waziri.

Lakini Mhe. Spika, nimeleta swali hili kutokana na kuwa wale watu waliokuwepo mwanzo wakati njia ile wanataka kuipara ili kwenda kuchimba hicho kifusi walikubali kuifanya hiyo kazi, lakini kwa sababu kulitokea mabadiliko wakaondoshewa wale wapya waliokuja ilikuwa taarifa hii hakuna na sisi hatukuandikiana kuhusiana na suala hili.

Kwa hivyo, ninahofia kwa sababu barabara nzuri hizi zinazojengwa zitamalizika hivi karibuni na sijaona ishara yoyote ya matengenezo, kama Mhe. Naibu Waziri ameshasema kuwa wameshakaa, wamekaa lini na kazi hii itaanza lini kwa sababu ikinyesha mvua siku moja tu ile barabara haipitiki tena na ni barabara muhimu sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha wiki mbili zilizopita nyuma mimi mwenyewe binafsi nilifanya ziara tukakutana na uongozi wa Kampuni ya H Young, miongoni mwa mazungumzo yetu ni pamoja na hili na yeye Mhe. Mwakilishi tulimuarifu hivyo.

Naomba nimuhakikishie kwamba pamoja na jitihada nyengine Kampuni ya H Young inataka kuhakikisha kwamba miradi ya barabara tatu ambazo zinagusa sehemu kubwa ya jimbo lako, inataka kuhakikisha kwamba katika mwezi wa Disemba wawe wametukabidhi.

Kwa hivyo, tulichokubaliana ni kwamba waharakishe kazi za kumaliza barabara zetu zile tatu ili sasa wapate nafasi ya kurekebisha eneo hili. Kwa sababu jambo ambalo lipo wazi hawawezi kurekebisha wakati bado wanaendelea kuchukua bidhaa ya kifusi katika maeneo yale. Hivyo *yumkin* wamalize barabara ikamalike halafu waweze kwenda kufanya marekebisho katika eneo hilo ambalo tumelitaja la Mto-Mkuu.

Niombe tu Mhe. Mwakilishi aendelea kuwa na imani na sisi tuendelee kufanya mawasiliano tuhimizane na tukumbushane ili na sisi tuweze kumkumbusha mkandarasi kutimiza ahadi kama ambavyo tumezungumza.

Na. 62

Umakini katika Kufanya Tathmini ya Malipo ya Fidia

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba. Kwa kuwa serikali tangu zamani na hadi sasa pengine na hapo baadae ililipa/imelipa na huenda ikaendela kulipa fidia pale ambapo mali za wananchi zimeharibiwa katika kupitisha ujenzi wa barabara hizo.

a) Ni kwa kiasi gani serikali imekosa umakini katika kufanya tathmini ya gharama mbali mbali za mali za wananchi kwa kuwalipa malipo ya chini kiasi cha kushindwa hata kupata gharama za kununua viwanja mara tu baada ya kuvunjwa nyumba zao hizo.

b) Jee, hivyo inavyofanya serikali sio dhulma ya wazi wazi kama ilivyotokea katika ujenzi wa barabara ya Mwera Pongwe na hata hii ya Mtoni – Amani?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 62 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

a) Mhe.Spika, naomba kumjuulisha Mhe. Mjumbe kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijakosa umakini katika suala zima la tathmini. Aidha naomba ieleweke kwamba kuna fidia za namna mbili ambazo hufanywa wakati wa matayarisho ya ujenzi wa barabara. Fidia ya kwanza ni fidia ya nyumba na fidia ya pili ni ya mazao na vipando. Tathmini ya fidia hizo hufanywa na taasisi maalumu zilizowekwa na serikali kufanya kazi hiyo, ambapo tathmini ya nyumba hufanywa na maafisa wanaotoka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na tathmini ya mazao na vipando hufanywa maafisa wanaotoka Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Aidha taasisi zote hizo zipo kisheria na hufanya tathmini kulingana na utaratibu uliowekwa kisheria. Mhe. Spika, wizara yangu hufanya malipo kulingana na tathmini zilizofanywa na taasisi nilizozitaja hapo awali.Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haifanyi dhulma yoyote katika zoezi hilo la fidia. Hadi muda huu jumla ya wananchi 49 wamelipwa fidia kwa ajili ya barabara ya Amani-Mtoni ambapo jumla ya shilingi milioni mia tano, tisini na nne laki sita na arobaini na sita elfu (598,646,000/=) zimelipwa na bado kuna wananchi 34 hawajalipwa ambao wanadai jumla ya shilingi milioni mia sita na kumi (610,000,000/=).

Lakini pia kwa barabara ya Unguja Ukuu, Jendele, Jumbi hadi Koani, jumla ya wananchi 21 wamelipwa ambapo kiasi cha shilingi milioni mia moja na thalathini na tisa (139,000,000/=) zimeshalipwa kwa barabara ya Koani/Jumbi.

Aidha maelekezo ya SMZ yapo wazi kwamba hakuna nyumba ya mwananchi yeyote Zanzibar itakayovunjwa kabla ya kulipwa fidia husika. Hivyo ninamthibitishia Mhe. Mwakilishi na Baraza lako kwamba hakuna mwananchi aliyedhulumiwa kwa msingi wa kuvunjiwa nyumba yake bila ya kulipwa fidia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri ametaja kwamba kuna taasisi zinafanya tathmini kwa upande wa mazao ni kilimo na upande wa nyumba upande ni Wizara ya Ardhi.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba wizara yako inaziamini taasisi mbili hizi. Jee, isingekuwa vyema kabla ya kufanya malipo ikaona hasa athari wanazozipata wananchi hao kwani hivi ninavyokueleza barabara ya Pongwe Mwera kuna watu wamevunjiwa nyumba za tofali lakini wamelipwa shilingi milioni moja wengine milioni mbili hata kiwanja hawapati? *Tha's (a).*

(c) Kuendelea kwenda kuwalipa watu hao bila ya kuhakikisha wameathirika kiasi gani si kuwafanyia dhulma wananchi hao wa maeneo hayo?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika majibu mama kwamba utaratibu wa kulipa fidia wizangu yangu inapokea taarifa za tathmini ambazo zimefanywa na taasisi husika. Lakini kabla ya kulipa kwetu naomba kukuthibitishia Mhe. Mjumbe na Baraza lako tukufu kwamba wizara huwa tunakwenda kuyaona maeneo yenyewe, tunazungumza na wenyewe, tunawakabidhi stakabadhi, tunawapiga picha.

Kwa hivyo, tunakijua kinachofanyika nini, hakuna mtu ambaye analipwa fidia ikawa kwamba wizara yetu haina taarifa za kutosha kuhusiana na fidia hizo. Hivyo kama kuna mtu ana malalamiko yake kuhusiana na suala la fidia utaratibu upo wazi, anatakiwa kumuandikia Katibu Mkuu wetu tutakwenda kuangalia kama ipo haja ya kufanya malipo ya ziada huwa tunafanya hivyo, kama hakuna haja tunaendelea kumuelewesha mtu huyo ili aelewe msingi na utaratibu wa ulipaji wa fidia.

Lakini hakuna mtu ambaye analipwa fidia bila ya wizara yetu kwenda kujiridhisha kwa kiasi gani huyo mtu amelipwa kwa mujibu wa taratibu husika.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi ningependa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa katika ujenzi wa barabara serikali inakata miti ya kudumu na mazao ya wananchi katika maeneo ambayo wanatarajia kujenga. Lakini ulipaji wake wa fidia huwa unasuasua mno.

Mhe. Spika, barabara za Mkoa wa Kusini Pemba sita zile zilizojengwa toka serikali iliyopita hadi leo, mazao ya wananchi hawajalipwa. Je, ni lini hasa serikali italipa fidia mazao yale, licha ya kuwa serikali ipo mbioni ni lini watu wale watalipwa?

Swali la pili, ni kuwa tathmini inayofanywa na Wizara ya Kilimo juu ya mazao ni ndogo mno; yaani ni ya zamani sana. Je, wizara hii ina mpango gani wa kufanya tathmini upya wa mazao ya wananchi ili wapate fidia inayoridhisha kidogo?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika ujenzi wa barabara kuna tathmini aina mbili kwa tatu. Kuna tathmini ya miti pamoja na vipando, kuna tathmini ya nyumba na kuna tathmini ambayo hufanyika kabla ya ujenzi wa barabara, halafu kuna tathmini ambayo inafanyika baada ya ujenzi wa barabara.

Malengo yetu kwamba tathmini kabla ya ujenzi wa barabara hatutovunja nyumba yeyote kabla ya kumlipa fidia. Wakati ujenzi unaendelea inawezekana wakati wa harakati uhamishaji wa vifaa na vitu vyengine nyumba zikaathirika, nyumba hizo tunachelewa kuzilipa. Lakini pia miti na vipando tuna desturi ya kuchelewa kulipa kwa kuona tu kwamba kipaumbele chetu tuanze kuwalipa watu ambao tumewavunjia nyumba zao au tuna dhamira ya kuwavunjia nyumba zao.

Kwa hivyo, kama kuna mtu ambaye hajalipwa fidia kwa suala la miti, ni kweli tunakiri hivvyo na tuna maeneo mengi ambayo ambayo tunadaiwa fidia kwa sababu ya miti na vipando. Madhumuni yetu ni kulipa lakini tatizo letu ni pale pale ni ukosefu wa fedha, miradi yetu ni mingi na mikubwa ambayo gharama zake ni kubwa. Na tukaona jambo la msingi tuelekeze tusiwasumbue watu katika makaazi yao lazima tuwalipe fidia kabla ya kuvunja nyumba zao.

Nam. 20

Nguvu Kazi ya Vijana Kutotumika kwa Kilimo Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub)- Alijibu:-

Mazao ya kilimo yamekuwa na soko la uhakika kutokana na kuimarika kwa sekta ya utalii, lakini vijana wengi wanakwepa kushiriki kazi za kilimo na kuachia wazee Zanzibar.

a) Je, serikali imechukua hatua gani kuondoa tatizo hilo?

b) Kwa nini serikali inaachia vijana waendelee kukaa katika vijiwe badala ya kuwapa elimu ya kujiajiri kupitia sekta ya kilimo Zanzibar?

c) Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vijana pembejeo za kilimo na zana za kisasa ili kuwavutia kupenda kazi za kilimo katika kupambana na tatizo la ukosefu wa ajira?

Mhe. Spika: Naona huyu ameshakuwa Kaimu wa Jimbo la Muyuni sasa (*Kicheko*).

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 20 kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ninakubali kuwa mazao ya kilimo yana uhakika, la uhakika katika sekta ya utalii na wakulima wa Zanzibar wangepaswa kuitumia fursa hiyo kwa kuzalisha mazao yenye ubora ili yakubalike katika masoko hayo. Ni kweli kuwa vijana wengi wanakwepa kazi ya kilimo na kukimbilia mjini ili wapate mipango ya kuwapatia fedha za haraka bila ya taabu.

Hata hivyo, suala la kilimo ni la hiyari, serikali haiwezi kuwalazimisha watu kulima lakini wakati huo huo serikali ina wajibu kuona kuwa vijana wanafanya kazi zenye kuwapatia riski za halali. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika zinandaa miradi ya pamoja na mazingira mazuri ya kuwawezesha vijana kujiajiri wenyewe katika sekta ya kilimo. Wataalamu wa kilimo wanafanya kazi ya kutoa mafunzo kwa vijana katika vikundi vya ukulima. Kwa mfano kilimo cha *rosela* na mboga mboga huko Tunguu na vile vile usarifu wa mazao. Miradi kama hii inatarajiwa kuanzishwa sehemu mbali mbali Unguja na Pemba. Bila shaka kuna changamoto kati ya suala hili hasa kupata maeneo yenye ardhi ya kilimo na mitaji ya uwekezaji katika kilimo.

Mhe. Spika, Wizara yangu inapenda kuona vijana wamehamasika na wanapatiwa taaluma ya uzalishaji lakini suala hili la kuhamasisha vijana linahitaji mashirikiano na viongozi mbali mbali wa mkoa, wilaya, Shehia na pia Wajumbe wa Baraza hili ambao ndio viongozi wa majimbo.

Kwa hivyo naomba Wajumbe wa Baraza hili tushirikiane katika kuhamasisha na pia inapowezekana kuwawezesha kwa nyenzo za kuanzia kazi za kilimo. Vijana ni raslimali ya taifa, kwa hivyo tuwasaidie kwa pamoja ili wajiajiri wenyewe badala ya kubaki vijiweni.

b) Mhe. Spika, serikali katika kutoa misaada haichagui kama inavyowapatia pembejeo wakulima kwa njia ya ruzuku, kwa hivyo na vijana pia wakijiajiri katika kilimo nao watakuwa ni wadau wa kupata misaada yoyote ya kilimo inayopatikana, mradi tu waitumie vizuri kama ilivyokusudiwa. Penye nia ipo njia.

Kama vijana watakubali kuhamasika katika kilimo kwa dhati basi bila shaka misaada ya kuwasukuma katika kazi hiyo wataipata ikiwemo taaluma.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa sababu vijana wa Muyuni wamejitokeza sana katika masuala ya kilimo cha mboga mboga na kwa sababu mvua ni tatizo kipindi hiki kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na kwa sababu Mhe. Mwakilishi amejitahidi kupeleka maji pale lakini hata hivyo hayajawa ya kutosha kwaa kutumia pamoja na kumwagilia.

(a) Je, ni lini wizara yako itawasaidia vijana wangu wa Muyuni pale ili waweze kutumia hayo maji kidogo kwa kutumia *drop irrigation* kwa sababu haitumii maji mengi. Ni lini utawasaidia vijana wa Muyuni hii *drop irrigation* ili waweze kuendeleza kilimo chao cha mboga mboga?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, ahsante sana ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, suala la kusaidia vijana kwa *drop irrigation* ni suala ambalo niseme ukweli ni suala ambalo mradi wake ni ghali sana. Lakini kikubwa kinachotoka kwenye wizara yetu ni taaluma ili kuwasaidia vijana kupata taaluma. Kama nilivyosema kwamba wizara yangu inatoa sana taaluma. Kwa hivyo, kuna mambo ambayo kama *drop irrigation* ni mambo ya kujipanga hasa sisi wawakilishi wa majimbo, tukae tuwasaidie vijana wetu mambo kama haya.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa vijana wangu wa Jimbo la Chonga wamehamasika sana hasa katika maeneo ya Pujini kule katika kilimo cha mboga mboga. Lakini kutokana na uchache wao wa taaluma ya kilimo hiki wanasumbuliwa sana na wadudu waharibifu.

(a) Je, ni lini Mhe. Naibu Waziri atawatembelea vijana hawa pamoja na kuwapatia wataalamu watakaowasaidia katika kuimarisha kilimo chao?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe anajua kwamba mimi ni mkarimu sana wa kutembea na ninapotembea mara nyingi huwapigia simu wawakilishi ili tuwe pamoja. Kwa hivyo, ninamuomba nitakapoanza ziara yangu tu safari hii basi nitatembelea katika hiyo sehemu na kuwapatia wataalamu watu wake hao.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ikiwa vijana hawa watajikusanya kwa kutaka kuimarisha kilimo. Je, wizara yako ina programu yoyote ya kuwasaidia vijana hawa na kama ipo utawasaidia nini?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, wizara yangu inayo programu ya kuimarisha huduma za kilimo. Kwa hivyo, mara nyingi programu hii huwasaidia wakulima kuwapa taaluma. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 51

Kuitangaza Zanzibar Kupitia Vyombo Vya Nje

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa sehemu za makumbusho ya mambo ya kale huwa ni moja wapo ya kivutio cha watalii na nchi nyingi zimekuwa zikitangaza sehemu za makumbusho ya mambo ya kale na vivutio vyengine ili watalii wavutiwe kutembelea nchi hizo.

(a) Je, Wizara inafanya matangazo hayo ya makumbusho ya mambo ya kale kupitia vituo gani vya TV ndani na nje ya nchi hususan TV za Kimataifa kama *CNN, BBC?*

(b) Kama bado Wizara ina mpango na mikakati gani ya kuitangaza Zanzibar kwa watalii kupitia makumbusho ya mambo ya kale kwa TV za ndani na TV za nchi za nje?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye kifungu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mhe. Spika, Idara kwa kushirikiana na *ZBC TV* huwa inarusha vipindi ambavyo huyatangaza maeneo ya kihistoria katika programu ya Utalii kwa wote, Pia Idara ina mpango wa kurusha vipindi vyake vya kuyatangaza maeneo ya kihistoria kupitia Star TV na Oman TV, imetengeneza programu iliyorushwa mara kwa mara vipindi ambavyo vinatokana na historia ya Zanzibar na utalii katika msimu wa Januari, Juni hadi Julai mwaka huu tukipokea vipindi mbali mbali ambavyo vinatoka Oman.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Lakini kabla sijauliza swali Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alinitaja kwa kusema kwamba mwakilishi Saleh wa Jimbo la Wawi. Mimi nataka kumbainishia

kwamba mimi naitwa Nassor Salim Ali Mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo sio Jimbo la Wawi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba wanatangaza masuala haya ya makumbusho kwa kupitia kama vile *Star TV* na *Oman TV*. Kwa kuwa suala hili la makumbusho huwa linatangaza sana masuala ya utalii, hususan katika nchi za ulaya kama vile Marekani, Uingereza, Ujerumani, China.

(a) Je, serikali kwa kupitia Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ina mpango gani wa kutangaza matangazo haya kwa kupitia televisheni kama vile *BBC, CNN* na *CCTV* ili watalii waweze kuitambua na kuifahamu Zanzibar kwa kupitia makumbusho?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, masuala yanayohusiana na *promotion* ya shughuli za utalii ni pana sana na wizara yangu kwa kupitia Kamisheni ya Utalii tunaziendeleza kwa awamu. Tunachofanya hivi sasa ni kukaribisha mashirika mbali mbali ya habari ambayo pamoja na wizara na Kamisheni ya Utalii, huwa tunawakaribisha na tunashirikiana nao kwa kutengeneza *documentary* maalumu kwa vivutio vya utalii vya Zanzibar, na kwa kweli zimesaidia sana kuitangaza nchi yetu.

Mashirika ya habari ya Ufaransa, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri Oman, Misri na China kwa mwaka huu yamekuja na tumefanya kazi hii. Hivi sasa bado hatujakuwa na uwezo wa kuweza kutangaza katika mashirika ya *CNN* na *BBC*, kwa sababu gharama zao za kutangaza ni kubwa sana. Kwa hivyo, hivi sasa bado tunashughulika na matangazo ya nchi nyengine. Kwa hivyo, wenzetu wa Ulaya kwa kupitia televisheni za Ufaransa wanaweza kuviona vivutio vya utalii vya Zanzibar.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kama swali mama lilivyoeleza kuwa haya magofu yanaingiza sana fedha katika serikali yetu kwa kutumia watalii wanaokuja

Nimezinduliwa Mhe. Spika.

Nam. 54

Hifadhi za Maeneo ya Kihistoria Vitongoji

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu, naomba Hansard iweke sawa vile vile kwamba mimi Maalim Saleh Nassor Juma ndio Mwakilishi wa Jimbo lile la Wawi, ambalo ndio jimbo lile alilotoka Mhe. Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambaye ni mpiga kura wangu. Mimi ndiye mwakilishi wa jimbo lile na sio Mhe. Nassor Salim Ali.

Baada ya maelezo hayo, naomba swali langu nambari 54 lipate majibu hivi sasa.

Kimsingi kijiji cha Vitongoji katika Wilaya ya Chake Chake Pemba inaonesha kwamba kinahistoria kubwa kwa ajili ya kupokea wageni mbali mbali karne za nyuma hususan kutoka Bara – Arab, India na hata katika visiwa vya Ngazija. Aidha, Historia inayoonesha kuwa Field Mashall – John Okelo alifikia Vitongoji na kuishi kwa miaka mingi na hatimae kuondoka siku chache kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa kuwa maeneo waliofikia wageni hao hususan Waraabu wa Kioman, Wangazija na hata eneo alilokua akiishi Field Mashall Okelo bado lipo.

Ni lini Serikali itafanya utafiti wa kina katika kijiji hicho na hatimae kukifanya kuwa ni sehemu ya makumbusho ya kihistoria?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika makadirio ya mwaka zimetengwa pesa kwa ajili ya kufanyiwa utafiti maeneo mengi ya kihistoria ikiwemo Vitongoji. Idara ina mpango wa kutengeneza makumbusho ya eneo la Vitongoji Ngezi na Kijumbani ili kuweka taarifa za kihistoria za eneo hilo. Mradi huo utakamilika baada ya kupatiwa fedha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kuna mambo yanahitaji tafiti na yale ambayo tafiti zake zimeshakamilika zamani. Kwa kuwa Vitongoji ni sehemu ya kihistoria sana kwamba Waarabu wa Kioman walifika pale Umangani, Wangazija walifika pale. Sio kwamba walifika tu na kuzaa, Marshal John Okelo alikaa pale na aliondoka siku chache tu kabla ya Mapinduzi, hapo hapahitaji tena tafiti.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mkamandume alikaa Pujini miaka mingi sana na hamjaendeleza.

a) Je, kuendelea kufanya tafiti tu bila ya kuchukua hatua si kuzidharau sehemu muhimu kama hizi na kufanya historia yake ipotee?

b) Kwa kuwa wenzetu wamehifadhi sehemu zao za kihistori, kwa mfano Wahindi pale Tajmahal wamepaweka vizuri sana. Leo kuendelea kudharau sehemu kama Mkamandume Pujini si ni kuidharau hata ile Pemba? Ahsante sana Mhe. Spika?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwakilishi nataka nikuambie wizara yangu kwa kushirikiana na watu wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, kama ulivyouliza swali lako kuhusu utafiti.

a) Nataka nikuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba utafiti umefanyika na maeneo mengine ya kihistoria ya Pemba nzima tunajipanga kwenye wizara yetu ili kufanya utafiti zaidi, kwa sababu wataalamu wa utafiti tunao na tumewasomesha wenyewe kwenye wizara yetu.

Kwa hivyo, kwa kushirikiana na wewe Mhe. Mwakilishi nakuomba sana tutembelee maeneo yote tuliofanya utafiti na tukagundue vitu ambavyo ni vya zamani sana, mifupa ya binadamu na vitu vyengine ambavyo tumevifanyia utafiti kwenye wizara yetu. Mhe. Mjumbe tunaweza kukuonesha na ukajua kwamba wizara yangu imefanya utafiti wa kutosha.

b) Mhe. Mwakilishi swali lako la pili umezungumzia kuhusu Mkamandume. Mhe. Spika,sisi wenyewe wizara kila mwaka tunafanya ziara ya kutembelea maeneo ya Makumbusho na Mambo ya Kale Pemba na maeneo mengine ya Unguja ili kuweka vigezo muhimu vya kihistoria ili wananchi wetu wajuwe kwamba hii ni historia yao ya Zanzibar, kuna makumbusho ambayo yanahifadhiwa na kufanyiwa utafiti.Mhe. Mwakilishi nakuomba sana tushirikiane pamoja, tunapokuja Pemba kufanya ziara basi ujuwe kwamba wizara inafanya utafiti na inatembelea maeneo yake yote ya kihistoria.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kisiwa cha Pemba kina maeneo mengi ya kihistoria kama vile Mkumbuu, Pujini na Msikiti Chooko.

(a) Je, kwa nini maeneo hayo hayaendelezwi na nini hasa kipaumbele cha wizara kwa Pemba kwa maeneo ya kihistoria?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba visiwa vya Unguja na Pemba sio Pemba peke yake vina maeneo mengi sana ya kihistoria, ni utajiri ambao tumeurithi, una hadhi kubwa na una heshima kubwa kwa nchi yetu na serikali inajitahidi muda wote kuyaendeleza.

Kwa hivyo, maeneo ya Pujini na hasa kama alivyosema Mhe. Saleh eneo la Mkamandume lina historia kubwa, wizara na serikali kwa jumla inalielewa hilo. Eneo la Mkumbuu nalo lina historia kubwa na Msikiti Chooko pia. Kwa hivyo tunayaendeleza na ili kuyaendeleza ni lazima yafanyiwe *study* kubwa, pana historia kubwa ambayo wengine wanaipotosha, wengine wanaizungumza sivyo, wengine wanalizungumza suala la Mkamandume Pujini kwa lugha tofauti. Ukimkuta mtu leo atakuambia Mkamandume maana yake nini. Kwa hivyo, huwezi ukachukua maneno ya mtu mmoja ukayakubali, ni

lazima pafanyiwe utafiti wa kina, waende pale wachunguzi wachimbe udogo waangalie historia ya miaka mingi. Mambo hayo tumeyaanza kwa kushirikiana na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na wenzetu wa nje.

Mhe. Spika, kwa hayo maeneo matatu ambayo Mhe. Salma Mohamed ameyauliza ndio hasa ambayo tumeyalenga kama Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kwamba ni maeneo ambayo yana historia pana sana. Ukenda pale Mkumbuu utaambiwa palikuwa na Msikiti uko chini ya bahari. Kwa hivyo haya ni mambo ambayo yanataka kufanyiwa utafiti mkubwa.

Kwa hivyo, kipaumbele cha wizara kwa maeneo ya Pemba ni kuhakikisha kwamba historia hii ambayo imeachwa kwa muda mrefu tunairudisha, tunaitafiti na kuna mambo ambayo tutayajenga upya ili ile historia ibaki kama ilivyokuwa zamani. Eneo la Msikiti Chooko lina historia kubwa ambapo kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri tumekwenda na watu wetu wanafanyakazi kubwa ya kuhakikisha kwamba tunairudisha hali halisi ilivyokuwa na kazi hiyo imeanza. Kwa hivyo, kwa Pemba kipaumbele chetu kikubwa ni maeneo hayo matatu. Msikiti Chooko ambapo pana Mazrui *Fort* imeanguka haipo kabisa na eneo hili la Mkamandume ambapo kulikuwa kuna *Fort* ya zamani kabisa nayo imeanguka kabisa ni kifusi na huku Mkumbuu nako kuna Msikiti ambao umezama uko chini ya bahari.

Kwa hivyo, ni maeneo ambayo serikali kwa kupitia wizara yangu na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, tumechukua jitihada kubwa ya kuona kwa Pemba hayo maeneo matatu ndio ambayo tutatia nguvu zetu za kutosha kuona kwamba historia yetu inarudi kama ilivyokuwa zamani.

Nam. 80

Wizara Kuwajengea Wananchi Sehemu ya Kusubiri Kuwaona Wagojwa Wao

Mhe. Saleh Nassor Juma: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Hivi karibuni Wizara ya Afya imeweka utaratibu wa kupunguza msong'amano wa watu kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hatua hii inafaa kupongezwa kwa vile inapunguza zogo na vurugu kutokana na wingi wa watu wanaoingia na kutoka bila ya utaratibu. Hata hivyo, kumekuwa na usumbufu kwa baadhi ya watu ambao wanakuwa na shida na dharura ya kweli ya kuingia wakati wowote kufukuzwa na walinzi bila kujali dharura na shida zao kwa wakati huo.

(a) Wizara haioni haja ya kujenga eneo maalumu kwenye sehemu ya Bustani ya Hospitali ya Mnazimmoja ambayo watu wataweza kukaa na kusubiri kuwaona wagojwa wao?

(b) Kwanini Wizara isiweke pasi maalumu za kuingia, kwa wale wananchi ambao wana dharura ya kushughulika na wagonjwa wao kwa mfano wagonjwa wa Operesheni, katika muda ambao siyo wa kutizama wagonjwa?

(c) Kwanini walinzi waliowekwa kudhibiti uingiaji wa watu hawatumii lugha nzuri kwa wananchi wanaotaka kupita mlangoni wakiwa na shida na matatizo mbali mbali yao wao au watu wao, na badala yake hufanywa kama vile wamekuja hapo bila shughuli maalumu inayowahusu?

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifutavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara iliona haja ya kujenga eneo maalumu "*waiting bay*" kwenye sehemu ya bustani iliyo mbele ya Hospitali ya Mnazi mmoja, ambayo watu wangeweza kukaa na kusubiri kuwaona wagonjwa wao. Baada ya kuona tatizo la msongamano ndani ya hospital, uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kupitia Wizara ya Afya iliandaa michoro na ilitenga bajeti kwa ajili ya ujenzi huo. Baada ya jitihada hizo ikabidi Wizara ipate kibali cha kujenga kutoka Mji Mkongwe, kwani ndio wenye eneo hilo. Kwa bahati nzuri Mji Mkongwe wa Zanzíbar ni

sehemu ya miji ya urithi wa dunia na haikubaliki kubadilishwa uhalisia wake isipokuwa kwa ruhusa maalumu. Kwa mantiki hiyo ruhusa kwa wakati huo haikutolewa ya kujenga mahala hapo kutokana na unyeti wa jambo lenyewe.

Hata hivyo, Mhe. Spika, ruhusa tumeshapata ya kulitumia eneo hilo kujenga *waiting bay* na maandalizi ya ramani yanaendelea na hatua za utekelezaji ziko njiani.

(b) Ilipoamulika kuweka ulinzi milangoni na njia za kwendea wodini, pasi maalumu kwa shuhguli tofauti ziliandaliwa kuweka taratibu za kuingia hospitalini. Pasi za magari, pasi za wanaokwenda kuonana na uongozi wa hospitali na utawala, pasi za kutizamia wagonjwa na pasi za wenye haja maalumu kama hizo za wenye dharura. Lakini si tunajuwa watu wa zama zetu ni wakati wa uwajibishwaji kutii sheria bila shuruti kidogo imekuwa ni matatizo. Wakipewa pasi hawarudishi au mtu anabaki ndani anamtuma mtu mwengine kumpa pasi mtu wa nje huku wakiwasiliana kwa simu na wengine wanaondoka nazo watumie kwa siku nyengine. Mwishowe ikawa vurungu na askari ndo askari, kuvurugikiwa na utaratibu hawapendi. Mhe. Spika, nawaombeni Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wananchi na Wajumbe wa Baraza hili kwa ujumla wetu tafadhalini tushirikiane na askari, kwa sababu nia njema ni kujitahidi kufuata utaratibu.

(c) Mwanzoni walipoanza ni kweli ilikuwa ni mchaka mchaka ule wa polisi, lakini na wananchi nao walikuwa hawataki kukubali kwamba sasa kuna haja ya mabadiliko ya utaratibu wa hospitali, tunaelekea kwenye hospitali na sio bustani ya forodhani. Kwa hivyo, yakawapata walokuwemo na wasiokuwemo. Lakini baada ya malalamiko ya watu, uongozi wa hospitali ulikaa na ukawafahamisha askari hao, kuwa wapole na hospitali wanaokuja wanashida na hawana budi kuwasikiliza mradi tu wakubali kufuata utaratibu. Lakini pia kwa upande wa wananchi sasa nao wameshafahamu, kwa hivyo malalamiko yamepungua sana.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa ulinzi ni jambo zuri na kwa kuwa walinzi wale waliopo pale mara nyingi ukimaliza muda wa kutizama wagonjwa huwa wanaingia ndani na wakawatoa wale watu wanaowatizama wagonjwa, lakini huwa wanaingia na virungu. Je, Mhe. Waziri haoni utaratibu huu unaweza ukasababisha athari zaidi hasa kwa wale wagonjwa ambao wana maradhi ya moyo?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kushika virungu ni sehemu ya ulinzi, wala hakuna nia ya kuwa atapigwa mtu kirungu, isipokuwa ni sehemu ya kazi yao. Pia, hakuna nia kwamba askari wale waingie ndani ya wodi na kuwatoa wananchi, isipokuwa kwa kawaida hupigwa kengele kwanza kwamba muda umekwisha. Sasa inapokuwa muda umekwisha na wananchi bado wamebaki kwenye wodi, ndio inaonekana sasa kunahitaji amri. Kwa hivyo, amri ya kiaskari bila shaka huwa inahitaji ulinzi, lakini hakuna nia mbaya ya kumpiga mtu wala tangu hapo hatujawahi kumpiga mtu, ni kujilinda tu.

Nam. 82

Kukosekana Umeme Katika Eneo la Kuchomea Taka

Mhe. Saleh Nassor Juma: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Kumekuwa na ukosefu wa umeme katika eneo la kuchomea taka katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, hali ambayo inaweza kupelekea maambukizi kuongezeka. Hii imetokana na shughuli za ujenzi zinazoendelea hapo na waya kukatika kwenye eneo la kitengo cha maradhi ya uti wa mgongo.

(a) Lini umeme utarejeshwa katika eneo hilo?

(b) Kwanini maeneo kama hayo zinapotokea hitilafu hayafanyiwi matengenezo haraka?

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 lenye kifungu (a) na (b) kwa ufupi kama ifuatavyo:-

(a) Umeme tayari upo katika eneo hilo alililiuliza.

(b) Inategemea na Kiongozi Dhamana wa sehemu linapotokea tatizo, na yeye anachangamka kiasi gani kuripoti kwa Katibu wa Hospitali au moja kwa moja katika sehemu ambayo inahusika na kurekebisha tatizo lililotokea. Kwa hili la umeme Kitengo cha Ufundi cha Mnazi Mmoja Hospitali kiko kama hatua 20 tu na hapo *Incenerator* ilipo. Kwa hiyo, ni mtu tu kutotaka kutimiza wajibu wake kama kiongozi wa sehemu, na huo ni uzembe tu wala haikuwa sababu kubwa.

Mhe. Spika, kwa taarifa ya wajumbe wako na wananchi ni kwamba saa 24 mafundi wetu wa umeme pale hospitali wanakuwepo kwa vitu vya dharura namna hii. Suala la kuzimika kwa umeme au kukatika umeme katika huduma kama zile ni la kawaida. Kwa hilo lililotokea tunaomba radhi, lakini matengenezo yameshafanyika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwanza nishukuru serikali inasema kwamba umeme umeshapatikana katika sehemu ya kuchomea taka. Mhe. Spika, pamoja na hayo, kuna siku nilitembelea katika ufukwe uliopo pembezoni mwa hospitali yetu na kuona kwamba kuna taka za hospitali ambazo zimo katika fukwe zinachukuliwa na maji.

(a) Je, hali ile ilitokea kwa bahati mbaya tu au ndio kwa sababu umeme ulikuwa haupo siku hiyo. Kama sio kwa bahati mbaya Mhe. Waziri huoni kwamba takataka za hospitali ni sumu, huoni kwamba ni uharibifu wa mazingira ya bahari jambo ambalo zitatuathiri hata sisi pale tutakapotumia samaki?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, hata sisi wizara tunasikitika sana na hali iliyokuwepo pale kwenye *incenerator* na ni kweli ni suala ambalo linaharibu mazingira na vile vile mabaki ya hospitali sio mazuri kutupwa ovyo. Suala hili sasa ni la muda mrefu na wizara inalishughulikia. Hivi ninavyoeleza tulishatoa *tender* kununua *incenerator* mpya kwa ajili hiyo. Lakini kwa kulifahamu hilo pia tuna *incenerator* nyengine zitakazojengwa pale mradi wa ORIO utakapokuja, suala hili linatuumiza sote na tunaendelea kulifuatilia na karibuni tutakapopata hiyo *incenerator* mpya suala hili litaondoka. Sote halitufurahisi na kwa kwali ni suala baya sana, tunasikitika kwa hilo, lakini ndio hali halisi lilivyo kwa muda.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nataka kuuliza swali dogo tu kwa Mhe. Waziri pamoja na majibu mazuri aliyoyaeleza hapa kwamba serikali inafanya jitihada ya kutafuta hizo zana za kuchomea taka. Labda angetueleza, kwa sababu na mimi kamati yangu imeshatembelea na hiyo hali imeshaiona, angetueleza Mhe. Waziri wakati wanasubiri hizo zana za kuchomea taka:

(a) Je, wana njia gani mbadala ya kutokutupa taka katika hilo eneo kwa sababu maji yanapojaa hayo mabaki yanakuwa yanatembea baharini sehemu nyingi?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, jitihada tunazofanya ni kuzichoma katika ile hali tuliyonayo. Hapo ilipotokea umeme ukazimika nadhani moja ilikuwa tatizo ni hilo, lakini hatufurahii hata kidogo kuzitupa taka zile baharini. Narudia kusema Mhe. Spika, pale

wameshakwenda kamati, ameshakwenda mpaka Makamu wa Kwanza wa Rais na imeshaundwa kamati ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa sababu anahusika na mambo ya mazingira, tungelishughulikia kwa pamoja na tukafikiria njia mbadala, tukakuta njia zote tunazotaka kuzitumia ni mbaya zaidi kuliko kulifanyia haraka tukapata ile *incenerator* mpya.

Maana njia mbadala uchukuwe taka ukazichome mwituni huko, lakini huo mwitu ni wa hali gani, ukifika huko na wananchi huko watakuambia hapana usituletee balaa huku. Kwa hivyo, tumeona twende nalo katika hiyo hali ya shida na huku tuhimize suala hili na limeshatolewa *tender* na tunategemea suala hili likamilike pale tutakapopata *incenerator* mpya. Kwa sasa tunazichoma kwa juhudi tunazoweza kuzichoma, halinifurahishi hata mimi, ni suala ambalo ni la kusikitisha.

TAARIFA YA SERIKALI

Taarifa ya Serikali juu ya Hoja zilizotolewa katika Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na majadiliano kuna taarifa moja fupi kama kuna mtu ambaye amepoteza simu humu ndani basi anaweza kwenda kwa makatibu hapa na akaweza kutoa utambulisho wake na kuweza kukabidhiwa simu yake hiyo na simu ipo hapa hapa nitamkabidhi mmoja wa makatibu wetu.

Waheshimiwa Wajumbe, nimearifiwa kwamba taarifa ya hoja hii iliyowasilishwa jana na michango haikuanza kutolewa sasa kama aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Manispaa yupo na anayo maneno, basi tunamkaribisha na kama hakuna basi twenda kwenye mchangiaji wa kawaida, inaonekana hakuna. Kwa hivyo, naomba nimkaribishe sasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadaye Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhanahu Wataalla* kwa kutujaalia kuwa hai na wazima wa afya na siku ya leo tukaweza kuendelea na shughuli zetu katika Baraza hili.

Mhe. Spika, pia naomba nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Hoja hii ya Taarifa ya Serikali juu ya Hoja zilizotolewa katika Ripoti

ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyochunguza Baraza la Manispaa la Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kabla ya kuzungumzia hoja hii nizungumze neno moja dogo sana ambalo kwa bahati mbaya ikiwa sikulisema hapa leo na kwa sababu leo ni siku yetu ya mwisho ya kikao hiki pengine inaweza ikainyima fursa nzuri serikali kulifuatilia.

Mhe. Spika, karibuni nchi yetu kidogo wananchi walipata mkanganyiko mkubwa kuhusiana na hoja ya kwamba katika kuandaa mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba uliwashirikisha Wazanzibari ama laa. Tunashukuru hatua hiyo hatimaye imejaribu kutafutiwa ufumbuzi kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete aliwaita Viongozi wa Vyama vya Siasa na wamezungumza na tulitolewa taarifa kwamba suala hilo litamalizwa vyema kwa njia ya majadiliano na tunategemea kwamba katika kikao kinachoanza mwisho wa mwezi huu cha Bunge, basi suala hilo *inshaallah* litapatiwa ufumbuzi.

Lakini Mhe. Spika, hapa katikati palitolewa taarifa kwamba kuna miswada mingine ambayo inakwenda katika Bunge na mmoja unahusu Sheria ya Kura ya Maoni kuhusiana na Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano na pili Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali ambazo tunapewa taarifa kwamba pia zinahusu mambo kadhaa ya Muungano.

Sasa Mhe. Spika, ilikuwa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ije Zanzibar, ili kuja kukwepa kutokezea matatizo kama yale ambayo yalitokezea awali. Lakini nimepata taarifa kwamba pamoja na taarifa ambayo ilikuwa imetolewa awali sasa kamati ile imezuiwa kuja Zanzibar kwa ajili ya kuja kuchukua maoni.

Kwa hivyo, najua hapa Mhe. Spika chombo hiki hakina mamlaka juu ya taratibu za Bunge, lakini nimeona niliseme ili serikali na hasa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo inaratibu masuala ya Muungano ilifuatilie, ili tusijetukaingia tena katika mzozano kama ule uliohusu mswada wa mwanzo.

Nadhani Wazanzibari ni wabia sana katika muungano huu na tuna haki sawa sawa na Watanganyika katika kusikilizwa juu ya yale mambo yanayohusu mchakato wa kuipata Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano. Mhe. Spika, niliona nilisema hilo na kama nilivyosema kama sikulisema hapa pengine lisipate nafasi ya kushughulikiwa ipasavyo.

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa naomba nirudi katika hoja ambayo iko mbele yetu. Mhe. Spika, kuhusiana na hoja hii kwanza naomba niipongeze serikali kwa sababu ripoti yake

ambayo imewasilishwa hapa ni ya kina na kwa kiasi kikubwa imejielekeza vilivyo katika yale mapendekezo ambayo yalitolewa na Kamati Teule. *(Makofi)*

Vile vile, nataka nimpongeze sana mtoa hoja au muwasilishaji wa taarifa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed na nilikuwa nikimwambia hapa ninamuonea huruma kwamba mizigo yote mizito huwa anatwishwa yeye ya kuja kulikabili Baraza hili, lakini kwa sababu ya umahiri na umakini wake wala hasiti Mhe. Spika na amekuwa akiifanya kazi hiyo kwa umakini na umahiri mkubwa. Hivyo, ninampongeza sana pamoja na kumpa pole kwa mara nyengine vigongo anavyovipata vya maneno, lakini mara zote mwili wake uko imara kuvipokea vigongo hivyo na bado akiwa na tabasamu kabisa wakati anajibu hoja zetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika mjadala wa taarifa kama hii kwa ile Ripoti iliyohusu Kuchunguza Shirika la Umeme (*ZECO*), kulijitokeza hisia na hata kwenye majibu ya serikali walilizungumza sana hili, kwamba isitafsirike katika kujadili masuala haya kuna kujigawa kikambi baina ya mawaziri au serikali kwa upande mmoja na wawakilishi ambao si mawaziri na tumezoea kuwaita *back benchers*.

Mhe. Spika, nataka nikubaliane na maelezo ambayo yametolewa na serikali na niwahakikishie kwamba kwa upande wetu hakuna dhamira yoyote mbaya katika kujadili masuala mbali mbali yanayoletwa na serikali, kuikosoa na kuielekeza kwa sababu hiyo ndio lengo la kuundwa chombo hichi na ndio dhamira ya kuwepo kwetu hapa.

Pia, nikubaliane na maelezo kwamba kuja hapa na misimamo haisaidii. Lakini naomba niseme kwamba ugomvi ni jambo moja na wala hakuna ugomvi baina yetu na serikali, lakini mivutano katika demokrasia ni jambo la kawaida na mivutano mara nyingi Mhe. Spika ndio inayojenga, kwa sababu inapelekea upinzani wa hoja ambao hatimaye hupelekea ukweli ujulikane na wananchi kupata taarifa sahihi ya kile ambacho kinatendeka katika nchi yao. Kwa hivyo, hilo nadhani lisikutishe, jambo la muhimu Mhe. Spika, kwamba sote kuwa wazalendo na kuongozwa na hoja ya maslahi ya taifa pamoja na watu wetu. *(Makofi*

Mhe. Spika, katika hili nadhani kama kuna jambo la kusisitiza hapa basi ni kuwaomba Waheshimiwa Mawaziri wawajibike au serikali iwajibike. Sasa ikiwa mawaziri au serikali itawajibika ipasavyo na wananchi wakaona na wakaridhika kwamba serikali yao pamoja na mawaziri wao wanawajibika ipasavyo, basi nadhani hata mwakilishi akisema nini hataweza kuaminiwa kwa sababu wananchi watakuwa wanajionea wenyewe na wahenga walisema ‘mwenye macho haambiwi tazama.

Lakini Mhe. Spika, nasema hilo ni muhimu sana kwa sababu tusijefika pahala tukachukulia kwamba labda uwaziri ni mapozi tu na kutembelea gari kubwa, ukapiga suti nzito, ukabadilisha mpaka mwendo na hiyo si dhamira ya uwaziri Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ilikuwepo nyimbo wakati ule wa miaka ya mwanzo ya Mapinduzi tena aliimba mpiga kura maarufu wa Jimbo la Mji Mkongwe Chagali Lali alipokuwa akiimba uwaziri ni dhamana na nyimbo ile ni maarufu sana ile kwamba "ukipewa uwaziri lazima kutulizana", kwamba uwaziri ni uongozi na ina maelezo mengi sana na wala sikusudii kwa leo kughana hapa na nimemuachia kazi Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ambaye aliimaliza jana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kinachokusudiwa katika nyimbo ile ni kwamba tumeusiwa kuwa uwaziri si mapozi, isipokuwa uwaziri ni kuwajibika na kuwatumikia wananchi. Katika hilo Mhe. Spika jambo muhimu sana ni kutokuwa na unafiki, tuongozwe na dhamira ya ukweli. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wiki iliyopita nilisikitika sana kwamba kuna Mjumbe mmoja wa baraza la Wawakilishi ni mwenzetu ambaye katika awamu iliyopita alikuwa na nafasi kubwa ya uongozi. Sasa wiki iliyopita alifanya mkutano wa hadhara na katika maelezo yake ambayo yalikaririwa katika vyombo vya habari na mpaka leo hayakukanusha bila ya shaka ni sahihi, alisema kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imefanya vitendo vingi vya ufisadi na akataja upotevu wa mamilioni na hata kutuhumu serikali kwamba haichukui hatua, haki yake.

Lakini nilisikitika Mhe. Spika, kwa sababu kama nilivyozungumza kwamba tuache unafiki, kwa nini? Mheshimiwa huyu ni Mjumbe katika Baraza hili lakini hakuchangia hapa na hoja yangu ni nini Mhe. Spika? Kwa kweli kama tunaongozwa na dhamira ya kweli ya uongozi na ukweli, uaminifu pamoja na uadilifu basi yeye alikuwa kiongozi mkubwa katika serikali iliyopita.

Kwa hivyo, kama alikuwa anayaamini yale kwamba serikali aliyokuwa akiitumikia kwa nafasi kubwa ulikuwa inafanya pengine mambo ya ufisadi, nadhani dhamira ya ukweli ingemtuma angekataa kuitumikia na angewajibika wakati ule kwa kujiuzulu. Mhe. Spika, mambo haya si mageni achilia mbali kwamba hukubaliani na jambo fulani, nimechukua mfano kwa ajili ya kuonesha ule umuhimu wa ukweli.

Mwaka 2002 mwezi wa Oktoba tarehe 23 aliyekuwa Waziri wa Elimu wa Uingereza akiitwa Bibi Estelle Morris alimuandikia barua Waziri Mkuu wake Mhe. Tony Blair

akamuomba ajiuzulu. Mhe. Spika, katika barua ile jambo la kufurahisha ambalo nadhani tunapaswa kujifunza kwa wenzetu, kwamba hakujiuzulu kwa sababu ya kashfa wala kwa kutuhumiwa kwa jambo lolote, isipokuwa alijiuzulu kwa sababu alimwambia Waziri Mkuu wake kwamba kazi aliyompa anahisi hana uwezo nayo.

Mhe. Spika, kwa sababu kabla ya kuwa waziri alikuwa Naibu Waziri na kwa mfumo wa Uingireza wanawaita *Ministers* na wale Mawaziri wanaitwa *Secretary of State* na wale *Junior Ministers* au Mawaziri Wadogo kila mmoja hupewa dhamana yake na huyu alipewa dhamana ya skuli na walimu na katika barua yake ambayo ninayo hapa Mhe. Spika, ambayo alimuandika Waziri Mkuu.

Mhe. Spika, alimwambia nilikuwa na uwezo mkubwa na nilifanya vizuri nikiwa na ile nafasi ya Waziri Mdogo katika masuala ya kusimamia walimu na maskuli, lakini katika hii ya kusimamia mikakati pamoja na uongozi wa Wizara ya Elimu naona nimeshindwa siiwezi, kwa sababu hiyo nitakuwa siwatendei haki wananchi wa Uingereza kwa sababu sitaweza kuwajibika ipasavyo. Kwa hivyo, naomba uniachie.

Kwa kweli barua hii ina mafunzo mazuri sana, kwa sababu anamwambia Waziri Mkuu humu kwamba nilipokuja kukuona kukuomba nijiuzulu ulinishawishi kwamba niendelee na ukanitaka nikafikiri tena, nimefikiri tena usiku wa kucha bado naamini kwamba fikra niliyonayo ni sahihi naomba nijiuzulu bibi huyu Estela Morris akajiuzulu akawacha heshima kubwa sana.

Sasa haya Mhe. Spika, tujifunze na sisi isiwe umekula raha za utawala ee! Ukakutumikia mpaka siku ya kuukabidhi halafu baadaye unakuja kupanda majukwaani kwa sababu pengine ya mambo mengine unakuja kuyakana yale ambayo uliyasimamia. Kwa hivyo, huo si uadilifu wala si ukweli Mhe. Spika, huo utakuwa na sijui niuite vipi, lakini niseme kwamba wananchi wa Zanzibar wasionekane labda ni wajinga kwamba hawayaoni haya.

Mhe. Spika, haya nimetaja kwa waliopita, lakini niwaombe na mawaziri wa hivi sasa wajifunze tusije tukafanya kosa kama hili waone kwamba uwaziri si mapozi wala kubadilisha mwendo ama gari kubwa, isipokuwa uwaziri ni utumishi wa dhati kwa wananchi ambao wametuchagua kutuleta kuwashughulikia katika serikali hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, sasa nije katika yale ambayo yamo kwenye ripoti, kama nilivyosema kwamba ninaipongeza sana serikali. Sasa moja ambalo limeibuka kwenye taarifa hii ya serikali Mhe. Spika, ni kwamba bado kuna maeneo ambayo kamati iliyatolea maoni kwamba yachukuliwe hatua za kisheria na serikali imetujibu kama

ilivyokuwa kwa ripoti iliyopita, kwamba yanapelekwa katika Jeshi la Polisi au mengine yamepelekwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo yanahitaji masuala ya ushauri wa kisheria, ili hatua ziweze kuchukuliwa vizuri.

Mhe. Spika, nilipochangia ripoti iliyopita nilisema wazi wazi kwamba mimi ninaunga mkono kwa kufuata taratibu kwamba huwezi kupeleka kesi kutoka Baraza la Wawakilishi moja kwa moja ukaipeleka Mahakamani, lazima tufuate taratibu kwa kufika Polisi, kwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na baadaye ndio uende mahakamani. Mhe. Spika, nimeona nilisema hili kwa jumla kwa sababu moja tu, kwamba nilichangia wakati ule na leo narejea tena, kwamba kwa Jeshi letu la Polisi na hali tunayoiona katika kesi nyengine uwezo wake unaonekana umekuwa mdogo.

Vile vile, inaonekana si kwa kesi hizi hata kesi nyingi zinazopelekwa mahakamani kupata uthibitisho wa madai inakuwa kazi kubwa sana, tunaliona hili na hata kwenye ripoti mbali mbali zilizotolewa zinathibitisha. Kwa hivyo, hii mara nyengine inaonekana ni uwezo mdogo katika masuala ya uchunguzi na pengine uwezo mdogo kwa maana ya maarifa na elimu pamoja na taratibu za kisasa za kufanya uchunguzi. Pia nikutokana na uwezo mdogo wa kibajeti.

Mhe. Spika, naomba kama serikali imeamua mambo haya kimsingi kuyapeleka kule, basi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pia ndio inayosimamia masuala ya Muungano, ione vipi inaliimarisha Jeshi la Polisi kwanza kwa kuwajengea uwezo wa kitaalamu, lakini hata wa kibajeti kwa ajili ya kufanya kazi zao vizuri, ili haya yasijeyakafika pahala wananchi wakaona kwamba yanapelekwa kule ikawa serikali inaondosha njiani, kwa sababu kama hayachukuliwi hatua watakuja kuona hivyo na hilo ni moja.

Pili, Mhe. Spika, ni lile linalosemwa kwamba kuna mambo mengi humu yameambiwa yamepelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, namuonea huruma sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa sababu hali ninavyoiona sana ni kwamba mambo mengi, ili kujaribu kuhakikisha kwamba tunafuata sheria basi yanapelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni jambo sahihi.

Lakini nadhani jambo la msingi ni kwamba serikali iimarishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa sababu picha tunayoiona sasa ni kama vile kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imekuwa ni mwanasheria Mkuu yeye mwenyewe basi na wala sisemi kama hawapo wanasheria. Sasa hata miswada tunayoipitia hapa mara nyingi Wawakilishi wako Mhe. Spika wameshawahi kusema kwamba utaona kuna makosa na mapungufu mengine

kwa sababu inaonekana kama haikupitia katika jicho la Mwanasheria Mkuu mwenyewe basi kuna tatizo.

Katika hali kama hii hatuwezi Mhe. Spika, kwa sababu tutamchosha na inaweza ikafika pahala hata akakosa ufanisi Mwanasheria Mkuu wetu mzuri, makini kwa sababu tunampa kazi nyingi. Kwa hivyo, ndipo nikasema kama serikali imeamua kwamba haya mambo ya msingi na leo tunasema hata mambo ya Baraza la Manispaa mikataba yake ikitaka kufungwa basi ipelekwe katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ni jambo sahihi lakini ikiwa kila jambo mpaka alipitie Mhe. Othman Masoud Othman kwa kweli Mhe. Spika, tutamchosha.

Kwa hivyo, serikali ni vyema iimarishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na tayari tumeshaipitishia sheria ofisi hii, nadhani hilo ni muhimu sana Mhe. Spika, yafanywe nasema tena kwamba Polisi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili tuweze kupata hiyo tija ambayo tumekusudia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba nigusie maeneo machache yaliomo kwenye ripoti kutokana na taarifa ya serikali. Moja Mhe. Spika, serikali tunaiomba sana kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ijifunze kuchukua hatua kwa wakati, kwa sababu hii ripoti Mhe. Spika nakumbuka iliwasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi mwezi wa Oktoba, 2012. Mhe. Spika, imechukua mwaka mzima kuleta ripoti hii na bila ya shaka katikati iliwahi kuleta ripoti na kuikataa Baraza la Wawakilishi.

Lakini nataka kuiambia serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kuna ule usemi unaosema kwamba "*haki inayocheleweshwa ni sawa na haki iliyozuiwa''* au ambayo haikutolewa "*justice delayed is justice denied*".

Mhe. Spika, katika ripoti hii kuna watu wawili ambao wametajwa wameshafariki dunia, katika kipindi cha tangu tumechunguza na kuleta hapa mpaka leo na hawa walikuwa wanahusika kwa njia moja au nyengine. Kwa kweli najua si serikali wala si chombo hichi kinachoweza kumzuia Mwenyezi Mungu asifanye kazi yake ya kuchukua roho yake akiamua.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema kwamba mara nyengine tunapochelewesha inaweza yakatokea mambo kama haya na watu wanaona kwamba mpaka mtu anaaga dunia hakutendewa haki na hiyo hata wewe unayehusika ikawa inakukwaza katika nafsi yako kusema kwamba hii sikutendewa.

Mhe. Spika, watu wawili ambao wameshatangulia mbele ya haki na kwa sababu bahati nzuri angalau mmoja wao alikuwa ndani ya Mji Mkongwe, lakini wote wanafanyashughuli zao katika maeneo hayo. Mmoja ni marehemu Rashid Ali Halfan ambaye ni katika wale watu wawili waliokuwa wamepewa tenda ya kujenga maduka katika Soko la Darajani au Marikiti. Mhe. Spika, wapili ni ndugu Nassor aliyekuwa na Duka la *Diplomatic Supermarket* Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema wote na sisi atupe mwisho mwema.

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba mara nyengine tukichelewesha ndio kama haya yanaweza kuwa hata yasikamilike vyema kwa sababu kuna mambo mengine pengine ya ushahidi sasa ikawa ni tabu kuyapata.

Vile vile, jambo jengine ni kwamba wanazo haki zao. Kwa hivyo, naomba kama kuna haki ya mtu isijeikawa kuondoka kwake ndio mwisho wake, kwa kweli hawa bila ya shaka wanao warithi wao basi ni muhimu kufuatiliwa, ili kuona pale panapo haki yao, basi haki ile inapatikana.

Nikiendelea na mchango wangu kuna suala jengine ambalo limejitokeza humu ndani pametajwa kwamba baadhi ya mambo ambayo tuliyoyapendekeza kutachukuliwa hatua kupitia Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa. Mhe. Spika, suala hili limeshachukua muda mrefu sana na kila siku ahadi tu ya Sheria ya Serikali za mitaa hatuioni na hata leo tumepewa miswada hapa ambayo itakuja kusomwa hapa kwa mara ya mwanzo, ili ije kujadiliwa katika kikao kijacho bado Serikali za Mitaa mswada wake haumo na kila siku tunaahidiwa na tayari tumeshapewa mpaka semina Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na mswada huu bado haujaja.

Sasa Mhe. Spika, tujue kwamba tunaposema kuna marekebisho ya sheria hiyo na halafu ikawa haiji, maana yake marekebisho hayo tunayakwamisha na badala yake tunataka kufanya mambo yaendelee kama ambavyo yamekuwa yakifanyika.

Mhe. Spika, niiombe serikali kupitia kwako Mhe. Spika, mbali ya kuangalia Sheria ya Serikali za Mitaa, humu katika Ripoti yetu ya Kamati Teule tuligusia mara nyingi kuhusu suala la kukiukwa kwa Kanuni zinazoongoza Baraza la Manispaa. Lakini moja ambayo tuliligundua wakati ule hata zile Kanuni zenyewe nazo zimepitwa na wakati, yaani kuna maeneo mengi zinahitaji marekebisho. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani pia na hili sikuliona humu kwamba serikali ione haja ya kulisaidia Baraza la Manispaa kuzipitia upya Kanuni zake, ili ziendane na mahitaji ya wakati huu.

Kanuni zile nimeziangalia Mhe. Spika zimetungwa tangu kama sikosei kwenye mwaka 1995 wakati Mhe. Ali Abdalla Ali akiwa Waziri wa Nchi, (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ ndio kuna saini yake pale tumeziona. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kuzipitia upya.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nataka nilitolee maoni ni kuhusu baadhi ya mambo. Kwa mfano kuna maeneo Mhe. Spika, ambapo serikali imesema wahusika wanaweza kwenda mahakamani. Kwa kweli suala hili kidogo limenipa shida ambalo liko kwenye ukurasa wa 22 na 23 hoja nambari 14. Mhe. Spika, hii inahusu suala la kuwatoza ada ya usafi wafanyabiashara wanaopanga biashara zao ndani na nje ya maduka kwamba ni dhuluma.

Sasa serikali kwenye ukurasa wa 23 inasema kwamba ikiwa wanahisi kuwa hawatendewi haki basi wanaweza kupeleka malalamiko yao mahakamani kwani Baraza lina hadhi ya shirika na linaweza kushtaki na kushtakiwa ni sahihi Mhe. Spika. Lakini tuzione mahakama zetu na tuone ugumu wa utaratibu wa kupeleka kesi mahakamani na hasa gharama za kupeleka kesi mahakamani, kwa sababu hawa ni wafanyabiashara ndogo ndogo wanaouza tungule, pilipili, mboga mboga pale.

Mhe. Spika, unapowaambia hawa wakafungue kesi maana yake watafute wakili na tunajua sote gharama za kesi hii, kwa sababu suala hili lishughulikiwe kiutawala nadhani ni vyema serikali yenyewe itafute njia ya kulitafutia ufumbuzi hili na inaliweza kwa sababu mamlaka hizi ziko chini yake na kuliko kuliondosha njiani kwa kusema kwamba hawa wapeleke kesi yao mahakamani.

Vile vile, kuna suala ambalo nataka kulizungumzia la kadhia ya watu waliojenga katika Soko la Darajani. Kwa kweli ripoti ilisema na pia serikali imesema kwamba imekubaliana na kamati ambapo hatimaye ripoti yake imeridhiwa na Baraza hili Mhe. Spika, kwamba hawa wahusika wawili ndugu Suleiman Mselem Nassor na marehemu Rashid Halfan Ali walipewa tenda, lakini katika suala zima la hiyo tenda yenyewe ya kujenga hayo maduka pana kizungumkuti kikubwa katika utaratibu wenyewe waliopewa pamoja na mikataba yenyewe, kwa sababu wameambiwa wamepewa na ile Kampuni ya *SMK Enterprises Limited*, lakini hapo hapo mikataba wamefunga na Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, si hayo tu wameambiwa watajilipa baadaye, lakini mikataba baina ya wao na wale waliokodishwa maduka waliyajenga wao yote ni sawa sawa na wala hakuna utaratibu wa kujilipa wao na mpaka leo wanalalamikia haki zao. Mhe. Spika, wengine wanatuhoji hivyo nyie Baraza la Wawakilishi kazi yenu kuja kutwita na kutuhoji na kuahidi kwamba mtashughulikia haki zetu halafu baadaye kimya tu. Kwa hivyo, nafikiri

serikali hili ilifuatilie na haya maelezo ambayo wametoa kwamba na wao pia wafikirie kupeleka mashauri yao mahakamani kwa ajili ya kulishtaki Baraza la Manispaa, nadhani hilo halikuwa sahihi kwa upande wa serikali.

Kwa kweli kuna maeneo kadhaa humu serikali imesema kwamba imeliagiza Baraza la Manispaa kufanya malipo katika mambo mbali mbali ambayo yalikuwa yanadaiwa. Sasa kwa nini katika hili kwa sababu imeridhika na vielelezo ambavyo vimetolewa na serikali imesema kwamba imeridhika na maelezo ya kamati pamoja na ushahidi ambao umetolewa. Kwa hivyo, kwa nini isichukue hatua za kiutawala tu na kuliambia Baraza kama kuna haki yao basi wapewe haki yao na badala ya kusema waende mahakamani, hilo Mhe. Spika sikuridhika nalo.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni lile suala lilioko kwenye ukurasa wa 29 linalohusu maeneo ya masoko kujengwa maduka badala ya utoaji wa huduma za kisoko. Mhe. Spika, serikali katika maelezo yake imesema katika kuendeleza mambo ya kisasa badi mambo haya yanafanyika, ni kweli Mhe. Spika. Lakini soko au tulivyozoea kuita hapa kwetu marikiti ni pahala ambapo tumezoea kufuata mahitaji maalumu, kilichopo Mhe. Spika unachokiona si kweli kwamba Baraza la Manispaa au mamlaka nyengine yoyote inapotoa maeneo yale kuimarisha kwamba ina lengo la kufanya mazingira yawe mazuri zaidi.

Mhe. Spika, kama ni hivyo bado ingefanywa mazingira mazuri zaidi, lakini wale watakaobakishwa ni wale wale wanaotoa huduma kwa kupewa maelekezo namna ya kutoa huduma zao. Lakini kinachofanyika ni kwamba wale wanatolewa wanakoseshwa pahala pa kutafuta riski Mhe. Spika na badala yake wanaletwa watu wanafungua maduka haya ya kutoa huduma ambazo tumezizoea mitaani.

Kwa hivyo, kila siku tunalifinya soko au marikini zetu, zinakuwa badala ya kutoa zile huduma zilizokusudiwa zinageuzwa ni mwahala mwa maduka. Kwa mfano, tukaangalie eneo la Darajani leo Mhe. Spika panauzwa *perfume* na mengine yanauza vifaa vya kuandikia (*stationeries*) na ukija huku kwenye Soko la Mboga Mboga maduka yaliyojengwa pale leo yanauza bidhaa kama ambazo unazipata kwenye maeneo ya makontena ya Darajani.

Sasa zile huduma hasa za kisoko au marikiti tulivyozoea tunavyoita sisi za kupata mboga mboga, matunda, vyakula vinavyopikwa, samaki au nyama zile kila siku tukijenga maeneo yale zitapatikana wapi Mhe. Spika, na ndio maana hali ya mchafu koge

unayoiona katika soko ni kwamba kumezidiwa kwa sababu ndani yake zile huduma hasa zinahamia nje kwani tunazitoa katika maeneo yake yaliyokuwa yamekusudiwa tangu mwanzo. Mhe. Spika, hili sikubaliani na serikali kwa hiyo iangalie tena na hata kama imeamua kubadilisha mazingira yawe mazuri, basi iwe kwa nia ya kuwarejesha wale wanaotoa huduma badala ya kuwapa wenye maduka.

Mhe. Spika, naomba unipe dakika tano nimalizie. Jengine ambalo limejitokeza katika ripoti hii kwenye ukurasa wa 33 na 34 ambalo linathibitisha maelezo ambayo yaliyokuwa yametolewa na kamati, kuhusu suala la huduma za uimarishaji mazingira katika Manispaa yetu. Kwa mfano, yale mambo ya kuweka viguzo, sehemu za kupitia wananchi wanaokwenda kwa miguu, bustani zake, mabwawa pamoja na mambo mengine nataka kuyakusanya yote kwa sababu ya muda sitaki kuzungumza moja moja.

Serikali imeridhika na kamati kwamba kuna utaratibu wa kuwapa watu binafsi wengine walikuwa wafanyakazi wa Manispaa. Kwa mfano, kuna huyu bwana mmoja anaitwa Ali Kibasi ndio imekuwa kila huduma anapewa yeye, lakini alikuwa mfanyakazi na baadaye akaacha kazi, badala yake inaonekana kwamba kulikuwa na maelewano fulani na wakubwa pale kwamba anapewa kazi hizi nje ya utaratibu wa manispaa. Hata hivyo, lakini anatumia mafundi na hata wakati mwengine mpaka vifaa vya Manispaa na huduma zenyewe zimeonekana ziko chini ya kiwango Mhe. Spika, kwa sababu vingi ukivitizama vile viguzo vinaanguka ovyo Mhe. Spika kwa taharuki ndogo vikipata, pengine ujenzi wake sio wa viwango.

Mhe. Spika, serikali imesema jambo zuri sana humu kwamba inakubaliana na kamati kuwa huduma hizo zitolewe na Manispaa yenyewe na hili ni sahihi. Lakini maana yake Manispaa nayo ijikite katika kufanya hizo kazi badala ya kugeuka zaidi wakala wa kutafuta biashara. Kutokana na hali hii, Mhe. Spika Manispaa yetu imebadilika badala ya kuwa watoa huduma wamekuwa zaidi ni watafutaji wa mapato na ingekuwa haya mapato baadaye yanatumika katika kuimarisha huduma zake ingakuwa ni jambo la maana, lakini sivyo inavyofanyika. Kwa hiyo, Mhe. Spika nasisitiza sana Manispaa kufanya kazi zake.

Mhe. Spika: Mhe. Ismail Jussa Ladhu, muda.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: La mwisho kabisa Mhe. Spika, ninalotaka kulizungumza ni kwamba katika ripoti yetu ya Kamati Teule tulibainisha maeneo mengi sana ambayo

yalikuwa yanalalamikiwa wale waliokuwa wakifuatia huduma mwanzo hukosa haki zile Mhe. Spika, baada ya kuwa maeneo yao wamenyang'anywa au wengine kama hivyo wameambiwa walipie vibaraza katika Soko la Mwanakwerekwe gharama hazitambulikani walizoambiwa na ni tofauti walizolipishwa. Tarehe za kulipishwa mikataba haifahamiki. Sasa naomba serikali iwatizame sana hawa, kwa sababu hawa wakijakupoteza imani na vyombo hivi vya utawala, wanatuona tunaunda Kamati, tunakwenda kufuatilia lakini baadaye hakuna hatua zinazochukuliwa wanaweza wakatafuta njia za mkato.

Mhe. Spika, tumeona katika nchi nyingi machafuko yameanza kwa sababu wananchi wameanza kutopoteza imani na taasisi za kiutawala. Tusifike huko, wananchi wa Zanzibar ni watu wasikivu, ni watu waliozowea kutii mamlaka za utawala zilizokuwepo, tusije tukawasukuma kwenye ukuta wakatafuta njia nyengine. Mhe. Spika, naiyomba sana serikali ijifunze katika hili ili wajenge imani.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, hili linahusu jimbo langu, naomba tena, mara nyingi tuliwahi kusema kwamba kuundwa kwa Kamati teule kusiwe sababu yakuwakomoa wale ambao wameingizwa katika Kamati Teule zile. Niliwahi kusema Mhe. Spika, baada ya kuundwa Kamati Teule ile tukaanza kazi Baraza la Manispaa lilikuja ghafla kuchukua hatua kwa wananchi wa Mji Mkongwe kuwapandishia katika hali isiyokuwa ya kawaida gharama au ada za *Land Rate,* ambazo kimsingi tayari Baraza hili tumeshafanyia marekebisho, zikahamishwa kutoka Baraza la Manispaa zikapelekwa kwamba zikusanywe na *ZRB*. Baraza hili lilipitisha marekebisho ya Sheria lakini Manispaa imeng'ang'ania na tafsiri yangu walikuwa wanakomolewa kwa sababu Mwakilishi wao kashiriki katika Kamati hii na kwamba kafichua uouvu uliokuwa ukifanywa.

Naomba Mhe. Spika, serikali ifuatilie na mimi niliwaambia wananchi kwamba wasilipe zile gharama walizokuwa wamepandishiwa na mpaka leo nawambia wasilipe. Kama kulikuwa kuna haja ya kupitia ilikuwa tukae na *ZRB* tuone wanalipwa mamlaka yale, lakini Manispaa kuchukua mamlaka yale kwenda kuwakomoa wananchi kwa sababu tu na haikuwa sehemu yote ya mji ilikuwa kwa Mji Mkongwe tu, kwa sababu ya kukomoa watu fulani, Mhe. Spika, tabia hii si nzuri.

Baada ya kusema hivyo Mhe. Spika, nataka niseme naiyunga mkono taarifa ya serikali katika hili lakini naomba sana yale maeneo ambayo tumeyatolea maoni yakafanyiwe kazi

na yale ambayo serikali imeahidi kuyafanyia kazi basi baadaye tupewe ripoti kwamba yamefikia wapi. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru na mimi kwa kunipatia fursa hii, lakini kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai wake tukaweza kukutana hapa. Pia nimshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri ambaye amewasilisha hoja hii kwa jinsi alivyokuwa mfasaha katika usomaji wa ripoti yake.

Mhe. Spika, mimi kwanza napenda nichukue fursa hii kuipongeza sana serikali kwa hatua ambazo wameonekana kuzichukua katika ripoti ambayo wametuletea jana lakini na hii ambayo ipo leo mezani.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme pamoja na pongezi ambazo tunaipongeza serikali lakini pia tunaiyomba sana serikali kuwa makini sana katika kushughulikia masuala yale ambayo yanakuja mbele yetu. Napenda kusema hivyo kwa sababu serikali hii tusingependa ifanye vibaya hasa tukitegemea mwaka 2015 tunatarajia kurejea tena kwa wananchi wetu na kwenda kuomba ridhaa zao. Kwa hivyo tungependa serikali iweze kufanya vizuri ili tunaporudi kwa wananchi wetu basi tuwe na majibu mazuri ambayo yatakuwa hayana kigugumizi.

Mhe. Spika, sisi wawakilishi tunakuwa wakali sana na si kama ukali wetu labda kwamba tunaichukia serikali au labda tunawachukia Mawaziri wetu, hapana. Mhe. Spika, tunaipenda sana serikali yetu na tunaiyombea kheri kila wakati iweze kwenda vizuri ili tuweze kupata mafanikio mazuri.

Lakini kwa nini wawakilishi tunakuwa wakali, ni kwa sababu ya dhima ambayo na sisi tumepewa na wananchi wetu kutoka katika majimbo au kutoka katika Mikoa yetu. Wenzetu wametupa dhamana hii kwa kutuamini kwa kutuleta hapa kwa kusema hawa wenzetu tunaowatuma waende wakatuwakilishe basi wanaweza wakatuwakilisha vizuri. Ndio maana tunapoona yanatokea mambo ambayo hayaendani na utaratibu au ubadhirifu unatokea katika serikali na tukijua sisi tumetumwa na wananchi kuja kusimamia haki zao hapa, ndio maana tunakuwa wakali katika kuikemea serikali ili tuone na sisi tunatimiza ule wajibu ambao wametutuma wenzetu.

Mhe. Spika, mimi ni mwakilishi wa viti maalumu kutoka Mkoa wa Kaskazini, Wanawake wa Mkoa wa Kaskazini ndio ambao wamenisababisha nikaweza kufika katika jengo hili. Na wanawake hawa wanamatumaini makubwa na wana imani kubwa na Chama cha Mapinduzi ambacho wanajua ndio mkombozi wao. Nasema hivyo kwa

sababu na serikali iliyopo madarakani inaongozwa na Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, ni imani yangu lazima tuwasimamie wanawake hawa au wananchi wote wa Zanzibar waweze kutendewa haki kwa manufaa ya wote.

Mhe. Spika, Wawakilishi tunazidi kuwa wakali tunapoona lengo na dhamira hasa ambayo imeletwa na muasisi wetu hayati Abeid Amani Karume inaendewa kinyume. Lengo la muasisi huyu ameleta mapinduzi kwa sababu ya kuona anataka wananchi wote wa Zanzibar waweze kufikia katika maendeleo mazuri, waweze kuwa na maisha bora, waweze kupata huduma bora. Kwa hivyo, kuona watu wachache ndio wanafaidika na matunda yale ya mapinduzi hii ndiyo inayosababisha kuona Wawakilishi labda wanapanda hasira sana, kwa sababu lile lengo linakuwa halikufikiwa.

Mhe. Spika, mimi naiomba sana serikali, ripoti hii tumeiyona na hatua ambazo wamechukua tumeziona na ambazo bado hazijachukuliwa pia tumeziona, tunaiomba sana serikali kwamba bado isije ikaridhika baada ya kupitisha ripoti hii katika Baraza hili wakasema Wawakilishi wameshaipokea ikawa ni basi. Lazima serikali iendelee na utaratibu wa kuona wale ambao watagundulika wana hatia basi waweze kuchukuliwa hatua za kisheria, ili iweze kujenga imani kwetu lakini pia kwa wananchi wetu ambao wametuleta katika vyombo hivi.

Mhe. Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wetu Dokta Ali Muhammed Shein, nampongeza kwanza kwa sababu ya uwadilifu wake. Rais huyu ni muadilifu wala hana tamaa ambayo imepindukia mipaka. Na hili linapaswa kwa mwanadamu yeyote kuwa na tamaa ya kiasi kwa sababu tumeambiwa tamaa tuwe nayo lakini iwe ya kiasi sio ya kupindukia mipaka. Kwa hivyo, Mhe. Rais wetu anatuonesha mfano mzuri na tunapaswa sisi ambao tupo chini yake basi kuiga mfano wake ili tuweze kuwa na mustakbali mzuri katika kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, mimi niwaombe watendaji wetu ambao wapo serikalini, wawe waadilifu, waweze kuwafanyia kazi wananchi wa nchi hii katika njia ya uadilifu wakijua kufanya hivyo wanajijengea heshma wao wenyewe lakini pia wanatekeleza wajibu wao kama inavyowapasa.

Mhe. Spika, niiyombe tena serikali pamoja na ripoti hizi ambazo zimekuja mbele yetu serikali bado iendelee yenyewe kufanya uchunguzi katika taasisi zake ambazo zipo zimebaki na isisubiri mpaka ikaundwa Kamati Teule. Lakini kwa sababu wao wana wajibu wa kuwasimamia watendaji wao basi ni lazima wajipange kuona wanaendelea

kuwasimamia watendaji ili waweze kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa na nchi hii.

Mhe. Spika, mimi nilitaka niseme tu kidogo katika ripoti hii kwa sababu ya kuona sisi Wawakilishi tuna wajibu na lazima wajibu huu tuwaufikishe na lazima tuseme pale panapokuwa na makoseo, lazima tushauri pale tunapoona unahitajika ushauri. Naomba serikali izingatie na ituone Wawakilishi kama sisi hatuna chuki nao, lakini bali tunataka serikali yetu ifike katika mafanikio yaliyokuwa mazuri kwa pamoja.

Mhe. Spika, mimi sina mengi ya kuzungumza, lakini naomba nichukue fursa hii kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na kuiomba serikali iendelee na utekelezaji wake kama ilivyojipangia. Ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia ripoti hii au taarifa hii ya serikali juu ya hoja zilizotolewa katika ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Baraza la Manispaa. Kamati ambayo mimi nilikuwa ni Mwenyekiti wake. Kwa hivyo, nakushukuru kwa kuniteuwa katika Kamati ile, lakini pia niwashukuru na wajumbe wenzangu kwa kuniteuwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Spika, nilipata taarifa kuwa ulikuwa unanitafuta asubuhi baada ya Mhe. Waziri kuwasilisha ili nitoe maoni lakini nadhani kwa kuwa jana ulipata safari mimi sikuweka hati mezani kwa ajili ya kutoa ripoti. Na nilimwambia Katibu kwamba asiniweke kwa sababu sina mchango wa Kamati katika hili sina maoni isipokuwa nitatoa maoni yangu mimi mwenyewe binafsi. Kwa sababu sikupata nafasi ya kukaa na Kamati yangu kujadili ripoti hii.

Mhe. Spika, itakuwa si vyema nikasimama kutoa maoni ambayo sijakaa na wenzangu na kwa sababu ripoti hizi ni kubwa zina hitaji maamuzi, pengine naweza kuja nikaiyunga mkono au nikaikataa wajumbe wangu wakaja wakanambia hapana hayo ni maoni yako. Kwa hivyo, niliogopa nikamwambia sina hoja ya kamati isipokuwa mimi mwenyewe nitachangia kama mjumbe, na wajumbe wenzangu watachangia na wao kama wenyewe walivyoiyona hiyo ripoti yenyewe. Nashukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameshatoa maoni yake mengi hapa na bahati nzuri ameunga mkono baada ya kutoa masahihisho ya hapa na pale.

Mhe. Spika, ripoti imewasilishwa, imeonekana namna ya utekelezaji wake, pamoja na kwamba kuna baadhi ya mapungufu ambayo yameonekana. Hii kwanza Mhe. Spika,

natumie nafasi hii kumpongeza sana Mstahiki Meya wa Manispaa ya Zanzibar na nimpongeze kwa makusudi kwa sababu baada ya kutolewa ripoti hii na kutakiwa serikali ianze kutekeleza yeye mwenyewe Mhe. Meya alianza kufuatilia kwa sababu tulikuwa tunawasiliana, akataka nimpe moja kati ya *copy* za ripoti ili aweze kupata nafasi ya kuanza kutekeleza yale ambayo alikuwa ana mamlaka nayo kuyatekeleza.

Nadhani katika utekelezaji ule imetupa urahisi katika utekelezaji wa jambo hili, kwa sababu hatuta kusubiri. Katika mambo mengi ambayo tuliyapendekeza Mstahiki Meya alianza kuyachukulia hatua. Lakini pia hata Mkurugenzi mpya ambaye ameteuliwa na Mhe. Rais na yeye amefanya vizuri, amechukua juhudi ya kushirikiana na Mstahiki Meya ili kuondosha zile kasoro zilizoonekana na kamati. Kwa hivyo, niwapongeze wote, nimpongeze Mstahiki Meya pamoja na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa na kwa kweli niwaombe waendelee kuwa na mashirikiano katika kusimamia chombo kile wakishirikiana na Madiwani wao.

Mhe. Spika, mimi kwa bahati nzuri nimekitumikia chombo kile pale mwanzo kilipoanzishwa kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 1995. Sheria ile ambayo ilikuwa ya mwanzo kuanza kutumika katika mfumo ule. Sheria ambayo kwa sasa hivi ina takriban miaka 18. Kwa hivyo, sheria huwezi kuyaona mapungufu yake hadi pale unapoanza kuitekeleza. Sheria yetu ina mapungufu mengi inahitaji sasa ianze kushughulikiwa kwa kuandikwa upya. Miaka 18 ni mingi na sheria ile ilikuwa ndio kwanza. Ili chombo hiki kiweze kwenda vizuri na kiende na wakati basi kuna haja ya kufanya mapitio ya sheria ile ili sheria sasa iendane na wakati.

Mhe. Spika, chombo kile kimetungiwa sheria, kina kanuni zake, lakini pia kuna sheria zile za serikali kama vile sheria za fedha na sheria za mitaji ya umma za kiserikali ambayo nazo sheria zile chombo kile hutakiwa kuzifuata katika masuala ya manunuzi na mambo ya matumizi ya fedha. Kwa hivyo, wamekuwa wakitawaliwa na sheria nyingi ile ni sheria yao na kanuni zao lakini na zile sheria za serikali ambazo zipo kwa mujibu wa namna ya utekelezaji hasa katika maeneo ya manunuzi na masuala ya utumiaji wa fedha. Kama tunavyojua, kwamba taasisi ile ina maeneo makubwa sana yanayohusu masuala ya manunuzi na masuala mengine ya fedha. Kwa hivyo, pia huwajibika kuzifuata sheria hizo.

Moja kati ya tatizo kubwa ambalo linaonekana lipo ni namna ya utekelezaji au kufuata sheria. Ripoti hii inaonesha kwamba katika chombo kile kilikuwa kinakwenda hivi hivi kama vile ni taasisi ya mtu binafsi, hakuna sheria zile zinazofuatwa na hata zile kanuni

ambazo wenyewe wamejitungia nazo zilikuwa hazifuatwi. Hata zile sheria za fedha zilikuwa hazifuatwi na hata sheria za manunuzi pia zilikuwa hazifuatwi. Ushahidi wa ripoti hii unaonesha na kuna ushahidi mwingi unaonesha juu ya jambo hilo. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba pale palikuwa hapafuatwi taratibu zile za kisheria ambazo zipo.

Kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba kanuni zile zilikuwa za muda mrefu, tuliona hilo. Na kweli zilikuwa zinahitaji kufanyiwa marekebisho. Lakini utakuta bado zilikuwa zinafanya kazi na tulipozungumza nao walikuwa wanasema kwamba maana yake kiwango hiki kidogo. Lakini sasa kanuni ipo, itabidi ni lazima ifuatwe kama haijafanyiwa marekebisho, kutokuifuata kanuni ile maana yake ni kwenda kinyume na sheria au ifanyiwe *amendment*. Kwa hivyo, kuna haja sasa ya kuzipitia sheria na kanuni zilizopo. Tunashukuru Wizara ya Fedha nayo imekubali kuzifanyia mapitio sheria za manunuzi na sheria za fedha ambazo na wao wanafanya mchakato wa kuzirekebisha, ili zote kwa pamoja ziende kwa wakati na wenzetu hawa watendaji waweze kutekeleza sheria zile.

Kwa hivyo, mimi nashukuru hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa ambapo Mhe. Waziri amezieleza katika kuhakikisha chombo hiki kinafuata sheria. Jengine ambalo linaonekana lipo katika taasisi zile ni mivutano ambayo mara nyingi inakuwepo. Hata wakati wangu nilipokuwepo kulikuwa na mivutano, na mivutano inayokuwepo pale ni kati ya Mkurugenzi na Meya, mara zote kunakuwa na mivutano, maana kila mmoja anajiona ana mamlaka katika chombo kile. Wakati sheria imeelekeza vizuri, katika hili haikubakisha. Meya imeeleza mamlaka yake na Mkurugenzi imempa mamlaka yake na madiwani na wao pia wana mamlaka yao juu ya sheria ile. Lakini Mkurugenzi wakati mwengine anafika pahala anasema mimi nimeteuliwa na Rais bwana.

Wakati mmoja Mhe. Spika, nilipokuwa nipo Manispaa wakati ule Mstahiki Meya alikuwa Maulid Salum na Mkurugenzi wangu alikuwa Mussa Juma, tuliwahi kufika pahala tukenda kumshtaki kwa Rais yule Mkurugenzi wakati ule alikuwa ni Dokta Salmin Amour ndiye Rais. Katika mashtaka yetu tulimshtaki kwa kukataa kutekeleza yale maamuzi ya *full council* kwa sababu sheria inamtaka Mkurugenzi atekeleze yale maamuzi ya *full council* lakini yeye alikuwa hataki anatekeleza vile ambavyo yeye inafaa na akafika pahala akasema sasa hata kama *full council* atanambia nikajenge nyumba katika viwanja vya Mnazi Mmoja maana yake mimi nikajenge tu.

Alifika kujenga hoja hiyo kwamba maamuzi mengine yanayopitishwa kwenye *full council* yanakuwa hayaendani na taratibu, lakini sasa sheria ndio imemtaka afanye hivyo, kwa sababu pale pana wanasiasa. Kwa hivyo, maamuzi ya chombo kile maana yake yanayotakiwa ni maamuzi ya wanasiasa, yakiwa ndivyo yakiwa sivyo yeye anatakiwa atoe utaalamu wake ili ionekana kwamba yale maamuzi ya chombo kile yanakwenda kwa mujibu wa sheria, lakini hawezi tena kufanya vyenginevyo.Hilo ndio limekuwa tatizo la chombo kile.

Lakini tunashukuru safari hii *Alhadulillah* inaonekana mwanga kidogo upo katika Baraza hili la sasa, kati ya Mstahiki Meya na Mkurugenzi, inaonekana wanakwenda vizuri na ndio maana yale malalamiko na malumbano yamepungua kwa kiasi kikubwa. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri akisimamie kwa karibu sana chombo hiki ili kuona kinakwenda vizuri na kinakwenda kwa mujibu wa sheria na kanuni na kama kuna kanuni zinahitaji kufanyiwa marekebisho basi zifanyiwe marekebisho ili ziweze kuendana na wakati.

Mhe. Spika, utekelezaji wa ripoti tumeuona lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo wenzetu wanahitaji kuyaangalia upya. Mhe. Ismail Jussa Ladhu kagusia hapa juu ya kuwataka baadhi ya watu wale pengine waliodhulumiwa haki zao kwenda Mahkamani. Nadhani si busara katika yale maeneo ambayo uchunguzi wa kamati umeonekana kwamba ni dhahir hawa watu wamedhulumiwa kwamba tuwatake waende Mahkamani.

Pamoja na kwamba chombo kile ndicho kinachotoa haki lakini kuna mambo ambayo yapo wazi na ipo haja ya serikali kuwasaidia watu hawa kwa sababu hawa ni wananchi wetu na vyombo hivi ni vyetu na Mahkama zetu tunazifahamu, zinavyokwenda, hatuwezi kuzungumzia lolote. Lakini ni vyema kama kweli kuna mtu amedhulumiwa na inaonekana kwamba kweli kadhulumiwa na serikali ikiridhika kwamba huyu mtu amedhulumiwa au amekoseshwa haki yake, basi ni vyema Baraza la Manispaa likamrejeshea haki yake.

Kwa mfano Mhe. Spika, kuna mwananchi mmoja anaitwa Ussi Ali Pandu ambaye amezungumzwa hapa. Ripoti yetu kama ukiangalia ilimzungumzia huyu na alikuja kwenye Kamati kutoa taarifa yake juu ya utaratibu wa ujenzi wa maduka 16. Kulikuwa kumetangazwa *tender* ya ujenzi wa maduka 16 pale Darajani kwenye soko la mbogamboga. Wakati huo Mkurugenzi alikuwa ndugu Mabrouk Jabu, kwa bahati nzuri huyu ndugu Ussi alibarikiwa kuifanya ile kazi na akafunga mkataba na Manispaa, lakini kwa ghafla yule ndugu Mabrouk akaja akaondoshwa, kabla ya kukabidhiwa lile eneo kwa

ajili ya kuanza kulifanyia kazi, akahamishwa ndugu Mabrouk ndio akaja ndugu Rashid pale kushika Manispaa.

Lakini mikataba yote tuliiyona na alianza kukata vibali kwa sababu moja kati ya masharti yao walikuwa wanatakiwa wakate vibali Mji Mkongwe, alikata vibali mbali mbali huku akisubiri kupewa lile eneo kwa ajili ya kuliendeleza. Lakini alipokuja ndugu Rashid matokeo yake ule mkataba ulibadilishwa na akapewa mtu mwengine. Alichoomba yeye kwa kuwa ile kazi hakupewa basi *at list* zile gharama zake alizoingia wakati ule wa kutaka kutekeleza mkataba ule basi arejeshewe mwenyewe zile pesa na hiyo ilikuwa imeonekana dhahiri.

Mhe. Spika, huku ukizingatia kwamba hata Sheria Nam. 3 ya mwaka 1993 inamtaka Mkurugenzi kwa mujibu wa ibara ya 51 Kifungu cha (C), sasa awe anaifuata mikataba iliyotangulia. Lakini mwenzetu alishindwa kuifatilia ile mikataba kwa sababu ile ni halali na inatakiwa ifuatwe. Matokeo yake baada ya kuingia yeye akaufuta ule mkataba akauwacha na akaendeleza mkataba mwengine. Jambo ambalo lilisababisha hasara kwa huyu mwananchi ambaye aliyekuwa keshabarikiwa kufanya shughuli zile.

Ukiangalia ripoti yetu hii inasema kwamba mwananchi yule sasa *at list* apewe gharama zake na kutokana na soko kwa sababu ni muda mrefu aliopewa. Lakini serikali imezungumzia huyu mtu aende Mahkamani kudai haki yake kwa sababu Manispaa ina haki ya kushtaki na kushtakiwa. Kwa kweli uamuzi huu mimi siuoni kama ni wa busara.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba kuna haja ya kubadilisha maamuzi ili kuona watu wa aina hii, na wako wengine, baadhi yao wametajwa humu. Basi wawe wanarejeshewa haki zao ili waondoshe yale manung'uniko waliyokuwa nayo na huo ndio utawala bora. Pamoja na kwamba tunasema tuwapeleke Mahkamani lakini hawa ni wananchi wetu hawana uwezo wa kwenda Mahkamani. Kesi zinachukua muda mrefu. Kwa hivyo, hili linaweza likasababisha kukosa haki zao, kwa sababu hawa hawendi Mahkamani watakosa haki zao bure, jambo ambalo si la busara.

Mhe. Spika, Kamati yangu wakati wa utekelezaji wake mbali ya mambo ambayo iliyafanya, mapendekezo iliyoyatoa lakini ilitoa mapendekezo ya ujumla. Ukiangalia kwenye ripoti kuna mapendekezo ya Kamati teule kwa ujumla kuna mambo kama 13 humu tuliomba serikali iweze kuyatekeleza. Yapo ambayo yemezingatiwa, lakini yapo mengine ambayo hayakupata majibu. Kwa mfano kuna eneo moja hili, pendekezo la 12

lilizungumzia juu ya Sheria hii iliyopo kuwa na mapungufu. Katika sheria ile kifungu cha 3(1) kinazungumzia kuwepo kwa *first schedule* ambayo ilikuwa katika sheria ile inazungumzia mipaka ya Manispaa kwa mujibu wa sheria hii ya Nam. 3 ya mwaka 1995.

Mipaka ya Manispaa ipo ya aina nyingi; kuna mipaka ya Kiserikali, na kuna mipaka mengineyo. Lakini mipaka inayozungumziwa hapa ni mipaka ile ya Minispaa kwa mujibu wa sheria Nam. 3 ya mwaka 1995 ambayo *first schedule* hiyo tokea imeanzishwa sheria ile hakuna tokea imeanzishwa sheria ile hakuna, tokea sisi tupo pale tumelizungumzia hili kwa maana hiyo hakuna mipaka ya Manispaa kwa mujibu wa sheria hii. Jambo ambalo kwa kweli kisheria sisi si wanasheria lakini tunaona ni kasoro moja kubwa sana. Sasa hili lilikuwa linahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka na kama tunasubiri sheria nyengine mpya inayokuja basi sheria hiyo nayo ije kwa haraka kwa sababu hii ni kasoro kubwa sana kisheria. Na kama Mawakili wetu wanasheria wetu wa sasa wataizungumzia, hili basi pengine inaweza ikatuletea matatizo katika utekelezaji wa sheria hii. Kwa hivyo, hili naona halikuzingatiwa.

Lakini kuna eneo moja ni pendekezo la 12, kuhusu watendaji wa Mamlaka ya Hifadhi ya Uendeshaji wa Mjimkongwe wanapotoa barua za taasisi waandike majina yao. Tuligundua hilo kwamba Mamlaka ya Hifadhi ya Mjimkongwe wakati ule wanapoandika barua zao wale waandishi hawaandiki majina yao hili nalo tumeliona kwamba ni kasoro na tumependekeza kwamba lifanyiwe kazi ili yule anayesaini ile barua basi aandike na jina lake, utakuta wao wanaweka saini tu halafu hamna jina hata ukimfatilia inakuwa tabu. Tumepata tabu hata kuwatafuta wale walioweka saini katika vibali mbali mbali vile walivyokuwa wamevitoa. Na mapendekezo mengine halkadhalika yapo ambayo hayakuweza kutolewa ufafanuzi.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, sina maelezo mengi juu ya ripoti hii. Ripoti hii imeanza kutekelezwa mapema, maeneo mengi yameweza kutekelezwa tunashukuru lakini bado kuna haja ya kuendelea kuzingatia na baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi ili Baraza letu la Manispaa liweze kufanya kazi zake vizuri na lionekane kwamba linatoa matunda kwa ajili ya wananchi wa Manispaa hii. Na kama tunavyojua kwamba Manispaa ni kioo, kwa sababu hii ndio sura ya mji wanapokuja wageni wakiona hali si nzuri basi kwa kweli haileti sura nzuri. Kwa hivyo, tuwawezeshe wenzetu hawa waweze kufanya kazi zao vizuri, mji wetu uwe safi, michirizi hii na iliyopo kama tulivyozungumza asubuhi kwenye maswali isafishwe, maji yaweze kutiririka vizuri, mji wetu ulete haiba. Nadhani hayo ndio matarajio ya wananchi.

Kwa hivyo, baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi sina maelezo mengi kama nilivyotangulia kusema na kwa sababu tokea mwanzo nimeridhika namna ya hatua hizi zilivyoanza kuchukuliwa tokea mwanzo. Kwa hivyo, mimi naunga mkono hoja hii mia juu ya mia na katika yale maeneo ambayo yana kasoro basi yaweze kurekebishwa.

Mhe. Spika, mimi ninalotaka kusema namalizia la mwisho kwamba kinapokuwa kitu kizuri ninasema hiki kizuri, na mimi hiyo ndio *principle* yangu na kinapokuwa kitu hiki kibovu hakifai mimi nasema hiki kibovu hakifai siwezi kwenda kinyume na *principle* yangu. Kwa hivyo, nadhani kuna haja ya kuelewana katika hilo. Jambo likiwa linafaa tutasema linafaa na jambo likiwa halifai tutasema hili halifai. Kwa hivyo, nadhani wenzetu wafike pahala watuelewe hivyo. Na nia yetu ni kuona kwamba tunakwenda vizuri pande zetu zote mbili ili wananchi wetu wajenge imani. Na ni matarajio yetu kwamba tutakwenda vizuri katika siku za baadae ili wananchi wajenge imani na serikali hii ya Chama cha Mapinduzi na chaguzi zinazokuja za 2015 na 2020 Chama cha Mapinduzi kiweze kushinda zaidi kwa kishindo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia ripoti hii. Pili, natoa shukurani kwa serikali kwa kuwa makini katika kufatilia, kuchambua na kujibu hoja za Baraza la Wawakilishi. Tatu, napenda kuwapa pole viongozi na watendaji wa Baraza la Wawakilishi kwa kupita katika kipindi kigumu cha misukosuko mbali mbali. Na nne natoa pongezi kwa Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kwa ufafanuzi mbali mbali wa hoja ambazo zimetolewa katika ripoti hii.

Mhe. Spika, mimi nitachangia katika ukurasa wa kwanza kifungu cha 1(2) ambapo katika mapendekezo ya Kamati Teule imesema, kama ingawa Baraza la Manispaa ni taasisi inayojitegemea *Board of Corporate* kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha sheria ya Baraza la Manispaa, bado serikali kwa kupitia Waziri mwenye dhamana ya Baraza la Manispaa ihakikishe kuwa taasisi zake zinatekeleza majukumu waliopewa kwa misingi ya sheria na kanuni za nchi.

Mhe.Spika, ninavyofahamu Baraza la Manispaa lisingefaa kuwa na *Board of Corporate,* kwani hii maana yake ni Shirika au Mamlaka ambazo zimeanzishwa kwa mujibu wa sheria ya mitaji ya umma. Na Baraza la Manispaa limeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Nchi ikiwemo Wizara ya Tawala za Mikoa, ambapo Tawala za Mikoa zimo katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Shehia pamoja na serikali za mitaa yenyewe ambao zimo Halmashauri, Manispaa yenyewe na Baraza la Mji. Sheria ya Mitaji ya Umma Mhe. Spika, ilipoanzishwa inaruhusu kuwa na Bodi za Wakurugenzi.

Hapa nilikuwa na ushauri tu Mhe. Spika, niishauri serikali au Wizara zinapoanzisha serikali za mitaa wakati wa kuja kupitia mageuzi ya serikali za mitaa iangalie kwa kina suala hili litakapotekelezwa, kwa kiasi fulani matatizo haya yaliyojitokeza ambayo ya kutofuatwa utaratibu wa manunuzi au kutofuatwa utaratibu wa mikataba yanaweza yakaondoka kabisa au kupungua.

Mhe. Spika, nitachangia katika ukurasa wa 1 kwenye kipengele kidogo cha 4 ambapo kinasema serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwa Madiwani na watendaji wa Baraza la Manispaa wanashirikiana ili kuleta tija iliyokusudiwa. Hapa Mhe. Spika, nilikuwa nina ushauri kwa sababu watendaji waachiwe wafanye kazi zao za utendaji na wanasiasa hapa nimekusudia Madiwani wafanye kazi zao za siasa za kutunga sheria, kutunga sera, kupitisha bajeti na pia kusimamia utekelezaji.

Nitatoa mfano kwa hivi sasa ninavyosikia Madiwani wanapewa pesa mikononi ili kutekeleza miradi ya maendeleo katika wadi zao. Utaratibu huo Mhe. Spika, sio rafiki katika kusimamia sheria ya fedha na manunuzi. Hapa nilikuwa nashauri Wizara ya Tawala za Mikoa, miradi yote inayotekelezwa katika ngazi za wadi ingewasilishwa katika serikali za mitaa ili kutekeleza miradi hiyo kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizokuwepo. Lengo hasa ni kuwasaidia wananchi kwa hivyo fedha zinazotolewa na serikali zifanye kazi ambayo imekusudiwa na tija iwe inapatikana kwa wananchi wote.

Mhe. Spika, ninakwenda kwenye kipengele cha 9(1) ambacho taarifa iliyotolewa na serikali inasema hivi, 'serikali imelifatilia kwa kina suala hili na kuona kwamba Baraza la Manispaa tayari limeanza kutekeleza sheria ya ununuzi na uuzaji wa mali za umma namba 9 ya 2005 na kuanzisha kitengo cha ununuzi yaani (PMU). Hapa Mhe. Spika, nilikuwa nina ushauri tu kwa serikali kuwepo labda na muundo wa *Tender Board* zao kwa mujibu wa sheria hii namba 9 ya 2005 ya Mitaji ya Umma na pia kuanzishwe *Tender Board* kwa mujibu wa kanuni ambazo zipo. Hii pia itasaidia kuondosha migongano au kutumia pesa za serikali ambazo ni kinyume na taratibu zilizowekwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia nafasi hii nikawa kichinja mimba wa uchangiaji katika ripoti hii ya Manispaa. Kwanza Mhe. Spika, ukitaka pepo au moto lazima ufe lakini kabla ya kufa kwanza la mwanzo uzaliwe, ukue, ulelewe halafu ujue jema na baya.

Sasa hii Manispaa hata sijui huyu bilisi wa moto kaingia wapi, sasa ninaomba twende kwa malaika wa pepo tuachane na bilisi wa moto. Mhe. Spika, ni imani yangu na nimpongeze sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Bazara la Mapinduzi kusikia kilio cha wananchi na kusikia kilio cha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kutokana na Uteuzi wa Mkurugenzi, nimpongeze sana. Lakini pia nichukuwe nafasi hii kwa Mheshimiwa Waziri ambaye ameteuliwa hivi juzi kushika madaraka katika Wizara hii ambayo ndani yake imo Manispaa.

Nimuombe Mhe. Waziri na ninavyomjua ni mwepesi kujifunza na pia ni mwepesi kufuatilia shughuli zake. Nimuombe Mhe. Waziri kwamba katika shughuli zake na ni shughuli ngumu ambazo walizopewa, ukiitizama Wizara hii ni ngumu.Kwa hivyo, nimuombe kwamba katika kufuatilia kwake basi ahakikishe anafuatilia kila pembe na kila sehemu asikubali kupewa maneno na watendaji wetu litamfikisha pahala pabaya.

Lakini pia niseme Mhe. Spika, nina imani sana na Mkurugenzi ambaye ameteuliwa kushika nafasi ya Manispaa nimuombe Mkurugenzi ripoti hii awe nayo na asome mambo yaliyomo humu asije akafanya madhambi ambayo yamefanywa kipindi kilichopita. Lakini si Mkurugenzi peke yake Mhe. Spika, lazima ashirikiane na Mstahiki Meya, lazima ashirikiane na Madiwani kwa sababu hawa ndio timu ya kuweza kufanya kazi ili kuhakikisha Manispaa sasa inapata ufumbuzi wa mageuzi ya hali ya juu kabisa.

Mhe. Spika, Mwenyekiti wangu amezungumza mengi, Mhe. Ismail Jussa Ladhu amezungumza mengi kwa sababu na mimi ni miongoni ambaye nilikuwa mwana Kamati Teule, sasa na mimi niombe baadhi ya mambo ambayo serikali katika haya mengi ambayo wametueleza nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba hakuna kitu muhimu kama umoja. Mkurugenzi akishirikiana na Mstahiki Meya, akashirikiana na Madiwani wake basi hakuna matatizo yoyote yatakayojitokeza Manispaa. Wenzangu wamezungumza hapa ni kutokuwa na mashirikiano ya pamoja maana Mstahiki Meya alijiona yeye kwa upande wake ana uwezo, na Mkurugenzi aliyepita kwa upande wake ana uwezo na alikuwa hafati taratibu na sheria ambazo wao wenyewe wamezipitisha.

Kwa hivyo, niombe sana katika vichwa vitatu hivi baina ya Mkurugenzi, Mstahiki Meya na Madiwani basi kitu muhimu ni kutumia vikao. Vikao vyao ndio vinastahili kuelekeza mambo yote ya Manispaa. Lakini yasije yakaonekana tena yakaenda vile *shaghla baghla*. Maana kulikuwa Manispaa na mimi naisema kama alivyosema Mwenyekiti wangu na wenzagu wengine hapo wamesema ilikuwa kama Kampuni ya mtu binafsi. Ilikuwa

completely wewe kila unapokwenda hakuna mahesabu, pesa zinakusanywa hazijulikani zinapokwenda, hakuna chochote ambacho utapewa kitu hichi, hakuna mikataba hakuna chochote.

Sasa ninayazungumza haya Mhe. Waziri ananisikia na wengine wananisikia walioko juu tunaomba tumsaidie Rais kwa sababu ameteua Mkurugenzi, ana imani naye na amemteua Waziri kwamba hii Wizara sasa itafanya kazi zake ipasavyo. Niseme kwamba Mhe. Spika, na mimi niunge mkono wale wote ambao wamedhulumiwa katika uongozi uliopita ninaiomba sana serikali ndio nikasema kwamba tuondoke kwenye bilisi wa moto twende kwenye malaika wa pepo. Ninaomba sana Waziri aliyeteuliwa hivi karibuni afatilie ripoti hii akae na Mkurugenzi pamoja na Mstahiki Meya na Madiwani wahakikishe wanaipitia tena ripoti hii yale matakwa ambayo tumeyaainisha humu katika Kamati Teule basi yafanyiwe kazi.

Ni imani yangu Mhe. Spika, kwamba kama tulivyoelekezwa jana hapa kwamba lazima tutumie taratibu, sheria, tuangalie Katiba inasemaje basi na hili tuchukuwe hatua kama tulivyoelekezwa jana hapa. Si vyema wananchi wetu wakadhulumiwa kiasi ambacho kwa kweli wakatokwa na imani. Niseme kwamba Mwenyekiti wangu amesema hapa na mimi narudia kusema lile ambalo ninahisi hili lina maslahi na wananchi la ukweli nitalizungumza, lile ambalo ninahisi hili bado wananchi wana malalamiko wakubwa basi sitochelea kuwatetea wananchi wale. Mimi niseme kwamba nimeingiwa na imani na ripoti hii ya Manispaa kwa sababu imetuelekeza vizuri, niseme kwamba ninaiunga mkono mia juu ya mia na niseme kwamba *wallahi* tuna imani sana na serikali yetu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kama serikali yetu itawajibika kama hivi basi tutakwenda sambamba na mihimili huu na serikali yetu, ili yale ambayo tunatoa maelekezo yawe yanachukuliwa hatua, hatuna matatizo. Yale yanayothibitika haya kwa kweli tufate taratibu na sheria na mimi niko pamoja na serikali, lazima tufate taratibu na sheria. Kwa sababu mimi ndio mtunga sheria siwezi nikakiuka sheria wala kanuni, wala katiba ya nchi ambayo tunaitunga sisi wenyewe. Pale ambapo panaharibika tuelezwe. Mimi nitoe mfano Mheshimiwa kama hatukupinga ripoti ya jana, tukatia mikiki kwamba hatuipitishi na tulikuwa hatuipitishi kweli lakini serikali kuna haja ya kuwaelimisha wenzetu kwa sababu sisi tunatetea wananchi. Na wananchi wamesikia malalamiko yote tuliyoyatoa kwa serikali yao lakini niishukuru sana serikali kwamba ilitoa ufafanuzi mzuri na

wananchi wetu wamesikia ufafanuzi wa serikali yao. Sasa kama tutakwenda namna hii *wallahi* mihimili mitatu hii itakuwa haina matatizo tutashirikiana na tutakwenda sambamba ili kuhakikisha taifa hili halinyimi haki ya binaadamu yoyote katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.Baada ya kusema hayo nirejee tena niseme naunga mkono hoja mia kwa mia lakini nimuombe Waziri aifanyie kazi ipasavyo. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia asubuhi ya leo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuliotumwa na wananchi wetu kuja kuwatumikia mambo yao kutupa uzima na kufika hapa na tukaanza kutekeleza wajibu wetu. Pili, nikupongeze Mheshimiwa na mimi kuniona kuwa mchangiaji wa sita katika ripoti hii ya taarifa ya serikali juu ya hoja zilizotolewa na Kamati Teule juu ya Baraza lako Tukufu na namna serikali tulivyokaa hasa baada ripoti hii kucheza kibatawata kwa muda na hatimae jana Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aliiwasilisha na hatimae leo waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili tumepata nafasi ya kuichangia.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kwanza niwashukuru wale wote ambao wametoa maoni yao juu ya ripoti hii na wale wote waliobahatika Mheshimiwa wameiunga mkono hoja hii ya serikali iliyoletwa mbele yetu na ni imani yangu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dokta Ali Mohammed Shein, tutaendelea kusimamia na kutekeleza yale ambayo tunaamriwa na kushauriwa na Baraza lako Tukufu tukiwa tunafanya kazi ya kuwatumikia wananchi.

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Spika, niende katika hoja ambazo zimetolewa. Nakubaliana na hoja ambayo imetolewa kwamba mawaziri tuwajibike kwa maana ya kuwatumikia wananchi kwa sababu mwisho sisi mawaziri ndio tunaounda serikali na serikali huchaguliwa kila baada ya miaka 5, na miaka 5 hii tupo mawaziri ambao tumebahatika kukaa huku mbele na hatimae nakubalianana na msemaji kukaa kwetu mbele si kwa sababu ya kutia mbwembwe tunachotakiwa tufanye kazi. Na ni kweli uajibikaji unatakiwa uonekane na uutekeleze wakati ule ambapo una nafasi.Uajibikaji sio unakuja kuusema baada ya wewe kutoka ndani ya uongozi.

Kwa hivyo, sisi Mawaziri nadhani tunalijua hilo na tutasikiliza sana na tutafuata ushauri wa Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi, kwamba sasa hivi wakati tukiwa kwenye nafasi hizi za Uwaziri ndio tunatakiwa tuwajibike na sio mwaka 2015, baada ya serikali itakayoundwa ikiwa Haji Omar Kheri hakubahatika kuwa Waziri sasa uanze kusema makosa ambayo yamefanywa katika kipindi hiki kutoka 2010 mpaka 2015. Ni lazima

kama kuna mapungufu basi uyafuatilie wewe mwenyewe katika kipindi hiki na uyarekebishe na ukishindwa kuyafatilia ukiona mambo mazito basi uwajibike kwa kuachia ngazi na sio kusubiri mwaka 2015.

Mhe. Spika, tunakubaliana kwamba mikataba ya Baraza la Manispaa na wafanyabiashara na watu mbalimbali kama ilivyosemwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi haikuandikwa kwa umakini na hilo serikali tumelisema na ndio maana tukasema basi mikataba hii yote lazima ipitiwe upya chini ya ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa sababu inaonekana hata ilipotengenezwa hii mikataba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu haikuhusishwa kikamilifu.

Kwa hivyo, hilo tunalikubali na ndio maana tutafanya hivyo na atakapokuja Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atalieleza vizuri. Na tutafanya hivyo kwa sababu serikali tayari imeanza kutambua hilo jukumu la kuijengea uwezo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na katika kuijengea uwezo ni sambamba na kuweza kuipatia miundombinu, ndio maana serikali imeweza kujenga lile jengo pale la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, na kuwapatia wataalamu na halafu kwa mujibu wa sheria yake ile ambayo tumeitunga hapa wanasheria wa Mawizara watakuwa vile vile nao ni *state attorney* ambao watakuwa wanafanyakazi chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa maana hiyo, tunajua kwamba pale kwa Mwanasheria Mkuu upo upungufu lakini wale wanasheria waliopo katika Taasisi za Serikali nao watakuwa wanafanya kazi chini ya muongozo na sheria ile ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Kuhusu sheria za Serikali za Mitaa na Sheria ya Baraza la Wawakilishi, wengi mmezungumza hapa ni kweli ni muda mrefu tumekuwa na *local government reform* na hivi sasa sera ya mageuzi ya Serikali za Mitaa tayari serikali imeshaitunga. Hivi sasa tunachofanya wizara ni kuichapisha katika vitabu ili tuweze kuisambaza kwa wahusika mbali mbali wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Hivi sasa vile vile tuko katika mchakato, tulikuwa tunadhani kwamba pengine Sheria ya Mageuzi ya Serikali za Mitaa, Sheria ya Baraza la Manispaa pamoja na sheria nyengine tungeweza kuzileta katika mkutano wa mwezi wa Januari.

Lakini hata hivyo, kutokana na ubiya wetu tutalazimika pengine kwenye kikao cha Mwezi wa Januari tuje tuusome Mswada kwa mara ya kwanza ili kikao kinachofuata cha mwezi wa Aprili tuje tuwasilishe sheria. Ikibidi tutamuomba Rais miswada hiyo ailete kwa hati ya dharura ikiwezekana kutokana na haja halisi ambayo ipo. Kwa hivyo, nakubaliana na Wajumbe ambao wamesema sheria imechukua muda mrefu na sisi kama

serikali nadhani tumekamata kijiti pale tulipoachiwa na wenzetu na hivi sasa tuko katika huo mchakato wa kuona kwamba hizo sheria tunaziandika na hasa Sheria ya Baraza la Manispaa.

Sheria ya Baraza la Manispaa inatakiwa iandikwe upya, kwa sababu hata muundo wenyewe wa Baraza la Manispaa unatakiwa ubadilike na sio ule uliopo sasa. Ule uliopo sasa tunahisi una matatizo na hauwezi ukatupa ufanisi katika kutekeleza shughuli mbali mbali za kuwatumikia wananchi ndani ya Baraza la Manispaa.

Pia, limezungumzwa suala la wafanyabiashara wanaotozwa ada ya usafirishaji mara mbili. Serikali tumesema waziwazi kwamba si halali kuwatoza wafanyabiashara ada mara mbili mbili. Kwa hiyo, atozwe ada mara moja ili asidhulumiwe kutozwa ada mara mbili ndivyo tulivyosema.

Jengine Mhe. Spika, Mheshimiwa aliyechangia suala hili pia amesema serikali iangalie tena namna ya uimarishaji wa masoko. Ni kweli mimi nilipotembelea masoko nimegundua kwamba ule utaratibu uliojengwa lile soko haukuwa sahihi. Kwa hivyo, hapo tutakapofanya marekebisho makubwa ya ujenzi wa masoko yetu nafikiri tutazingatia maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na mipango au taratibu zinazoendana kisasa na sio vile zilivyo. Kwa sababu ni kweli mimi nimejionea milango ya maduka na sikujionea *slab* kwa ajili ya kuuza tungule, kuuza nini. Kwa hiyo, ni kweli kuna makosa ambayo yamefanyika na ndio maana tukasema serikali kwamba haya ni makosa yalikuwa hayakupaswa kufanywa kama vile yalivyofanyika.

Manispaa ijitahidi kufanya kazi zake zaidi kuliko kutafuta mapato. Kwa kweli Manispaa tutajitahidi kufanya kazi zetu chini ya Mkurugenzi mahiri ambaye ameteuliwa hivi sasa, chini ya mashirikiano kati ya Mkurugenzi kwa maana ya ngazi ya utendaji na wanasiasa katika ngazi ya Mstahiki Meya na Madiwani. Tutazidisha mashirikiano ili utendaji uwe mzuri, lakini ili utendaji uwe mzuri tufanye yote mawili waheshimiwa Wajumbe, tufanye kazi zetu lakini vile vile tuimarishe ukusanyaji wa mapato, bila ya ukusanyaji wa mapato hatuwezi kufanya kazi kwa ufanisi mzuri zaidi.

Kwa hivyo, tutayazingatia yote mawili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kufanya kazi zetu kwa mujibu wa sheria na kanuni na kutekeleza ile kanuni ya uwajibikaji kwa watendaji na mimi nikiwa waziri naahidi kwenu kwamba nitalisimamia hilo kwa ujasiri, umahiri na busara kubwa ili mafanikio na ufanisi katika utendaji wa Baraza la Manispaa uweze kupatikana.

Kumezungumzwa suala la kodi ambazo Manispaa waliamua kuzitoza na ilihali wajibu huu ulikuwa wajibu wa *ZRB*. Mimi nataka kidogo nitoe ufafanuzi juu ya jambo hili, ni kweli Baraza la Wawakilishi lilipitisha sheria ya *proper tax* ambayo inasimamiwa chini ya *ZRB*. Kwa makubaliano kwa mujibu wa sheria ile kwamba ile kodi itakapoanza kukusanywa kuna asilimia fulani inatakiwa irejeshwe Baraza la Manispaa, lakini nini kinachofanyika? Na mimi naunga mkono lile suala la kuzifanyia marekebisho kanuni za Baraza la Manispaa (*by-law*) ambazo ndizo zinazotoa mamlaka kwa Baraza la Manispaa kukusanya ada ya *sanitary and light rate* katika kila nyumba ambayo imo ndani ya Mji Mkongwe. Kwa hivyo, hii ambayo wanaifanya ijapokuwa ada yenyewe haikusanywi ipasavyo na katika eneo hili ni moja kati ya mambo ambayo mimi toka nimeingia kuwa Waziri wa Wizara hii nimeliona kwamba lina mapungufu.

Kwa hiyo, hawakusanyi kodi ya majengo au ya ardhi hapana, wanachotakiwa Manispaa kukusanya ada ya *sanitary and light rate*, (ada ya usafishaji mji na uwashaji wa taa za njiani), tunaweza tukapata hoja taa zenyewe mbona hazipo. Sasa hayo ni mambo kati ya marekebisho ambayo lazima kama serikali tunatakiwa tuyaone na tuhakikishe kwamba Baraza la Manispaa wanayatekeleza hayo ili wao wakusanye ada yao kwa mujibu wa kanuni na sheria lakini vile vile watekeleze ule wajibu wao kama vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu alivyotushauri kwamba tutekeleze wajibu wetu. Sasa katika ukusanyaji wa ada, hii lazima yale ambayo yanapaswa kufanywa na Baraza la Manispaa kwa mfano kuweka taa, kusafisha mji. Maana ya kusafisha kwa maana ya kuzoa taka na kusafisha mitaro lazima wajibu huo tuweze kuutekeleza. Kwa hivyo, nakubaliana na ushauri wake na hilo tutalisimamia kwa kushirikiana na watendaji na Madiwani wa Baraza la Manispaa.

Jengine ambalo limejitokeza ni suala la serikali yenyewe kuwa iendelee kusimamia watendaji wake. Kama nilivyosema mwanzo wizara itajitahidi kufanya hilo kwa niaba ya serikali ili kuhakikisha kwamba kila mtendaji anasimamia vizuri au anawajibika vizuri katika kutekeleza majukumu yake ambayo amepangiwa.

Tunapokea pongezi za Mstahiki Meya ambazo zimetolewa na Mhe. Salmin Awadh Salmin pamoja na Mkurugenzi mpya. Na mimi nataka niseme kwamba toka tumeteuliwa tarehe 20 mwezi wa 8 mpaka leo ni karibu miezi miwili na siku kama mbili hivi tumekuwa tukishirikiana vizuri na Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa pamoja na wale watendaji ambao wapo hivi sasa, tunakwenda vizuri na ni imani yangu

pongezi hizi hazitawalevya. Pongezi hizi zitawapa ari ya kuweza kuzidisha mashirikiano na kutekeleza majukumu yao vizuri.

Limezungumzwa suala la sheria nambari 3 ya mwaka 1995 kwamba imepitwa na wakati. Ni kweli tunahitaji kuifanyia mapitio upya, Sheria ya Baraza la Manispaa na sheria hii kama nilivyosema tutaiandika upya na sheria tutakapoitunga basi tutaitunga ili iowane na kutokupingana na sheria nyengine za nchi hasa ile Sheria ya Fedha pamoja na Sheria ya Manunuzi na Ugavi ile ya nchi yetu. Tutafanya hivyo baada ya kufanya marekebisho au kuiandika upya Sheria ya Baraza la Manispaa.Kanuni nimeshasema kwamba zimepitwa na wakati nazo tutazifanyia marekebisho.

Mivutano kati ya watendaji na madiwani. Ni kweli kutokana na utendaji mbovu ambao ulionekana na Baraza hili inaonekana kweli kulikuwa na matokeo mabaya ya mvutano kati ya watendaji na wanasiasa ambao ni Madiwani. Na hili baada ya mimi kuingia nilijaribu kufanya vikao na madiwani, kufanya vikao na watendaji ili kuondosha mivutano hii isiyo na maana ili tuweze kuwatumikia wananchi. Kazi yetu sote ni kuwatumikia wananchi, tuliochaguliwa kazi yetu ni kuwatumikia wananchi na wale walioajiriwa kazi yao ni kuwatumikia wananchi kwa kufuata sera na taratibu ambazo serikali iliyopo madarakani imetoa maelekezo ya kiutendaji.

Kwa hivyo, hatuna nafasi ya kugombana na wale ambao watakuwa bado wanataka kuendeleza tabia za kugombana basi nadhani watuachie chombo chetu watafute safari waende wakalime mashamba yao huko, lakini sisi watuachie kazi zetu tuwatumikie wananchi.

Mkurugenzi kutokufuata mikataba ya nyuma. Ni kweli hilo serikali tuliliona na ndio maana serikali ikapata hoja ya nguvu ya kusema kwamba sasa hii mikataba yote tuna haja tuipitie upya na tuione utekelezaji wake ile iliyokuwa haina maana tuachane nayo na ile ambayo inatuwajibikia sisi kama Baraza la Manispaa kuendelea kushirikiana na wale ambao tumekubaliana nao bila ya kumdhulumu mtu. Ni vizuri tukaipitia upya ili serikali tusije tukafanya maamuzi halafu yakaja yakatugharimu, ndio maana tukasema mikataba hii lazima tuipitie upya.

Kuhusu mipaka ya Manispaa, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba serikali imeshaamua sasa hivi imetoa kazi kwa taasisi zinazohusika kupitia Idara ya Mipango Miji kuharakisha *master plan* ya mji wa Zanzibar ili kuijua mipaka halisi ya Baraza la Manispaa na hata kuondosha mzozo kati ya Baraza la Manispaa na Halmashauri nyengine ambazo imepakana nazo. Katika hili tunakwenda mbali zaidi, tunataka kujua

hivyo katika hali tuliyonayo sasa ni vigezo vipi ambavyo tunavyo tunaweza tukafikia badala ya kuwa na Baraza la Manispaa tukawa na jiji. Kwa hivyo, hayo ni mambo ambayo yanatizamwa kwa pamoja na kwa bahati nzuri katika *local government reform* mambo hayo yameelezwa vizuri sana. Kwa hivyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba hiyo kazi tunaifanya kwa kuelewa kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmin na yeye anaelewa vizuri kwa sababu alikuwa diwani katika Baraza hilo. Lakini vile vile na mimi naelewa vizuri kwa sababu mwaka 1979 mpaka 1984 nilikuwa mtumishi wa Baraza la Manispaa.

Pia, imezungumzwa kwamba Waziri mwenye dhamana ahakikishe Baraza la Manispaa linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba mimi Waziri mwenye dhamana Haji Omar Kheir basi nitafanya wajibu wangu kama ninavyotakiwa kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi hii. Na nitaifanya kazi hiyo kwa uadilifu, ujasiri na kwa umakini mkubwa sana ili nihakikishe kila mtendaji anatekeleza wajibu wake lakini sio mtendaji tu, hata mimi waziri nihakikishe natekeleza wajibu wangu ili kuepukana na yale ambayo ameyazungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Baada ya Rais kunitengua nisije tena nikasema, unajua kule Manispaa ilikuwa kuna hivi, hivi na hivi. Sasa kama hayo nayaona natakiwa niyachukulie hatua sasa kabla ya kesho.

Suala la kuzingatia sheria tutakapotunga sheria tuzingatie sheria nyengine. Nafikiri nishalisema na katika hili lazima tuzingatie sheria za nchi ili tusije tukagongana na Sheria zetu za Baraza la Manispaa, lakini tutazingatia zaidi Sheria ya Fedha na Sheria ya Manunuzi. Kwa sababu katika mambo mengi ambayo yamezungumzwa na Baraza la Wawakilishi kupitia Kamati Teule ilikuwa zaidi ni uvunjaji wa Sheria ile ya Fedha pamoja na Sheria za Manunuzi na Ugavi ya Zanzibar. Kwa hiyo, hilo tutalizingatia sana.Madiwani na watendaji wafanye kazi zao. Nakubaliana na hili na kama nilivyosema tumeshaanza kulizungumzia.

Kuhusu suala la *Tender Board*, sisi hili tulilijadili serikalini tukaona kwamba katika sheria ile ya *tender board* kuna *schedule I* na *schedule II*. Baraza la Manispaa halina Wajumbe wa Bodi lakini lina Madiwani, Madiwani ni wanasiasa ndio maana serikali ikaamua kwamba tutumie ile *schedule II* ambayo inampa uwezo Katibu Mkuu kuweza kuagiza suala la kuwepo kwa *Tender Board* katika taasisi inayojitegemea kama Baraza la Manispaa iunde *Tender Board* kupitia wakuu wake wa idara ambao wako hivi sasa. Kwa hiyo, hilo serikali imeliamua kupitia hiyo sheria na kupitia hizo *Schedules* ambazo nimezitaja.

Mchangiaji wa mwisho kwa leo alikuwepo Mhe. Asha Bakari Makame, ‘iso kongwe haivushi’. Nataka nimshukuru sana Mhe. Asha Bakari Makame kwa ushauri wake ambao ametupa, nataka nimhakikishie kwamba ushauri wake yeye na ushauri wa Waheshimiwa wengine Wajumbe wa Baraza hili tukufu tunaupokea na tutahakikisha kwamba tunaufanyia kazi ili kuondosha *gape* kati ya mihimili hii miwili, kati ya muhimili wa kutunga sheria na muhimili wa utendaji. Tutapokea ushauri huo kama tulivyoupokea ushauri wa Kamati Teule ya Baraza, yale ambayo wao wametushauri na wanahisi kama serikali hatujayaweka vizuri hususan lile suala la kufikiriwa wale watu ambao haki zao kama zinaonekana zimepotea. Hili nataka niwahakikishie kwamba serikali tunalichukua tutalizingatia na hakuna mtu atakayekosa haki yake.

Vile vile, amenihimiza nihakikishe kufuatilia majukumu ya taasisi zilizochini yangu, nitafanya hivyo Mheshimiwa. Mkurugenzi aisome ripoti nadhani anayo na kazi nzuri ambayo ameifanya toka ameteuliwa ripoti hii imemsaidia sana katika kujua ukweli wa mambo wa pale Baraza la Manispaa, kumjua huyu yukoje na yule yukoje. Kwa hiyo, nadhani Mkurugenzi wangu amesikia pale na ndio maana toka ameteuliwa kichwa chake kimeanza kubadilika rangi, nina wasi wasi mpaka ikifika Disemba kichwa cha Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kitakaribiana na cha Mhe. Spika, pale, amekuta mambo mengi na hiyo inatokana na kwa sababu ya kufikiri sana mtizameni Mhe. Spika pale, anafikiri sana namna ya sisi tunavyotoa maoni na kuchangia anatakiwa afikiri haraka sana ndio maana kichwa cha juu cha Mhe. Spika kimebadilika. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hivyo, na Mkurugenzi wangu nadhani ikifika Disemba kitakuwa kama cha Mhe. Spika. Niliogopa Mhe. Spika, nisijenikaulizwa kama alivyoulizwa mtu mmoja siku moja. Kwa hivyo, ndio maana nilisema nitoe ufafanuzi wa kichwa kipi kwa hiyo ni kichwa cha juu. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, mashirikiano na madiwani nishasema kama walivyosema Waheshimiwa tutazingatia na tutajaribu kuendeleza na kuwaweka karibu watendaji na Waheshimiwa Madiwani kama walivyoshauri Waheshimiwa wote waliochangia.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe ambao wametoa maoni yao na mimi naiunga mkono kwa asilimia mia moja Ripoti hii ya serikali juu ya Hoja ya Baraza la Manispaa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nimshukuru sana Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kunirahisishia kazi Mhe. Spika. Aidha Mhe. Spika, niwashukuru sana tena ndani ya dhati ya moyo wangu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa namna walivyochangia taarifa hii kwa umakini na undugu na kwa nia ya kurekebisha yale mapungufu ili kujenga msingi wa kuwahudumia wananchi. Narudia Mhe. Spika, kusema nimeridhia sana ndani ya moyo wangu na michango ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameitoa na lazima nilipongeze Baraza letu hili Mheshimiwa kwa namna linavyopevuka, linavyofanya kazi na linavyoonesha njia ili tufikie hatua kubwa zaidi ya maendeleo ya nchi yetu, na naamini wananchi watakuwa wanatusikia yote haya tunayoshughulika nayo kwa nia ya kuwahudumia.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa niwashukuru Waheshimiwa waliochangia katika taarifa hii. Nianze na:

1. Mhe. Ismail Jussa ladhu
2. Mhe. Panya Ali Abdalla
3. Mhe. Salmin Awadh Salmin
4. Mhe. Marina Joel Thomas
5. Mhe. Asha Bakari Makame na
6. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ

Mhe. Spika, kwanza nianze kupokea pongezi za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwa kuipongeza taarifa hii iliyoletwa na serikali ambayo chanzo chake inatokana na taarifa ya utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar. Kwa niaba ya serikali nazitoa pongezi hizo na shukurani na nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba nia na madhumuni ya serikali ni kuleta taarifa itakayoeleweka, itakayofahamika ili kuondoa mivutano kati yetu upande wa serikali na upande wa Wajumbe ili kila jambo linalokuja hapa liweze kufahamika zaidi, na pale ambapo panakuwa na mapungufu yaonekane mapungufu ya kibinadamu na turekebishe kwa pamoja ili kujenga hatma njema ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nianze na ushauri wa Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Kwanza napenda niupokee ushauri wake kuhusu suala la miswada inayohusiana na mchakato wa katiba hususan suala la kura ya maoni ama miswada mingine itayojitokeza inayohusiana na hayo ili ofisi yetu ya Makamu wa Pili wa Rais ifuatilie mapema kuona ni miswada gani inayokuja

tuweze kushirikiana na wenzetu kwa nia ya kuondoa mizozo na hasa kwa nia ya kujenga kauli moja ya Wazanzibari bila ya kuwepo na tofauti. Nalipokea sana shauri hilo.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwa kumpongeza Waziri, watendaji wake, Meya wetu wa Manispaa ya Zanzibar na Mkurugenzi mpya kwa kazi nzuri wanazozifanya za kuliimarisha Baraza la Manispaa. Pale penye kasoro Mheshimiwa lazima tuseme pana kasoro na pale ambapo panafanyika mema lazima wenzetu tuwape moyo ili wazidishe *speed* ya kufanya mazuri zaidi. Kwa kweli katika kipindi kifupi tumeona mabadiliko na hatua zimeanza kuchukuliwa na inaonesha wazi Mkurugenzi wetu aliyepo ni msikivu wa hali ya juu nampa hongera nyingi sana. Naamini yale yote yaliyolalamikiwa sasa Waheshimiwa Wajumbe si muda mrefu yataondoka na kutokana na maoni na mapendekezo yao yatazidi kujenga mafanikio mema.

Nia ya kamati hizi kama nilivyosema jana wanapofanya uchunguzi ni kuturekebisha ili tufanye vizuri na wajibu wetu ni kuonesha yale mabadiliko mema kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, hatua hizo tutazichukua.

Kuhusu suala la kujadili sana humu ndani tusionekane kwamba tuna kambi mbili au tunapotofautiana kwenye mawazo tukaanza kuchukiana na kujengeana hoja ambazo hazina msingi. Ni ukweli kabisa Mhe. Spika, tunapofanya kazi kwa pamoja sisi viongozi ndio mfano wa wananchi wetu na ndio dira ya mafanikio yetu. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa kwamba suala la kujigawa tukaonesha kuwa tuko kambi mbili haina msingi, suala la msingi ni kufanya kazi kwa pamoja, tupokee ushauri, tupokee mawazo, na suala zima la kuhakikisha kwamba tofauti ya mawazo ndio msingi wenyewe, ndio mafanikio yenyewe, ndio demokrasia. Tusiogope kupeana mawazo ya msingi ya maendeleo, mawazo ndio hoja zenyewe ukipewa wazo pokea kama una hoja zaidi jibu hilo suala lenyewe. Kwa hivyo, sote tukubaliane kwa upande wa serikali tupokee mawazo na Wawakilishi nao wapokee mawazo ndio tutapokwenda vizuri. Mimi nakubaliana kabisa na hoja hii.

Suala la uwajibikaji Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ amelieleza vizuri. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe jambo hili tutajitahidi kwa kila inavyowekezana mana kigezo chetu katika uongozi ni uwajibikaji na uadilifu, mapozi, mbwembwe hazisaidii chochote, zinasaidia nini katika kuwatumikia wananchi ukawa na mapozi na mbwembwe haisaidii chochote. Mimi nikubaliane kwamba wakati huu ambapo tunafanya kazi hasa tuliomo serikalini tuna maamuzi ya pamoja, jambo letu pamoja, huwezi kuwa serikalini ukalaumu wenzako ndani ya serikali,

imo ndani ya Serikali ya Zanzibar, imo ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, zote serikali tunafanya kazi za kutumikia wananchi, lazima hapa tujue kwamba serikali ikiwa kuna kosa ni kosa la wote ndani ya serikali na yakiwepo mafanikio ni mafaniko yote ndani ya serikali. Kwa hiyo, tupunguze jazba za kusimama kwenye majukwaa ya siasa tukigongana na kushutumiana wakati na wewe ni sehemu ya jambo hilo. Itakuwa ni vizuri tu kufanya kazi kwa pamoja na mashirikiano na tuwajibike na mimi naunga mkono suala hilo moja kwa moja.

Kuhusu uwezo wa polisi. Mhe. Spika, ni kweli jeshi letu linahitaji kuimarishwa zaidi na ndio nia ya serikali na ndio maana kukawa na hii sera ya maboresho ndani ya Jeshi la Polisi, tuna upungufu mkubwa. Lazima tukiri mapungufu hayo yapo hasa kwenye suala zima la *intelligence* na mambo ya kufanya uchunguzi ni wajibu wetu kwa pamoja kuona namna gani tatizo hili tunalitatua kwa kulisaidia Jeshi letu la Polisi lifanye kazi zake vizuri. Kwa sababu Mhe. Spika, ni kweli tumewapa mzigo mkubwa, yako mambo mengi sasa hivi polisi wanapaswa kuyashughulikia, tukayaona yote haya ambayo yamependekezwa na Baraza hili tukufu kwa kiasi kikubwa inahitaji *facilitation* ya Jeshi la Polisi, watakapochelewa wao kufanya wajibu wao watachelewesha mtiririko mzima.

Kwa hivyo, niseme kuwa ushauri naupokea na ndio nia ya kuimarisha Jeshi la Polisi tunaliona hilo na itabidi serikali kufanyakazi karibu na Jeshi la Polisi kuona namna gani tutahakikisha mambo haya yanafanyika kwa umakini uadilifu na kwa haki. Kwa sababu asitokea mtu hapo katikati akaharibu nia njema ambayo tayari serikali imeikubali na Wajumbe wa Baraza hili wameionesha.

Kuhusu kuimarisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ndio dhamira ya serikali. Tunajua kwamba uhitaji huo upo na tumeanza kwa kujenga miundo mbinu kama alivyosema Mhe. Waziri hapa kwa jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Lakini kuwa na *State Atony* katika mawizara na taasisi mbali mbali za serikali. Lakini pia kuongeza ajira ya wanasheria kwa msingi wa kufanyakazi hizi kwa wepesi zaidi kutokana na hali halisi ilivyo sasa ni kweli uzito mkubwa sana unamtegemea sana Mwanasheria Mkuu wetu hapa anafanyakazi nyingi huo ni ukweli na uhakika kabisa.

Kwa hivyo, kadiri tunavyojitahidi sasa na katika mpango wetu wa maboresho ya mishahara hii tumeweka eneo maalumu la kuwafurahisha wanasheria kwa msingi kwamba wafanyekazi katika Ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu na serikalini ili shughuli hizi ziweze kufanyika vizuri.

Kuchukua hatua kwa wakati ushauri tunaupokea kwa sababu kazi kubwa zinafanyika hizi za uchunguzi, kamati zetu za uchunguzi zinaafanyakazi hizi za kuleta taarifa hapa na tunapochelewa ni kweli wakati mwengine haki za mwengine zinapotea. Lakini hatuchelewi kwa kupenda tunachelewa kwa sababu ya kufanya tathmini, utafiti na kutafuta haki. Lakini tutajitahidi ili tuweze kuchukua hatua mapema iwezekanavyo kwa msingi wa kwamba haki itendeke zaidi. Kuhusu Sheria ya Serikali za Mitaa Mhe. Waziri anehusika ametoa ufafanuzi wa kutosha.

Kuhusu suala hili la wahusika kwenda Mahkamani kama ripoti ilivyoamua Mhe. Waziri amelitolea ufafanuzi na mimi nakubaliana nae kwamba tutafute utaratibu utakaowezesha kulimaliza hili tatizo. Kwa sababu ni kweli wako wananchi wetu hawa watashindwa kwenda Mahkamani kufatia jambo hili. Inabidi tukae zaidi tulifikirie namna ipi itaeka utaratibu ulio mzuri zaidi kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Spika, suala la soko libaki kama ni soko. Ni hoja ya msingi kabisa na ndio maana serikali tukasema kwa sasa kwa pale ambapo soko linafikiriwa kujengwa na wanaona upo umuhimu wa kuwa na maduka katika soko hilo. Basi katika hatua za awali ioneshe hii sehemu ya soko, hii sehemu ya maduka hii itafanyika shughuli hii na shughulii hii tokea mapema. Kwa hivyo, ushauri ndio serikali ndio ambao serikali unao na unaendelea kufanyiwa kazi.

Nakubaliana kwamba Manispaa iwe ni sehemu ya kutoa huduma sasa hivi kufanya kazi itoe huduma zilizo bora hiyo ndio nia ya serikali na ndio maboresho yataelekezwa sana katika Baraza la Manispaa ili liweze kutoa huduma zake vizuri liweze kukidhi haja na naamini litakapofanyakazi vizuri sote tutakuwa tumeridhika na shughuli hizo.

Kwa hiyo, tupeni nafasi Waheshimiwa Wajumbe kuifanyakazi hii naamini kuwa wizara husika imejipanga vizuri na Waziri nimemuona namna alivyojitayarisha katika kusaidia jambo hili na mimi nampongeza sana kwa hatua anazozichukuwa.

Kuundwa kwa Kamati Teule kusiwe sababu ya kukomoa wengine wanaotoa taarifa. Sio nia yetu kabisa kabisa kumkomoa anaetoa taarifa. Tungependa watu watupe taarifa lakini tunapenda vile vile watu wasitumie kivuli cha kutoa taarifa kwa kuziba maovu yao. Watoe taarifa watusaidie utekelezaji uwe mzuri. Lakini isiwe unaona umefanya kosa unahukumiwa kwa kosa lako, ukarukia sasa kwenda kutoa taarafa kusudi unatoa taarifa za mwengine zako hutaki kuzitoa. Kwa hivyo, tunapofichua la yule lazima na wewe tukushughulikie hatutaweza kukuachia.

Nakubaliana kwamba serikali kuwa makini na utendaji wake na tufanye kazi vizuri na tuheshimu yale ambayo maelekezo tunayoyapata.

Nakubaliana na ushauri wa Mhe. Salmin Awadh Salmin kuhusu mapungufu ya mapitio ya mipaka kwa Manispaa ya Zanzibar. Naamini kabisa kwamba jambo hili linalihitaji tulifanyie kazi ili tuhakikishe kwamba mipaka ya Manispaa yetu inajulikana vizuri na kwa sababu sasa hivi *Master Plan* ya mji iko *final stage* sina shaka yoyote tutakuwa na mipaka mizuri ya Manispaa ya Zanzibar.

Suala la Mapitio ya Sheria Mhe. Waziri ameshalieleza vizuri na hapana shaka yoyote taratibu na sheria na mambo mengine na hata kanuni zitabadilika ziendane na mahitaji ya sasa.Kuhusu Mikutano kati ya Meya na Mkurugenzi. Mimi sasa niwapongeze tu na Mhe. Waziri kaeleza vizuri nimpongeze sana Mstahiki Meya kwa *commitment* yake na Mkurugenzi mpya na namna wanavyofanya kazi pamoja. Inatupa moyo sote inatupa moyo sote tuwatakie kheri mambo haya yaende vizuri zaidi.

Kuhusu vibali na barua ziwe na majina ya wahusika zinapotolewa. Ushauri mzuri huwezi kukaa tu ofisini, huko ofisini ukaandika barua na ukatia saini tu jina lako haliko. Tukujue wewe ulietia saini nani na cheo chako, huo ndio utaratibu sahihi na barua zitakazokuwa na saini tu ambazo hazina jina na nafasi ya muhusika barua hiyo iwe basi tena.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo niupokee sana ushauri wa dadaangu Mhe. Asha Bakari Makame ameeleza suala zima la kufanyakazi kwa pamoja na mimi nimwambie na niwaambie Wajumbe wote kwamba serikali tunaipokea kabisa kwa mikomo miwili suala la kufanyakazi kwa pamoja. Tunaamini ushirikiano ndio mafanikio, umoja ndio silaha kubwa ya Wanzanzibari wote sio tu hapa katika Baraza hili. Tutakapokuwa wamoja wananchi wote wa Zanzibar kila jambo gumu mnaloliona leo linakuwa rahisi na mafanikio yanapatikana.

Kwa hivyo, suala la kuwa pamoja tukajenga nchi yetu kwa maendeleo ya watu wetu ni suala la msingi tunakubaliana nalo na Mhe. Spika, mimi kwa kweli kabisa kabisa niseme wazi michango inayotolewa na inayoendelea kutolewa na Wajumbe wa Baraza letu hili tukufu inatupa faraja kubwa sisi ndani ya serikali ya kuifanyiakazi na hoja zisitutafautishe. Hoja iwe ni kigezo cha kushindanisha kila mmoja aje na hoja ya msingi kwa ajili ya maendeleo ya Wazanzibar.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Mhe. Waziri nakushukuru na nashukuru kwa majumuisho hayo ambayo yanamalizia shughuli yetu hii.

Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaoikubali na kuipokea Taarifa hii ya Utekelezaji wa Manispaa wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Nadhani muda uliopo sijui kama unatosha kumaliza kazi hiyo. Tuna jambo dogo sijui kama Mawaziri mmejipanga tayari sawa. Tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia masuala ya

Ukimwi Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu wanaoishi

au Walioathirika na Virusi vya Ukimwi.

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko (Kny) Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa heshima yako naomba kusoma kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia masuala ya Ukimwi Zanzibar Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu wanaoishi au Walioathirika na Virusi vya Ukimwi na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.(*Makofi*).

Mswada wa Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mswada wa Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza. Naomba kuwasilisha.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Sasa Waheshimiwa naomba nimalizie kwa kumkaribisha Mhe. Waziri wa Miundo Mbinu na Mawasiliano.

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Amri ya Barabara Sura 134

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Naibu waziri wa Miundombinu na Mawasiliano (Kny) Mhe. Waziri wa Miundomnibu na Mawasiliano: Naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Amri ya Barabara Sura 134 na Mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Mswada huo pia umewasilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza.

Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukuwe nafasi kuwashukuru kwa kumaliza shughuli za mkutano huu vizuri na kwa punde tu hii kuwasilisha ile Miswada ambayo imesomwa kwa mara ya kwanza.

Shughuli ya ufungaji rasmi ya mkutano huu itafanyika hapo jioni.

Kuna matangazo mawili yanayoshughulikia na masuala ya michezo.

Tangazo la kwanza ni kwamba kwa ajili ya kusheherekea kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi yetu Matukufu wa Zanzibar ya tarehe 12 Januari mwaka 1964 kuna maandalizi ya Timu au mechi mbili za michezo ambazo timu yetu makini ya Baraza la Wawakilishi itacheza na timu ambayo tuna uhakika wa kushinda ya Bunge la Jamuhuri la Muungano wa Tanzania siku ya tarehe 10/01/2014.

Lakini mechi ya pili ya timu yetu hiyo hiyo ambayo napo tutashinda kwa kishindo ni mechi itakayochezwa kati ya timu yetu na timu ya Bunge la Jamuhuri ya Uganda. Mchezo huo utafanyika siku ya tarehe 13/01/2014 na michezo yote miwili hiyo itafanyika katika Uwanja wa Amani.

Tangazo la Pili: Waheshimiwa Wajumbe naomba kutoa tangazo rasmi juu ya mafanikio mazuri ya timu yetu makini ambayo imeshinda katika ligi ya kombe la Mabenki na kuchukuwa kombe. Bahati nzuri wakati tunashinda mchezo huu mimi nilikuwa nchini China. Bahati nzuri na Mtendaji wa *People's Bank* naye pia alikuwa huko huko nikampigia simu nikamwambia kuwa nimekushinda.

Kwa hiyo, leo hii kutakuwa na sherehe rasmi ya kusherehekea ushindi huo. Lakini kabla ya kwenda kwenye sherehe hiyo ambayo itafanyika pale *Cafeteria,* leo chakula hapa hapa. Mara baada ya kuondoka humu ndani tutakusanyika hapo *Cafeteria* ili tuendelee kusheherekea ushindi wetu huo.

Naomba hilo kombe liletwe lile kule. Basi Waheshimiwa Wajumbe hiyo ndio kazi nzuri ya timu yetu makani ya Baraza la Wawakilishi. Kombe hili ni kwa ajili ya mpira wa miguu. Lakini naamini siku moja tutaletewa na kombe jengine la mpira wa mikono. Mhe. Naibu pale ananiahidi kwamba kombe hilo litaletwa hapa siku moja.

Basi Waheshimiwa Wajumbe tunahimizwa sote tujumuike pale *Cafeteria* ili kupata chakula cha mchana ambacho ni mfululizo wa sherehe za ushindi huu ambao tumeupata kutokana na mchezo mzuri tulioshinda katika ligi kuu hiyo ya Mabenki baada ya kucheza fainali na *People's Bank of Zanzibar*.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe sasa naakhirisha kikao hicho hadi saa 11:00 jioni. (*Makofi*).

(Saa 6:50 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni leo).

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili kutufungia mkutano wetu huu wa 13, naomba nitoe maneno mawili matatu.

Kwanza kukushukuruni nyinyi Waheshimiwa Wajumbe kwa kujenga mashirikiano makubwa ya kufanya shughuli zetu kwa niaba ya wananchi wetu. Mashirikiano tuliyonayo ndio yanayohitajika sana kwa ajili ya kuwashughulikia wananchi wetu, lakini vile vile katika kutimiza wajibu wetu wa shughuli zetu sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote pamoja na Wajumbe wote wa *back benchers* kwa kazi nzuri ambayo muliyoifanya kiasi kwamba leo Katibu anatueleza kwamba shughuli ambazo zimepangwa kwa mkutano huu zote zimemalizika tena kwa wakati muafaka.

Nichukue nafasi hii vile vile kuwashukuru watendaji wetu wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri ya kuwahudumia Wajumbe, lakini pia kwa mashirikiano yao ili kufanya shughuli zetu zifanikiwe vyema. Bila ya utendaji wao bora, basi shughuli zetu zisingekuwa nyepesi kuzifanikisha kama vile ambavyo tumezifanikisha.

Lakini kama kawaida taarifa za shughuli zetu haziwezi kuwafika wananchi wetu bila ya kupata msaada mkubwa sana kwa ndugu zetu hawa ambao wanaochukua taarifa zote na kuonekana moja kwa moja kwa wananchi wetu. Kazi yao imekuwa ni kubwa na ni muhimu kwa sababu wananchi wamekuwa wanafuatilia kwa karibu sana namna Wawakilishi wao wanavyofanya kazi kwa ajili yao.

Pia, niwashukuru wote wapiga picha ambao nao wamekuwa wakishirikiana pamoja na sisi, bila ya kuwasahau wale ambao wanatoa tafsiri kwa wale watu wasiosikia na mabubu ambao kutokana na tafsiri zao kwa kutumia ishara na alama, basi wanapata kujua wananchi wanafanya nini au wanafanyiwa nini na Wawakilishi wao.

Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru watendaji wa serikali ambao nao wamekuwa karibu na Mawaziri wao ili kuona shughuli za mkutano huu wa 13 zinakwenda vizuri.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe na kwa kuwa hatuna shughuli nyengine kwa wakati huu. Sasa nichukue nafasi hii kwa heshima kubwa kumuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aje kutoa maelezo yake na hatimaye tumalize shughuli zetu kama zilivyopangwa.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais karibu. (*Makofi*).

KUAHIRISHA BARAZA

UTANGULIZI:

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika**,** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Mkutano huu wa kumi na tatu wa Baraza la Wawakilishi.

Aidha, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu pamoja na wananchi wote kwa dua zenu zilizonifanya niweze kukamilisha ibada yangu za Hijja kwa salama. Allah akujaalieni kila la kheri na awajaalie Pepo yake Tukufu, Amin.(*Makofi*).

Mhe. Spika, shukurani za dhati nazitoa kwako wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti na wasaidizi wako wote kwa kuendelea kuliendesha Baraza hili Tukufu kwa umahiri mkubwa na demokrasia ya kupigiwa mfano. Waheshimiwa Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbali mbali wamejitahidi kutumia hekima na busara zao walizojaaliwa na Mwenyezi Mungu katika kufanya kazi zao ambazo zimechangia kuongeza kasi ya maendeleo ya Taifa letu.

Mhe. Spika, mashirikiano makubwa yaliopo kati ya Baraza la Wawakilishi na Serikali yamepelekea kuleta ufanisi mkubwa na ongezeko la ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Natumia fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa hekima na busara zake katika kuiongoza nchi yetu. Pia, ninampongeza sana Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa kumshauri na kumsaidia ipasavyo Mhe. Rais. Tunazidi kuwaombea viongozi wetu hawa, Allah awazidishie hekima na busara ya kuiongoza nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sana, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kufanyakazi kwa bidii na ufanisi na kuleta tija. Naomba Viongozi wetu hao pamoja na watendaji waongeze bidii na umakini katika utendaji wa kazi zao na kuepuka kufanya kazi kwa mazoea, ili tija zaidi iweze kupatikana na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa aina yake ninavipongeza na kuvishukuru vyombo vya habari vyote hapa Zanzibar, hasa Shirika la Habari la Zanzibar (*ZBC*) kupitia redio na TV pamoja na *Cable TV* ambavyo vilirusha moja kwa moja mtiririko mzima wa shughuli za Baraza na kuwawezesha wananchi wetu kufuatilia kwa makini matukio yote yaliyojiri Barazani. Pia, nawapongeza wakalimani wetu wa lugha ya alama kwa kazi nzuri walioifanya ya kutafsiri mawasilisho na mijadala katika kipindi chote cha Baraza na kuwawezesha wananchi wenzetu wenye matatizo ya kusikia kufuatilia shughuli zote za Baraza namna zilivyokuwa zinakwenda ndani ya ukumbi huu. (*Makofi*).

Mhe. Spika**,** kama sote tunavyoelewa nchi yetu imo katika hatua muhimu ya kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo Rasimu ya Mwanzo ilizinduliwa tarehe 3 Juni, 2013. Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na makundi maalum tayari yameshaijadili Rasimu hiyo na kutoa maoni yao. Kazi hiyo ilifanyika kwa mashirikiano na mafanikio makubwa. Nachukua fursa hii, kuipongeza Tume ya Marekebisho ya Katiba, Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla kwa kufanikisha kazi hii muhimu.

Mhe. Spika**,** hatua inayoendelea hivi sasa ni kwa Tume ya Marekebisho ya Katiba kuandaa Rasimu ya Pili ya Katiba ambayo itapelekwa katika Bunge la Katiba kujadiliwa na hatimaye kupatikana kwa Rasimu ya Tatu ambayo wananchi watapata fursa ya kupigia

kura ya maoni kwa ajili ya kukamilisha mchakato huu. Nawasihi wananchi wenzangu kuendelea kuwa watulivu ili mchakato huu umalizike salama na Katiba Mpya kupatikana.

Mhe. Spika**,** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaendelea na kazi ya uandikishaji wa wapiga kura na uendelezaji wa Daftari la kudumu la wapiga kura. Kwa awamu ya mwanzo, kazi hii imekamilika kwa Majimbo 32 ya Wilaya sita (6) za Unguja na Majimbo 6 ya Wilaya nne (4) za Pemba. Kwa hivi sasa, Tume inaendelea na kazi hiyo kwa Pemba na inatarajia kukamilisha kazi hii siku ya tarehe 4 Novemba, 2013.

Mhe. Spika**,** napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wananchi wa Majimbo 12 yaliyobakia kwa Wilaya ya Wete, Chake Chake na Mkoani kujitokeza kwa wingi kushiriki katika zoezi la uandikishaji na uendelezaji wa daftari la kudumu la wapiga kura. Aidha, napenda kuwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kushiriki katika kazi hii inayoendelea kwa amani na utulivu mkubwa, jambo ambalo limeipa nafasi Tume ya Uchaguzi kuendelea na kazi hiyo bila ya usumbufu wowote.

Mhe. Spika**,** nachukua fursa hii kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba zoezi la uchumaji wa zao la karafuu kwa msimu huu wa 2013 limeanza na linaendelea vyema. Hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2013, jumla ya tani 1,063 zimeshanunuliwa katika vituo vyetu vya Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*). Matarajio ya ununuzi wa karafuu kwa msimu huu ulioanza mwanzoni mwa mwezi wa Julai, 2013 ni kupata tani 4,016. Napenda kuwaarifu wakulima wote wa zao la karafuu Unguja na Pemba kwamba *ZSTC* imejitayarisha vyema kuhakikisha vifaa vyote muhimu vinavyohitajika kwa uchumaji wa zao la karafuu vinapatikana nchini bila usumbufu wowote. Aidha, *ZSTC* imejipanga vizuri kununua karafuu zote zitakazo wasilishwa vituoni.

Mhe. Spika**,** napenda kuwapongeza sana wakulima wetu wa karafuu kwa kuendelea kuiamini serikali yao na kuuza karafuu zao katika vituo vya *ZSTC* kwani wamekuwa wakifanya hivyo kwa moyo wao wa uzalendo kwa Taifa lao. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wananchi wote wazidi kushirikiana na serikali yao katika kuwafichua wale watu wachache wenye nia ya kuendeleza magendo ya karafuu na kuhujumu uchumi wa nchi yetu. Watu hawa hawaitakii mema nchi yetu na hivyo kuna ulazima wa kupambana nao kwa nguvu zetu zote. Serikali tayari inayo taarifa ya kuwepo kwa watu hawa ambao wameibuka na mbinu mpya ya kuendeleza kuhujumu uchumi wa nchi yetu kwa kuwadhulumu wakulima wetu na kusafirisha karafuu zetu kwa njia ya magendo.

Mhe. Spika**,** kama tunavyoelewa kwamba Zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi lililofanyika mwishoni mwa mwezi wa Septemba, 2012 nchini kote liliendeshwa kwa mafanikio makubwa, na hivi sasa Taifa letu la Tanzania linajulikana kuwa na jumla ya idadi ya watu milioni 44,928,923. Kati ya idadi hiyo, Milioni 43,625,354 wapo Tanzania Bara na 1,303,569 wapo hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Spika**,** pamoja na kutolewa idadi ya jumla ya wananchi wa Tanzania, hivi karibuni Ofisi ya Taifa ya Takwimu (*NBS*) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (*OCGS*) imefanya uzinduzi wa Kitabu cha Pili cha idadi ya watu cha umri na jinsia, ambacho kitasaidia katika kupanga mikakati mbali mbali ya kimaendeleo. Aidha, Ofisi zetu hizi za Takwimu zimepanga kutoa Kitabu cha Tatu kuhusu takwimu za watu wenye ulemavu hivi karibuni.

Mhe. Spika**,** naomba kutoa wito kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, Taasisi mbali mbali na wananchi kwa ujumla kuzitumia Takwimu hizi kwa shughuli mbali mbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika**,** naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba hatua ya kuweka miundombinu ya Mkonga wa Mawasiliano inaendelea vyema na hivi sasa kazi zinazofanyika ni kufikisha miundombinu hiyo katika Wizara na Taasisi nyengine za Serikali. Kwa upande wa Unguja kazi hiyo imekwishafanyika kwa asilimia 80 ya kazi yote iliyokusudiwa ya kufikisha huduma hiyo muhimu kwa Taasisi 84 zilizochaguliwa katika hatua ya awali.

Mhe. Spika**,** kwa upande wa Pemba kazi ya upimaji imeanza na wakati wowote kazi ya uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano itaanza. Lengo ni kukamilisha kazi yote kwa Unguja na Pemba ifikapo Disemba, 2013. Kazi hii ya uwekaji wa miundombinu inafanyika kwa makubaliano baina ya Serikali na Kampuni ya simu za mkononi ya *Zantel*. Katika makubaliano hayo Kampuni ya *Zantel* ndio itakuwa mratibu mkuu wa uendeshaji, na usimamizi wa matengenezo ya miundombinu iliyowekwa pamoja na kufanya biashara kupitia mtandao huo. Wakati serikali kupitia Idara ya Mawasiliano itakuwa na jukumu la ufuatiliaji na umiliki wa miundombinu hiyo ya mawasiliano.

Mhe. Spika**,** baada ya kukamilika mradi huu wa uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano, serikali itakuwa imepiga hatua kubwa katika eneo hili la Afrika Mashariki katika masuala ya mawasiliano. Hatua hiyo itaiweka Zanzibar katika ramani ya dunia ya kuwa na miundombinu ya *ICT* yenye uwezo wa kutoa huduma za mawasiliano ya elektroniki katika sekta mbali mbali ikiwemo afya, biashara, elimu, kilimo pamoja na uendeshaji wa Serikali *(E-Government)* na mawasiliano katika jamii *(e-community).*

Mhe. Spika**,** serikali inakusudia kuendelea kutoa taaluma kwa watumishi wa umma na jamii kuhusu matumizi ya *ICT* ili kujenga jamii yenye muamko na uelewa wa masuala haya muhimu kwa maendeleo ya jamii na uchumi wa nchi yetu. Kukamilika kwa mradi huu pia kutapunguza gharama kwa kiasi kikubwa za huduma za mtandao na mawasiliano na hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji huduma na uzalishaji.

Mhe. Spika**,** kama sote tunavyoelewa nchi yetu hivi sasa imo katika shamra shamra za Sherehe za kuadhimisha Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, maadhimisho ambayo yalizinduliwa rasmi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein tarehe 15 Agosti, 2013 na yatafikia kilele chake tarehe 12 Januari, 2014. Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Halmashauri ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa inaendelea vyema na matayarisho kwa ajili ya maadhimisho hayo.

Mhe. Spika, miongoni mwa mambo yanayochukuliwa hatua kwa ajili ya maadhimisho hayo ni ujenzi wa Mnara wa Kumbukumbu ya Miaka 50 ya Mapinduzi unaoendelea kujengwa katika eneo la Michenzani mbele ya Jumba la Maendeleo nambari 2. Ujenzi wa mnara huo mbali ya kuwa ni kielelezo cha mafanikio ya maendeleo ya nchi yetu yanayotokana na Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964. Pia, unakusudiwa kuwa ni kichocheo cha kuleta haiba nzuri ya eneo la Michenzani kitakachovutia watu kutoka ndani na nje ya nchi kutembelea eneo hilo na hivyo kukuza fursa za biashara na kuwapatia vijana fursa za ajira.

Aidha, sherehe hizi zinakusudiwa kujumuisha uwekaji wa jiwe la msingi na uzinduzi wa miradi ya maendeleo ipatayo 150, kufanyika maonesho ya mafanikio ya miaka 50 ya Mapinduzi katika viwanja vya Beit el Ras, pamoja na kuwepo ngoma za asili na urushaji wa fash-fash siku ya mkesha wa kuamkia siku ya kilele yaani tarehe 12 Januari, 2014.

Mhe. Spika**,** katika sherehe za Mapinduzi kutimia miaka 49, niliweka nanga ya msingi kuanzisha ujenzi wa chumba cha hoteli kilioko chini ya bahari katika Hoteli ya *Manta Resort*, Kaskazini, Pemba. Nafurahi kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba chumba hicho, sasa kimekamilika na kinatarajiwa kuzinduliwa katika shamra shamra ya sherehe za Mapinduzi Matukufu kutimia miaka 50.(*Makofi*).

Kukamilika kwa mradi huu wa aina yake, Mhe. Spika**,** ni kielelezo cha Mapinduzi katika sekta ya utalii. Chumba hiki kilioko ndani ya maji baharini ni cha mwanzo cha aina yake kwenye nchi za Bahari ya Hindi, kinatarajia kuitangaza sana Zanzibar kiutalii.

Ni vyema wawekezaji wa sekta ya utalii wakafikiria miradi ambayo ina hadhi kubwa na ambayo itaitangaza nchi yetu kwa kiwango kikubwa zaidi.

Mhe. Spika, katika vikao vilivyopita vya Baraza la Wawakilishi, waliiagiza serikali kuhakikisha kwamba Uwanja wa Amani unatengenezwa ili sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu zifanyike kwenye uwanja wenye hadhi na sherehe hizo. Kwa kuzingatia maagizo hayo ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, Serikali iliiagiza Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kutekeleza agizo hilo.

Naomba kuwaarifu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba, kiwanja cha Amani kiko katika matengenezo ya mwisho yaliyokusudiwa. Kwa hivi sasa:

1. Kiwanja hicho kinamaliziwa kujengwa kwa kuwekwa kifusi na kokoto ili kiwe imara.

2. Nyasi bandia zitawasili nchini wakati wowote kuanzia sasa na mategemeo yetu ni kwamba ifikapo tarehe 12 Disemba, 2013, Kiwanja cha Amani kitakuwa kiko tayari kwa ajili ya sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwaomba viongozi na wananchi wote kushiriki kikamilifu katika maadhimisho haya kwani sherehe hizi ni zetu sote na ni vyema kutoa taswira ya umoja na mshikamano wetu ambao ndio kivutio kikuu kwa kukuza utalii na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika nchi yetu. Ni kitu cha kujivunia kwa nchi yetu kuendelea kubaki katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano katika kipindi chote cha miaka 50 tokea kufanyika kwa Mapinduzi ya mwaka 1964. Namuomba Mwenyezi Mungu atudumishie mafanikio haya ili vizazi vyetu vijavyo viweze kufaidika na mafanikio haya. Kauli mbiu ya maadhimisho haya ni "Tudumishe Amani, Umoja na Maendeleo ambayo ni Matunda ya Mapinduzi yetu – Mapinduzi Daima."

Mhe. Spika, katika mkutano huu wa 13, Baraza lako Tukufu lilikamilisha mambo makuu matatu yafuatayo:

i. Kujibu maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe.

ii. Uwasilishwaji wa miswada minne (4) ya Sheria ambayo ina umuhimu mkubwa kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu.

iii. Uwasilishwaji wa Taarifa ya Serikali juu ya utekelezaji wa ripoti za Kamati Teule juu ya Shirika la Umeme la Zanzibar na Baraza la Manispaa la Zanzibar.

Mhe. Spika**,** katika Mkutano huu maswali ya msingi yapatayo 71 na maswali yapatayo 157 ya nyongeza yameulizwa na Waheshimiwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri wa Sekta husika. Nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walioiuliza maswali ya msingi ambayo yalikuwa na lengo la kudadisi utekelezaji na ufanisi wa shughuli za serikali na kuielimisha jamii. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa majibu sahihi ambayo yalikidhi haja na kuwaondolea wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika**,** Mswada wa mwanzo uliowasilishwa ni Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria mbali mbali za Ardhi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, mpango wa MKUZA II umeeleza kuwa ifikapo mwaka 2015 asilimia 50 iwe imesajiliwa. Aidha, Serikali pia imetoa tamko kuwa majengo ya Taasisi za Serikali na maeneo yote ya serikali yasajiliwe na kupatiwa hatimiliki. Katika utekelezaji wa zoezi hilo kwa kuanzia na maeneo ya Mji Mkongwe imeonekana kuwa Sheria ya Ardhi Nambari 12 ya mwaka 1982 haitoi nafasi kwa Taasisi kumiliki hati ya matumizi.

Kwa upande mwengine marekebisho haya pia yamekuja baada ya kuwa na wananchi ambao wanapewa ardhi na serikali kuidai serikali ilipe fidia ya soko la ardhi pale serikali inapotakiwa kuchukua ardhi hiyo.

Mhe. Spika**,** jambo hili limekuwa likiitia hasara serikali ikizingatiwa kuwa wananchi wamepewa haki ya matumizi ya ardhi hiyo kwa kulipia fedha kidogo sana.

Mhe. Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kurekebisha mapungufu yaliyoonekana katika baadhi ya Sheria za Ardhi. Baadhi ya marekebisho hayo yataondoa mzigo mkubwa kwa serikali kwa kulipa bei ya soko pale inapofuta hati ya matumizi ya ardhi kwa viwanja vilivyotolewa na serikali.

Mhe. Spika, wakichangia Mswada huu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walieleza wasi wasi wao juu ya Taasisi za Serikali zilizopewa mamlaka ya kumilikisha ardhi kwamba zinachangia kwa kiasi kikubwa kuendeleza migogoro ya ardhi. Pia, wameishauri serikali kufanya tathmini ya mipaka ya maeneo yake ili kuondosha mivutano na utata wa umiliki wa ardhi unaoweza kujitokeza na kuleta athari kwa nchi yetu hapo baadae.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kwa mara nyengine tena kuwasihi viongozi pamoja na wananchi waelewe kuwa mwenye dhamana ya kugawa ardhi ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kwa maana hiyo Masheha, Madiwani, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wajibu wao ni kuthibitisha uwepo wa eneo la ardhi linalohitajika. Niwaombe sana viongozi wenzangu kuwa suala la kugawa ardhi waliache mara moja kwa dhamira njema ya kujenga nchi yetu kwa kuepuka kuendelea kuwa na migogoro ya ardhi ambayo inaleta bughdha kwa wananchi wetu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, Mswada wa Pili wa Sheria uliojadiliwa katika Mkutano wa 13 wa Baraza lako Tukufu ni Mswada wa Sheria wa kuanzisha Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara na Mambo Yanayohusiana na Hayo. Madhumuni ya Mswada huu ni kuanzisha chombo cha kusimamia utekelezaji wa mabadiliko ya mfumo wa utoaji wa leseni za biashara – Zanzibar. Chombo hiki kitaweka misingi imara ya kuendesha biashara na utaratibu thabiti wa utoaji leseni za kibiashara, jambo ambalo litasaidia kujenga uchumi kwa msingi wa nguvu za soko.

Mhe. Spika, katika michango yao Waheshimiwa Wajumbe, walishauri kuanzishwa kwa kituo maalum kitakachohusika na utoaji wa leseni na vibali. Waheshimiwa Wajumbe waliendelea kutoa michango yao kwa kueleza kuwa utoaji wa leseni za biashara uzingatie usahihi, usafi, usalama pamoja na afya kwa wafanya biashara. Aidha, walishauri kupunguzwa kwa gharama za utoaji wa mizigo bandarini.

Vile vile, Waheshimiwa Wajumbe walishauri kufanywe uhakiki wa maduka yote nchini ili kuweza kusaidia serikali kukusanya mapato yake vizuri. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa maduka bubu nchini jambo ambalo huinyima serikali mapato yake. Pia,

Wajumbe waliishauri serikali izingatie suala la mikopo kwa wafanya biashara wadogo wadogo ili kuwapatia wafanya biashara hao mitaji na kuanzisha na kuendeleza shughuli zao za kiuchumi na kujiletea maendeleo.

Mhe. Spika**,** nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao mizuri iliyoufanya Mswada wetu wa Sheria kuwa bora zaidi. Hata hivyo, napenda kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba tunayo Sheria ya Usimamizi wa Biashara ambayo ndio iliyotoa mamlaka kwa Taasisi husika juu ya ukusanyaji wa mapato na utoaji wa leseni na vibali. Aidha, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba gharama za utoaji wa mizigo bandarini zinatozwa kwa mujibu wa aina ya mzigo unaotolewa.Vile vile, masharti ya utoaji wa leseni za biashara yanazingatia vipimo vyote ikiwemo afya, usalama na usafi wa wafanya biashara wenyewe.

Mhe. Spika, **s**erikali italifanyia kazi kikamilifu pendekezo la Waheshimiwa Wajumbe la kufanya zoezi la uhakiki wa maduka yaliyokuwepo nchini, ili kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya serikali na kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuwapatia mikopo wafanyabiashara wadogo wadogo, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba tayari zipo juhudi mbali mbali zinazofanywa na serikali zinazolenga kuongeza fursa za upatikanaji wa mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo. Miongoni mwa juhudi hizo ni mikopo ya JK na AK na kuimarishwa kwa vikundi vya akiba na vya kuweka na kukopa. Kwa baadhi ya maeneo vikundi hivi vinafanya vizuri.

Mhe. Spika, Mswada wa Tatu uliojadiliwa ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Biashara ya Zanzibar Nam. 4 ya 1989 na kuweka Sheria Mpya ya Biashara, ili kuimarisha biashara ya Zanzibar na mambo yanayohusiana nayo. Madhumuni ya Mswada huu ni kukuza biashara ya Zanzibar kwa kuweka mfumo wa kisasa wa biashara ili kukidhi mahitaji muhimu yatakayoweza kukuza kipato kwa serikali, lakini pia kuleta tija na mafanikio kwa wafanya biashara.

Mhe. Spika, wakati wakichangia Mswada huu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameishauri serikali kuimarisha taasisi zinazohusika na biashara ili kuweka mazingira mazuri ya biashara hapa nchini.

Mhe. Spika, biashara yenye tija ni miongoni mwa mihimili mikuu ya uchumi wa taifa letu. Kama tunavyoelewa, historia ya maendeleo ya kiuchumi Zanzibar inatokana na sekta ya biashara na asilimia kubwa ya wakaazi wa Zanzibar huendesha maisha yao kupitia sekta hii. Napenda kutoa wito kwa wafanya biashara wote kuendesha shughuli zao kwa kuzingatia sheria za nchi na kufanya biashara zao kwa umakini zaidi ili kuongeza tija na kipato kwao wao binafsi pamoja na kuiongezea serikali mapato yake inayostahiki.

Mhe. Spika, Mswada wa Nne uliojadiliwa ni Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kuandikwa Upya Sheria inayohusu Kampuni na Jumuiya nyengine, Kuweka Masharti Madhubuti Zaidi ya Uratibu na Udhibiti wa Kampuni, Jumuiya na Mambo Yanayohusiana na Hayo. Madhumuni ya mswada huu ni kuwa na masharti yatakayowezesha kuwa na uratibu na udhibiti mzuri wa shughuli za usajili wa taasisi ili kuendeshwa kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, katika kuchangia mswada huu Waheshimiwa Wajumbe walishauri kuwe na utaratibu wa kukaguliwa kwa makampuni yanayotaka kupatiwa usajili. Vile vile, Waheshimiwa Wajumbe walieleza wasi wasi wao, kuwa kuna baadhi ya wamiliki wa makampuni wanaghushi nyaraka ili kampuni zao zionekane zimesajiliwa.

Mhe. Spika, tukielekea katika utekelezaji wa azma yetu ya kuimarisha uchumi na sekta za biashara ni jambo la msingi sana kwa jamii yetu kuzingatia umuhimu wa uaminifu na uadilifu katika shughuli za kiuchumi na kibiashara. Kwa msingi huo, napenda niungane na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kukemea tabia hii potofu ya kughushi nyaraka za serikali kwa maslahi binafsi kwa baadhi ya wafanyabiashara. Naomba kuchukua fursa hii kuziamuru taasisi husika kuchukua hatua kali za kisheria pale itapobainika mfanya biashara amekiuka taratibu za kisheria katika kuwasilisha nyaraka za usajili katika vyombo husika.

Mhe. Spika, katika kikao hiki cha 13 cha Baraza lako tukufu, serikali iliweza kutekeleza jukumu lake la kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi juu ya utendaji wa Shirika la Umeme (*ZECO*) na Baraza la Manispaa. Taarifa zote mbili zimeeleza kwa kina jinsi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilivyoyapokea na kuyatekeleza mapendekezo yote ya Kamati Teule za Baraza.

Mhe. Spika, katika taarifa zilizotolewa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako walionyesha kutoridhika na hatua zilizochukuliwa na serikali katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Kamati Teule na hasa juu ya hatua za kisheria na kinidhamu zilizochukuliwa kwa watendaji waliotuhumiwa kufanya makosa. Wajumbe walionyesha wasi wasi wao wa kwamba hatua za kinidhamu zilizochukuliwa ni ndogo ukilinganisha na makosa yaliyotendeka. Aidha, suala la kufikisha mashauri ya hoja zilizotolewa kwa Jeshi la Polisi kwa uchunguzi zaidi baadhi ya wajumbe walionesha kwamba halikua na umuhimu kwa vile tayari kamati hizo zilikuwa zimeshafanya uchunguzi wa kina.

Mhe. Spika, naamini Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wana imani kubwa na serikali yao na wanaitakia mema nchi yetu katika kuiletea maendeleo kwa faida ya wananchi ambao ndio wanaowawakilisha katika Baraza hili. Kwa imani hiyo hiyo ambayo

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanayo. Pia, wataamini kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa ina nia thabiti ya kuondosha maovu ya aina zote katika utumishi wa umma, kuimarisha utendaji na uwajibikaji na kuleta ufanisi na tija katika kazi.

Ndio maana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, wakati akiwasilisha taarifa za serikali kuhusu hoja mbali mbali zilizotolewa na Kamati Teule, alieleza kwamba serikali imepokea mapendekezo ya Kamati Teule kwa moyo mkunjufu na kushukuru Wajumbe wa Kamati zote kwa kuibua hoja ambazo ni muhimu kufanyiwa kazi katika kuimarisha uendeshaji wa vyombo vinavyohusika. Aidha, kupitia maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, serikali iliahidi kuyatekeleza mapendekezo yaliyotolewa kwa misingi ya haki na kwa nia ya kuongeza kasi ya uwajibikaji na kuondoa ubadhirifu wa mali za umma.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaelewa fika kuwa hatua zozote zinazohitajika kuchukuliwa dhidi ya watendaji wanaotuhumiwa kufanya makosa ya jinai ni lazima tuhuma hizo kwanza kufikishwa katika Jeshi la Polisi kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na uchunguzi huo unapokamilika taarifa hufikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kufunguliwa mashtaka mahkamani. Huu ndio utaratibu wa kuchukua hatua za kisheria ambao tumeuweka wenyewe na hivyo ni lazima kufuatwa. Serikali imefuata utaratibu huo kwa kulitaka Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ikiwa ni hatua muhimu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Teule kwa kufuata misingi ya sheria na kuondoa hisia za upendeleo. Aidha, hatu za kinidhamu zilizochukuliwa zimefanyika kwa kufuata matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 9 ya mwaka 2012.

Mhe. Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba serikali haitamuonea huruma mtendaji yoyote atakae bainika ndani ya utaratibu wa sheria kuwa ametenda kosa na hivyo itaiachia sheria kuchukua mkondo wake pasi na kuingiliwa. Hakuna mtendaji yeyote au kiongozi yeyote ambaye atakuwa juu ya sheria kwa maovu atakayoyafanya kuihujumu serikali au kuuhujumu uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, nawashukuru sana Wajumbe wote waliochangia ripoti hizi kwa uwazi. Ni ukweli michango ilikuwa mikali na hata baadhi ya wajumbe kutoziunga mkono hoja hizo. Hasa ile taarifa inayohusu *ZECO*. Hata hivyo, baada ya maelezo ya kina ya Waheshimiwa Mawaziri hoja hizo zimepokelewa.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwasihi watendaji wote wa taasisi za umma kuachana na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea, na badala yake kufanya kazi kwa mujibu wa sheria za nchi pamoja na kuzingatia maadili ya kazi na kuepukana na ubadhirifu wa aina yoyote wa mali za serikali. Serikali haitavumilia vitendo vyovyote vitakavyokwenda

kinyume na sheria za nchi. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuipa nafasi serikali kutekeleza mapendekezo waliyoyatoa kwa misingi ya kuaminiana na kushirikiana katika kupiga vita maovu ndani ya utumishi wa umma.

Mhe. Spika, katika kikao kilichopita, Waheshimiwa Wawakilishi walikuwa wakilalamika kuhusiana na kuyumba na kukatika kwa matangazo ya televisheni hasa kwa Pemba na Dar es Salaam.

Ni kweli katika majaribio ya televisheni kutoka Analogi kwenda Digitali iligundulika kuwepo na kasoro za kiufundi kwenye mnara wa Nungwi unaopeleka mawimbi ya Digital Televisheni Pemba, lakini pia mnara uliowekwa vifaa vya Digital Televisheni Mkoa wa Kaskazini Pemba ulioko Konde, haukuweza kumudu kufikisha mawimbi sehemu zote za Mkoa wa Kaskazini, Pemba.

Kampuni ya Agape iliyopewa kazi ya kuweka miundombinu ya Digitali imeliona tatizo hilo na wameahidi kwamba kasoro hizo zitakuwa zimerekebishwa katika wiki ya mwanzo ya mwezi wa Novemba mwaka huu. Ni mategemeo ya serikali ni kwamba kwa vile sherehe za Mapinduzi za kutimia miaka 50 zinaendelea, wananchi wote wa Mikoa ya Zanzibar wataweza kuona ufunguzi wa miradi mbali mbali kupitia Digital TV yetu kuanzia kipindi hicho cha Novemba.

HITIMISHO

Mhe. Spika**,** kwa mara nyengine tena, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa busara zako na umakini mkubwa katika kuliendesha Baraza letu. Aidha, narudia kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati Teule zote mbili na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kazi zao nzuri katika kusimamia utendaji wa serikali na kwa michango yao yenye lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika utumishi wa umma.

Mhe. Spika, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote waliosaidia kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Pia, nawashukuru waandishi wa habari na wakalimani wa lugha ya alama kwa kazi yao nzuri ya kuwapatia taarifa wananchi kuhusu majadiliano ya Baraza katika mkutano huu wa 13. Aidha, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Baraza wakiongozwa na Katibu wa Baraza kwa kazi nzuri wanazofanya za kuwahudumia Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, mkutano wetu huu umefanyika kwa mafanikio makubwa na umeendelea kuidhihirishia dunia juu ya kukomaa kwa demokrasia katika Baraza na katika nchi yetu na tumezidi kujenga matumaini makubwa kwa wananchi juu ya umakini wa Baraza na

Serikali katika kusimamia na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa faida ya wananchi na taifa letu.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba serikali yao chini ya uongozi madhubuti wa Rais wetu mpendwa, Dkt. Ali Mohammed Shein, itachukuwa kila juhudi inayowezekana kuhakikisha kwamba inaimarisha utendaji na uwajibikaji katika taasisi za umma na kamwe haitowavumilia watendaji wazembe, wababaishaji, wezi na wabadhirifu kutuchafulia hatua zetu za kuiletea maendeleo nchi yetu na kufikia azma yetu ya kuwa na maisha bora kwa wananchi wetu wote na kuwaondolea umasikini. Tuendelee kushirikiana na kuaminiana kwa pamoja tutashinda vita hivi.

Mwisho, Mhe. Spika, nawatakia wajumbe wote wa Baraza lako tukufu safari njema ya kurejea vituoni mwao, ili kuungana na wananchi wao katika ujenzi wa uchumi wa majimbo yao kwa maslahi na maendeleo ya wananchi wenyewe na taifa kwa jumla.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako tukufu hadi siku ya Jumatano, tarehe 11 Disemba, 2013 saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukuwe nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa hotuba nzuri ambayo ina maudhui ya kujenga umoja, amani na utulivu pamoja na maendeleo ya nchi yetu. Hoja imetolewa kwamba mkutano huu tuuahirishe mpaka tarehe 11 Disemba, 2013. Hapana shaka mnaelewa kwamba kipindi utaona ni kifupi, lakini tumezingatia kwamba mbele kutakuwa kuna shughuli kubwa sana muhimu ya Bunge la Katiba. Sasa baada ya mawasiliano ya hapa na pale ikaonekana itabidi tufupishe muda katika utaratibu wetu wa kawaida wa kuitisha mikutano inayofuata, baada ya mkutano huu wa kumi na tatu kumalizika. Hiyo, itawezesha basi shughuli zetu za Bunge la Katiba, lakini na mikutano yetu ya kawaida iweze kufanyika.

Tunawashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano makubwa ambayo mmetupa, katika kufanikisha shughuli za mkutano wetu huu wa kumi na tatu. Bila ya kuchukua muda basi, sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji, wale wanaokubaliana na hoja ya kuliakhirisha Baraza hili hadi tarehe 11 Disemba, 2013 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Basi baada ya hayo sasa, niahhirishe mkutano huu mpaka tarehe 11 Disemba, 2013 saa 3:00 barabara za asubuhi.

WIMBO WA TAIFA

(Saa 11:47 Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 11/12/2013 saa 3:00 za asubuhi)